

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA NNE

Kikao cha Kwanza – Tarehe 31 Agosti, 2021

(Mkutano Ulianiza Saa Tatu Asubuhi)

**WIMBO WA TAIFA NA WIMBO WA JUMUIYA YA AFRIKA
MASHARIKI**

*(Hapa Kwaya ya Bunge iliimba Wimbo wa Taifa na Wimbo
wa Jumuiya ya Afrika Mashariki)*

D U A

Spika (Mhe. Job Y. Ndugai) Alisoma Dua

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, naomba tukae.

TAARIFA YA SPIKA

Waheshimiwa Wabunge, Taarifa ya Spika chini ya Kanuni ya 39(2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Juni, 2020.

Waheshimiwa Wabunge, kwa masikitiko makubwa nichukue fursa hii kuwataarifu kwamba aliyekuwa Mbunge mwenzetu Mheshimiwa Elias John Kwandikwa na Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa alifariki tarehe 2 Agosti, 2021 katika Hospitali ya Taifa ya Muhimbili alipokuwa akitibibiwa na baadae kuzikwa tarehe 9 Agosti, 2021 jimboni kwake Ushetu.

Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Kwandikwa awali alipelekwa katika Hospitali ya Jeshi ya Lugalo na baadae kuhamishiwa Hospitali ya Taifa ya Muhimbili, Dar es

Salaam ambapo aliendelea kupata matibabu mpaka mauti ilipomkuta.

Waheshimiwa Wabunge kwa kuwa leo ni siku ya kwanza Bunge linakutana tangu msiba huo mzito utokee, kwa heshima naomba tusimame kwa dakika moja ili kukumbuka na kumuombea Mwenyezi Mungu ampokee na ampumzishe kwa amani, naomba tusimame.

*(Hapa Wabunge walismama kwa dakika moja
kumkumbuka aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Ushetu na
Waziri wa Ulinzi naJeshi la Kujenga Taifa,
Marehemu Elias J. Kwandikwa)*

SPIKA: Bwana ametoa, Bwana ametwaa, jina lake lihimidiwe.

Waheshimiwa Wabunge, naomba tukae.

Waheshimiwa Wabunge, karibuni tena Dodoma, leo ni siku ya kwanza ya shughuli zetu za Mkutano huu wa Nne, Kikao chetu cha Kwanza cha Mkutano wa Nne tangu Bunge hili la Kumi na Mbili lianze. Katibu

NDG. NENELWA MWIHAMBI, ndc – KATIBU WA BUNGE:

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa mezani na:-

MHE. SHALLY J. RAYMOND K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA BUNGE YA HAKI, MAADILI NA MADARAKA YA BUNGE:

Taarifa ya Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge Kuhusu uchunguzi wa Tuhuma zinazomkabili Mheshimiwa Josephat Mathias Gwajima, Mbunge za kuvunja Haki za Bunge, kudharau Mamlaka ya Bunge na kugonganisha Mihimili.

Taarifa ya Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge kuhusu uchunguzi wa tuhuma zinazomkabili Mheshimiwa Jerry William Silaa za Kuvunja Haki za Bunge, kuchonganisha wananchi na Bunge, wananchi na Serikali kwa kusema uwongo.

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Shally Raymond, tunakushukuru. Katibu.

NDG. NENELWA MWIHAMBI, *ndc* – KATIBU WA BUNGE:

MASWALI NA MAJIBU

SPIKA: Maswali, swali la kwaza litaulizwa na Mheshimiwa Ally Juma Makoa, Mbunge wa Kondoa Mjini, Mheshimiwa Makoa tafadhali uliza swali lako. Kwa niaba yake, Mheshimiwa Cecilia Paresso, kama kuna mtu amewasha *microphone* azime.

Na. 1

Ukarabati au Ujenzi wa Miundombinu ya Hospitali

MHE. CECILIA D. PARESSO K.n.y. MHE. ALLY J. MAKOA
aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itakarabati au kujenga Hospitali mpya ya Halmashauri ya Mji wa Kondoa kwa kuwa Hospitali iliyopo ni ya muda mrefu na miundombinu yake ni chakavu.

SPIKA: Majibu ya swali hilo TAMISEMI, Mheshimiwa Naibu Waziri Dkt. Dugange tafadhali.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA
SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais – TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ally Juma Makoa, Mbunge wa Kondoa Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua uwepo wa hospitali kongwe na chakavu katika baadhi ya Halmashauri nchini ikiwemo Hospitali ya Halmashauri ya Mji wa Kondoa.

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea na ujenzi wa Hospitali za Halmashauri 102 ambazo zipo katika hatua mbalimbali za ujenzi. Kwa kuwa, bado kuna Halmashauri 28 zisizo na Hospitali ya Halmashauri, Serikali katika mwaka wa fedha 2021/2022 imetenga kiasi cha shilingi bilioni 14 ili kuanza ujenzi katika Halmashauri hizo.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeweka kipaumbele kwa kuanza ujenzi katika Halmashauri hizo na baada ya hapo ukarabati wa Hospitali chakavu ikiwemo Hospitali ya Halmashauri ya Mji wa Kondoa utafanyika. Ahsante sana.

SPIKA: Mheshimiwa Paresto swali la nyongeza.

MHE. CECILIA D. PARESSO: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi niweze kuuliza maswali madogo mawili ya nyongeza kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, pamoja na kazi ya ukarabati katika hospitali mbalimbali kongwe hapa nchini lakini bado kumekuwa na upungufu mkubwa wa watumishi wa afya.

Je, Serikali ina mpango gani kuhakikisha kwamba mapungufu hayo yanakidhi haja iliyopo kwa maana ya idadi ya watumishi wanaotakiwa?

Mheshimiwa Spika, swali la pili; ujenzi wa hospitali au ukarabati wa zahanati, vituo vya afya na hizo hospitali ni pamoja na kuhakikisha mambo muhimu ya madawa, vitendanishi yanapatikana katika hospitali zetu. Je, Serikali inahakikisha vipi kwamba upatikanaji wa madawa yote muhimu yanapatikana katika hospitali zetu na katika vituo vya afya na zahanati zetu. (*Makofii*)

SPIKA: Majibu ya maswali hayo Mheshimiwa Naibu Waziri TAMISEMI tafadhali.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):
Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Cecilia Paresso, Mbunge wa Viti maalum kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba Serikali kwa kuwalijali na kuthamini sana afya za wananchi imeendelea kujenga vituo vya afya kote nchini na kwa kweli kuna upungufu wa watumishi kwa takribani asilimia 45. Serikali imeweka mipango thabiti ya kuhakikisha tunaendelea kuajiri watumishi katika vituo vya afya, zahanati na hospitali za Halmashauri na ndiyo maana mwezi wa Tano hadi wa Sita tulikuwa na ajira za watumishi wa afya 6,324 na watumishi hao wamekwisha ajiliwa tayari wamepelekwa kwenye vituo vya huduma za afya.

Mheshimiwa Spika, zoezi hili la kuendelea kuajiri watumishi ni endelevu, kwa hiyo nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali inatambua na itaendelea kuhakikisha kwamba inaanjiri watumishi kwa awamu ili kupunguza uhaba wa watumishi katika vituo hivyo.

Mheshimiwa Spika, pili; ni kweli kwa sababu ya ongezeko la vituo vya huduma za afya kumekuwa na upungufu wa baadhi ya dawa muhimu katika vituo vyetu na Serikali imeendelea kupeleka fedha Bohari Kuu ya Dawa mpaka Juni tarehe 30 mwaka huu, jumla ya bilioni 120 zilikuwa zimepelekwa Bohari Kuu ya Dawa kwa ajili ya kununua dawa kupeleka katika vituo vyetu.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka huu wa fedha 2021/2022 fedha zimetengwa zaidi ya bilioni 280 kwa ajili ya kuhakikisha kwamba dawa zinapelekwa katika vituo vyetu. Kwa hivyo, nimhakikishie kwamba suala hilo litaendelea kutekelezwa kwa ufanisi unaotakiwa ili dawa zipatikane katika vituo vyetu. Ahsante sana.

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na swali la pili la Mheshimiwa Bahati Kenneth Ndingo, Mbunge wa Viti Maalum, uliza swali lako Mheshimiwa Bahati.

Na. 2

Uanzishwaji wa Hati Fungani za Serikali za Mitaa

MHE. BAHATI K. NDINGO aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itakamilisha uanzishwaji wa hati fungani za Serikali za Mitaa?

SPIKA: Majibu ya swali hilo Mheshimiwa, bado tupo TAMISEMI tafadhali.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Bahati Kenneth Ndingo, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, wakati wa kuwasilisha hotuba ya bajeti ya Serikali ya mwaka wa fedha 2021/22 Waziri wa Fedha na Mipango aliwasilisha kuhusu kuanzisha hati fungani za Halmashauri. Kifungu cha 92 ya hotuba yake ilieleza, katika jitihada za kupanua wigo wa vyanzo vya mapato rasilimali fedha Serikali itaangalia uwezekano wa kutumia hati fungani zitakazotolewa na Halmashauri za Manispaa na Majiji kama njia mbadala ya kupata rasilimali fedha kwa ajili ya miradi ya kimkakati.

Mheshimiwa Spika, hatua hii itapunguza mzigo kwenye mfuko mkuu wa Hazina ya Serikali hasa kwa Halmashauri zenyne miradi ambayo imefanyiwa upembuzi yakinifu na kuwa na uhakika wa uwezo wa miradi hii kurejesha kwa faida kwa maana ya *bankable projects*.

Mheshimiwa Spika, Serikali kwa kushirikiana na Mfuko wa Maendeleo wa Umoja wa Mataifa (*United Nations Capital Development Fund – UNCDF*) na Mamlaka ya Usimamizi wa Masoko ya Mitaji (*Capital Markets and Securities Authority-CMSA*) imeanza mchakato wa kupitia miradi ya Mamlaka za Serikali za Mitaa ili kuhakikisha Halmashauri za Miji, Manispaa na Majiji yatakayokidhi vigezo na masharti ya matumizi ya hati fungani yanaanza kutumia utaratibu huu katika mwaka huu wa fedha 2021/2022. Ahsante sana.

SPIKA: Mheshimiwa Bahati Ndingo.

MHE. BAHATI K. NDINGO: Mheshimiwa Spika, nakushukuru.

Mheshimiwa Spika, ninashukuru Serikali kwa majibu mazuri lakini nina maswali mawili ya nyongeza.

Kwa kuwa Serikali imesema kwamba Halmashauri ambazo zitakidhi vigezo zitaanza kunufaika na hiyo hati fungani, sasa ni vigezo vipi ambavyo Serikali imeviweka kwa Halmashauri kuonekana zinakidhi.

Mheshimiwa Spika, pia kwa kuwa zoezi hili linaanza mwaka huu wa fedha, ni Halmashauri ngapi ambazo tayari zimekidhi vigezo.

Mheshimiwa Spika, ahsante.

SPIKA: Sina hakika kama takwimu hizo atakuwa nazo Mheshimiwa Naibu Waziri lakini basi kwa ujumla wake, majibu ya swali hilo tafadhalii.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Bahati Keneth Ndingo, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kama ambavyo nimetangulia kujibu katika swali la msingi, vigezo ni Halmashauri yoyote ambayo ina miradi ya kiuchumi, kimkakati ambayo imefanyiwa upembuzi yakinifu na kuonesha kwamba ina uwezo wa kurejesha fedha na faida. Kwa hiyo, Halmashauri yoyote ambayo itaibua mradi wowote wa maendeleo ambaa tayari umefanyiwa upembuzi huo wana uwezo wa kutumia hati fungani ili kushirikisha umma na wadau mbalimbali kupata mtaji na kuwekeza na hatimaye kuhakikisha kwamba wanapata miradi ya maendeleo katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, vigezo ndiyo hivyo, ni ile Halmashauri yenye uwezo kwamba miradi yake ina tija na inaweza ikazalisha faida basi watahusika na utaratibu huu wa hati fungani. Ahsante sana.

SPIKA: Tunaendelea Waheshimiwa Wabunge na Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora, swali la Mheshimiwa Dennis Lazaro Londo, Mbunge wa Mikumi, Mheshimiwa Londo uliza swali lako tafadhali.

Na. 3

Watumishi Walioondolewa Kimakosa wakati wa zoezi la Uhakiki wa Vyeti Feki

MHE. DENNIS L. LONDO aliuliza: -

(a) Je, ni Watumishi wangapi wamerejeshwa kazini baada ya kuondolewa kimakosa wakati wa zoezi la uhakiki wa vyeti feki na Wafanyakazi hewa?

(b) Je, ni Watumishi wangapi waliorejeshwa kazini wamelipwa stahiki zao kama mishahara ambayo hawakupata kutohana na kuondolewa kazini?

SPIKA: Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora, Mheshimiwa Deo Ndejembie tafadhali.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI
WA UMMA NA UTAWALA BORA alijibu:-**

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Dennis Lazaro Londo, Mbunge wa Mikumi kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi na Utawala Bora kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Serikali kuptitia ofisi yangu imewarejesha kazini na kuendelea kuwalipa mishahara jumla ya watumishi 4,380 walioondolewa kwenye orodha ya malipo ya mishahara kimakosa wakati wa zoezi la uhakiki wa vyeti vya elimu na watumishi hewa. Idadi hii inajumuisha Watendaji wa Kata, Watendaji wa Vijiji na Watendaji wa Mitaa wapatao 3,114.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuwarejesha watumishi tajwa, Serikali pia ilitoa msamaha wa kuwarejesha kazini watumishi walioondolewa kazini kwa kukosa sifa ya elimu ya Kidato cha Nne na baadaye wakajiendeze na kupata sifa tajwa hadi kufikia mwezi Disemba, 2020 ambao hawakudanganya katika taarifa zao kuwa wana elimu ya Kidato cha Nne au kubainika kughushi vyeti. Pia, mnamo tarehe 07 Mei, 2021 Serikali kuptitia ofisi yangu ilitoa maelekezo na utaratibu kwa waajiri kuhusu namna ya kushughulikia hatima za ajira za watumishi walioondolewa kazini kwa kukosa sifa ya elimu ya Kidato cha Nne pamoja na malipo ya stahiki zao. Napenda kuwakumbusha waajiri wote kukamilisha utekelezaji wa maelekezo hayo kwa haraka na kwa usahihi ili watumishi husika waweze kupata haki zao mapema.

Mheshimiwa Spika, napenda kutumia fursa hii kusisitiza kwamba msamaha uliotolewa unawahu watumishi wale tu walioajiriwa baada ya tarehe 20 Mei, 2004 bila sifa ya elimu ya Kidato cha Nne lakini baadaye wakajipatia sifa za kuajiriwa na haiwahu watumishi walibainika kuwa na vyeti vya kughushi au waliota taarifa za uwongo katika kumbukumbu zao rasmi za kiutumishi. Utaratibu wa kushughulikia watumishi walibainika kughushi vyeti

ulishatolewa awali na Serikali na watumishi wote waliobainika kughushi vyeti hawastahili kurudishwa kazini.

Mheshimiwa Spika, Serikali imelipa madai ya mishahara ya jumla ya shilingi 2,613,978,000 kwa watumishi 1,643 walioreshwa kazini baada ya kuondolewa kwenye orodha ya malipo ya mishahara kimakosa. Uhakiki wa madai yaliyobaki unaendelea na yataendelea kulipwa kwa kadri yanavyohakikiwa.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

SPIKA: Ahsante sana, Mheshimiwa Mbunge wa Mikumi swali la nyongeza Mheshimiwa Londo.

MHE. DENNIS L. LONDO: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa msamaha ultolewa kwa wale wote ambao waliondolewa kazini kwa kukosa sifa ya kidato cha nne na baadaye wakajidendeza kupata sifa hizo; na kuna maeneo ambayo watu hawana mawasiliano ya simu kama Ulingombe, Vidunda, Malolo na Kisanga.

Je, Serikali inatoa tamko gani kwa waajiri kuhakikisha kwamba watu wote ambao wame-*qualify* kurudishwa na hawana taarifa wanapata taarifa hizi kwa wakati na wanarudishwa kazini bila masharti ya ziada?

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa watumishi hawa ambao walishindwa kujidendeza kidato cha nne lakini walikuwa na sifa stahiki wakati wanaajiriwa waliondolewa kazini walitumikia hii nchi kwa uadilifu na uzalendo lakini hawakuwa na kosa mahali zaidi ya maelekezo ya Serikali.

Je, ni lini Serikali inaenda kuhakikisha kwamba malipo yao na stahiki zao zinalipwa?

SPIKA: Majibu ya swali hilo muhimu Mheshimiwa Naibu Waziri Utumishi, Mheshimiwa Deogratius Ndejembia tafadhali

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Dennis Lazaro Londo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, msamaha uliotolewa kwa watumishi hawa ambao walijiriwa baada ya tarehe 20 Mei, 2004 ambapo tangazo la Serikali lilitoka mpaka ifikapo Mei, 2004 watumishi wote wanaoajiriwa Serikalini ni lazima wawe na sifa ya kidato cha nne. Hata hivyo kuna waajiri ambao walijiri watumishi baada ya tangazo lile la Serikali. Tunatambua kwamba haikuwa kosa la wale watumishi walioajiriwa.

Mheshimiwa Spika, sasa Serikali ilitoa maelekezo kupitia Katibu Mkuu Kiongozi kwamba hawa watumishi wote walioajiriwa baada ya tarehe hilo wawe wamejiendeleza na kupata sifa ya kuajiriwa Serikalini, yaani cheti cha kidato cha nne mpaka ifikapo Desemba, 2020. Na waliorejeshwa kazini mpaka kufikia Desemba 2020 ni zaidi ya watumishi 4,335 ambao walirudi kwa sababu walikuwa wamejiendeleza.

Mheshimiwa Spika, sasa kwa wale ambao kama Mheshimiwa Mbunge alivyosema, kwamba hawakupata taarifa popote ya kwamba wajiendeleza na walijiendeleza kabla ya ile *deadline* iliywerekwa basi niwaelekeze waajiri wote nchini kuweza kuliangalia hili kuwachukua watumishi hawa kama walijiendeleza tu kabla ya kufikia Desemba, 2020 lakini hawakupata tangazo la kurejea kazini basi waajiri waweze kuliangalia hilo.

Mheshimiwa Spika, kwenye swali lake la pili aliulizia wale ambao hawakuijendeleza lakini walijiriwa baada ya Mei 2004. Hawa siku ya Mei Mosi Mheshimiwa Rais wetu mama yetu Samia Suluhu Hassan alitoa maelekezo, kwamba watumishi wote waliokuwa na sifa ya elimu ya darasa la saba walipwe stahiki zao kwa sababu hawa hawakughushi wao walijiriwa siyo makosa yao basi stahiki zao kama hawakurejeshwa kazini na kama hawakuijendeleza walipwe. Tayari ofisi yetu ilishatoa waraka kupitia Katibu Mkuu Ofisi ya

Rais Utumishi kwa waajiri wote nchini kuanza kushughulikia hawa wenye elimu ya darasa la saba ambao hawakurejeshwa kazini, na tayari linafanyiwa kazi.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

SPIKA: Asante sana. Nimekuona Mheshimiwa Mbunge mwakilishi wa darasa la saba, Mheshimiwa Musukuma

MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi niulize swal la nyongeza, na nimpongeze pia Mheshimiwa Naibu Waziri kwa kutupandisha daraja kutuita kidato cha saba.

Mheshimiwa Spika, watumishi wa darasa la saba ambao waliondolewa kazini walifanya kazi zao kwa uaminifu, wengine walikuwa watendaji na watu wengine; lakini tamko hili lilitoka na waraka ukatoka mpaka leo asilimia 95 hawajawahi kulipwa wala kuitwa wala kupokelewa tu na waajiri. Sasa ningewomba Mheshimiwa Waziri kama anaweza kutoa *commitment* angalau akatupa kopi ya zile nyaraka sisi Waheshimiwa Wabunge ili tuweze kwenda kutetea wale waliondolewa na hawajapata stahiki zao?

SPIKA: Majibu ya swal hilo Mheshimiwa Naibu Waziri tafadhalii

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swal la nyongeza ya Mheshimiwa Musukuma kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, watumishi ambao hawakujiedeleza mpaka kufika Desemba, 2020 walikuwa kama 1,491, ambao hawakujiedeleza, na hivyo walikosa sifa ya kurejeshwa katika utumishi wa umma.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema awali wakati najibu maswali ya nyongeza ya Mheshimiwa Londo, kwamba Mheshimiwa Rais wetu, mama yetu Samia Suluhu Hassan

alitoa agizo lake siku ya Mei Mosi pale Mwanza. Kwamba hawa 1491 stahiki zao zilipwe; na tayari ofisi yetu ya Utumishi ilishatoa waraka tarehe 21 Mei, 2021 kwa waajiri wote kuanza kuhakiki madeni haya na kuangalia stahiki walizotakiwa kulipwa hawa wa darasa la saba. Naamini baada ya muda mfupi hawa 1491 wataanza kulipwa, kwa sababu ilikuwa ni maelekezo ya Mheshimiwa Rais na hivyo tutalitekeleza kama alioyelekeza yeze Mheshimiwa Rais. Ahsante sana.

SPIKA: Tunahamia Wizara ya Kilimo Waheshimiwa Wabunge swalii la nne linaulizwa na Mheshimiwa Anthony Peter Mavunde Mbunge wa hapa tulipo. Mheshimiwa Mavunde.

Na. 4

Kuliendeleza Zao la Zabibu-Dodoma

MHE. ANTHONY P. MAVUNDE aliuliza:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuliendeleza zao la zabibu Mkoani Dodoma?

SPIKA: Majibu ya swalii hilo muhimu Mheshimiwa Naibu Waziri Kilimo, Mheshimiwa Hussein Mohamed Bashe, tafadhalii.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Anthony Peter Mavunde, Mbunge wa Dodoma Mjini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, uzalishaji wa zabibu kwa sasa ni wastani wa tani 16,000 kwa mwaka ukilinganisha na uwezo uliopo wa kuzalisha zabibu wastani tani 150,000 kwa mwaka. Mahitaji ya mchuzi wa zabibu kwa mwaka ni wastani wa lita milino 15 ambapo uzalishaji wa ndani wa nchi kwa mwaka tunazalisha wastani wa lita milioni 5 na jumla ya lita milioni 10 zinaagizwa kutoka nje zenye thamani ya dola milioni 6. Sasa Serikali imeliingiza zao la zabibu kuwa mingoni mwa mazao

ya kimkakati ambayo yamepewa kipaumbele katika kuendelezwa n Serikali kwa kushirikiana na sekta binafsi.

Mheshimiwa Spika, katika kuendeleza zao la zabibu Serikali imeweke mikakati mbalimbali ikiwemo kuhakikisha upatikananaji wa miche bora kupitia TARI na hal mashauri za wilaya husika, kuimarisha huduma za ughani katika zao la zabibu, kuongeza upatikanaji wa soko kutoka wastani wa asilimia 65 hadi 85, kuongeza tija ya uzalishaji wa tani 6.25 kwa hekta hadi kufika tani 30 ifikapo mwaka 2025. Vilevile kuweka mazingira bora ya uwekezaji katika tasnia ya zabibu, kufufua na kuanzisha mashamba makubwa ya zabibu na kutenga na kulinda ardhi kwa ajili ya kilimo cha zabibu.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kuijengea uwezo TARI kuendelea na utafiti na kuzalisha miche kwa kuongeza bajeti ya utafiti wa mazao ya killmo ikiwemo zao la zabibu kutoka shilingi bilioni 7.3 mwaka 2021 hadi kufika bilioni 11.63 mwaka 2021/2022.

Aidha, Serikali imetenga fedha kwa ajili ya kuwanunulia vitenda kazi Maafisa Ugani ambao hawana vyombo vyaya usafiri katika Mkoa wa Dodoma.

Mheshimiwa Spika, Serikali pia imeweke mkakati wa kufufua mashamba makubwa ya zabibu ambayo uzalishaji wake unasuasua. Katika kutekeleza adhima hiyo Serikali imefufua shamba la Chinangali II lenye ukubwa ekari 602 lilipo Wilaya ya Chamwino kwa kukarabati bwawa la maji na visima vilivyopo shambani.

SPIKA: Mheshimiwa Anthony Mavunde, nimekuona

MHE. ANTHONY P. MAVUNDE: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa nafasi hii ya maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa namna ambavyo ametusaidia sana kuchochea zao hili la zabibu, na kupitia yeye wakulima wamehamasika sana. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, hivi sasa ninavyozungumza zabibu zimejaa katika mashamba ya wakulima pale Hombolo, Matumbulu na Mpunguzi na hawana sehemu ya kupeleka. Je, Serikali ina mkakati gani sasa wa kuhakikisha kwamba zao hilo la zabibu linapata soko la uhakika?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, je, Serikali ipo tayari sasa kuwapeleka wataalamu wetu Maafisa Ugani waende kujifunza nje ya nchi namna ambavyo zabibu inalimwa ili kuongeza tija kwa mkulima?

SPIKA: Majibu ya maswali hayo Mheshimiwa Naibu Waziri Kilimo Mheshimiwa Bashe, hata mimi shambani kwangu zabibu zinaliwa na ndege tu hazina soko.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Anthony Mavunde Mbunge wa Dodoma Mjini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, cha kwanza hatua tunayochukua sasa hivi, kama Wizara tunaanza utaratibu wa kuweka *restriction* ya ku-*import* mchuzi kutoka nje kwa kampuni zinayotumia zabibu ndani ya nchi kabla hawajanunua zabibu yote inayozalishwa ndani ya nchi. Kwa hiyo tutatengeneza utaratibu wa *quarter system* kwamba aneye-*import* mchuzi lazima tuone *contract* zake na wakulima wa ndani; kwamba amenunua zabibu yote na imekuwa *exhausted* zabibu ya ndani.

Mheshimiwa Spika, kwahiyo tutatumia *model* kama tunayotumia, ya sukari, ili tuhakikishe kwamba zabibu yetu kwanza inapata soko kama inatumika kwenye *wine* ama inatumika kwenye vinywaji vikali ili kuhakikisha wakulima zabibu yao yote ina nunuliwa kabla ya kuruhusu kibali cha kuingiza mchuzi kutoka nje. Kwa hiyo huu ni utaratibu na tutaanza nao hivi sasa. Ndani ya siku mbili au tatu zijazo tutakutana na kampuni zote tatu kubwa ambazo ni *off taker* wa mazao ya zabibu katika nchi ili kutengeneza hii program na kuhakikisha kwamba jambo hili tunalisimamia.

Mheshimiwa Spika, la pili, tunahakikisha sasa kwenda kwenye hatua ya pili. Kwamba badala ya wakulima wa zabibu kuuza tunda waanze kuuza mchuzi. Kwenye hili tumeanza kuongea na wenzetu wa *TEMDO* Pamoja na wa *SIDO* ili tuanze kutengeneza *centres* ambazo wakulima watapeleka zabibu zao. Kama tulivyokwenda pamoja tukiwa na Mheshimiwa Waziri Mkuu tukaona ile *pilot* ya kile chama cha ushirika cha WAMAKU kilichopo barabara ya Iringa ambacho kinachakata mchuzi na kuuza mchuzi badala ya kuuza zabibu, kwa hiyo hili ni jambo la kwanza.

Mheshimiwa Spika, kuhusu wataalamu sasa hivi wizara tunatambua Maafisa Ugani sita ambao tutawapeleka katika nchi ya South Afrika ili waweze kujifunza; na tunashirikiana na sekta binafsi kwa ajili ya ku-*train* watu wetu hawa. Na mtaalamu mmoja tuliyenaye nchini, ambaye ni mbobezi ambaye anastaafu hivi karibuni tunafanya mchakato na wenzetu ndani ya Serikali angalau apate *extension* baada ya kustaafu wakati tuna-*train* hao wataalamu sita nje ya nchi ili wakirudi tuwe tuna wataalamu wa kutosha wa zabibu.

SPIKA: Nimekuona Mheshimiwa Mariam Ditopile, uliza swali la nyongeza tafadhali.

MHE. MARIAM D. MZUZURI: Mheshimiwa Spika, nashukuru. Kwanza niipongeze Serikali ya Awamu ya Sita chini ya Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan pamoja na Wizara ya Kilimo; kwa kweli wakulima wa alizeti wameona neema kubwa sana. Hivi tunavyoongea bei ya mbegu ya kilo moja ya alizeti ni 1600, haijawahi kutokea katika nchi yetu. Kutokana na bei hiyo kupanda na kuleta matumaini makubwa sasa muamko umekuwa mkubwa kwa watu kwenda kulima alizeti. Je, Serikali kuititia Wizara ya Kilimo imejipangaje kutuletea mbegu nyngi za kutosha na za kisasa ili tuweze kulima zao hili kwenye msimu unaokuja hasa kwa Mkoa wetu wa Dodoma?

SPIKA: Majibu ya swali hilo muhimu hatutaki mwakani mafuta ya kupikia yatoke nje tuna uwezo wa kuzalisha ndani, mbegu lakini.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Ditopile kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali sasa hivi tumeanza kuchukua mahitaji ya mikoa wanayotuletea wao wenyewe kutokana na uwezo wa mkoa husika katika suala la uzalishaji. Katika mkoa wa Dodoma tunashirikiana kwa karibu kabisa na Ofisi ya Mkuu wa Mkoa na RAS ambayo ina-*coordinate* kutuletea mahitaji ya kila Wilaya ili sisi kama wizara tuweze kuwapatia mbegu. Nataka niwahakikishie wakulima kuwa mwaka huu tutahakikisha wakulima wa alizeti wanapata mbegu.

Mheshimiwa Spika, pamoja na changamoto zilizoko duniani za upatikanaji wa *hybrid seed* lakini *at least* tutahakikisha kwamba wakulima wote wanapata angalau *standard seed* ambazo zitaweza kuwasaidia katika mwaka huu na sisi Serikali wakati huo tunajipanga vizuri kwa ajili ya mwaka mwingine ili tuwe na *hybrid* za kutosha. Tumeshafanya *aggregation* tumeshaingia mikataba na wasambazaji na, hivi karibu tutaanza kusambaza mbegu kutokana na mahitaji ya mkoa husika.

SPIKA: Tunataka kuhakikishia Mheshimiwa Naibu Waziri hata ikija mbegu ya kununua watu watanunua ilimradi bei *affordable*, si lazima iwe ya bure hapana, watu wa-*afford* kununua *after all/safari* hii bei ya alizeti ni nzuri sasa wanaweza kununua mradi bei iwe ni ile ambayo inanunulika. Mheshimiwa Yustina Arcadius Rahhi bado tuko Wizara ya Kilimo

Na. 5

Kutatua Changamoto ya Huduma za Ugani Manyara

MHE. YUSTINA A. RAHHI aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kutatua changamoto ya upatikanaji wa huduma za ugani Mkoani Manyara

kutokana na upungufu wa wataalamu wa kilimo na mifugo katika ngazi ya Kata na Vijiji?

SPIKA: Majibu ya swali hilo, bado tuko kilimo, Mheshimiwa Hussein Bashe tafadhalii

NAIBU WAZIRI WA KILIMO alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo naomba kujibu swali la Mheshimiwa Yustina Arcadius Rahhi Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, lengo la Serikali ni kuhakikisha kila kijiji na kata kuwa na afisa ugani mmoja. Hadi sasa mahitaji ya maafisa ugani kulingana na vijiji, mitaa na kata zilizopo ni 2,538; na maafisa ugani waliopo ni 6,704 sawa na asilimia 33 ya mahitaji ya uwiano wa afisa ugani mmoja kwa vijiji vitatu. Aidha, kwa taarifa za mwaka 2020 Mkao wa Manyara kuna jumla ya maafisa ugani 188 sawa na asilimia 49 ya mahitaji ya maafisa ugani 386. Kwa hali hiyo Mkao wa Manyara una maafisa ugani zaidi ya wastani wa nchi ulioko sasa.

Mheshimiwa Spika, pia Wizara katika kukabiliana na uhaba wa maafisa ugani tumeanzisha mfumo wa kieletroniki wa Mobile Kilimo uliouunganishwa kuanzia ngazi ya kijiji, kata, wilaya, mkoa na wizara. Mfumo huo unawezesha wakulima kutumia simu za mkononi kutuma ujumbe mfupi na kuomba ushauri wa kitaalamu na kujibiwa na afisa ugani aliyesajiliwa kwenye mfumo.

Mheshimiwa Spika, hadi kufika mwishoni mwa mwezi Agosti, 2021 maafisa ugani wote na kaya za kilimo zaidi ya milioni 4.5 wamejisajili kwenye mfumo kati ya kaya za kilimo milioni saba. Kutokana na mfumo huo wakulima wengi wamekuwa wakipata ushauri wa huduma za ugani kwa urahisi zaidi.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais-TAMISEMI inaendelea kuajiri maafisa ugani kadri vibali vyta ajira vinavyopatikana, na wagani hao

wapelekwe kwenye maeneo yenyé upungufu wa Maafisa Ugan ikiwemo Mkoa wa Manyara.

SPIKA: Mheshimiwa Rahhi

MHE. YUSTINA A. RAHHI: Mheshimiwa Spika, nakushukuru, nashukuru pia kwa majibu mazuri ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, nina maswali madogo ya nyongeza. Kwanza kwa kuwa hali ya maafisa ugani ni mbaya zaidi kwa baadhi ya halmashauri ikiwepo Halmashauri ya Mbulu Mjini na Vijijini ambayo imebakiwa na maafisa kilimo watano tu tangu Mkuu wa Idara hadi vijijini na Halmashauri ya Mji ina maafisa ugani saba tu.

Je, Serikali sasa ina mpango gani kufanya hata *reallocation* wakati tunasubiria ajira ya Serikali kupeleka maafisa ugani katika maeneo haya?

Mheshimiwa Spika, swali langu la pili mimi naomba *commitment* ya Serikali kwa mwaka huu wa fedha unaoanza kuweza kuwapeleka maafisa ugani katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbulu? asante.

SPIKA: Majibu ya maswali hayo Mheshimiwa Naibu Waziri Kilimo, tafadhali.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Yustina Arcadius Rahhi Mbunge wa Viti Maalum kwa ufupi sana kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika nimwombe tu kwamba baada ya Vikao vyá Bunge hapa tukutane, tutakaa na wataalamu wa wizara, na tutashauriana na wenzetu wa TAMISEMI kuangalia *option* mbili. *Option* kwanza kungalia kama kuna uwezekano wa kufanya *reallocation*; lakini kwa kuwa kuna *shortage* kubwa tunatumia bodi zetu za mazao kuwaajiri maafisa ugani kwa ajili ya mazao mbalimbali; na Mkoa wa Manyara una *advantage* kwamba ni moja kati ya mkoa ambao unazalisha zao la pamba. Kwa hiyo tutaitumua bodi yetu ya pamba

katika *allocation*yao ya kuajiri maafisa ugani ili tuone namna gani tunaweza kupeleka maafisa ugani ambao wanaajiriwa na bodi zetu za mazao katika Mkoa wa Manyara na maeneo yenye upungufu.

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara ya Maji na swali la Mheshimiwa Alexander Pastory Mnyeti, Mbunge wa Misungwi kule Gwambina.

Na. 6

Hitaji la Maji Kijiji cha Nyanhomango

MHE. ALEXANDER P. MNYETI aliuliza:-

Chanzo cha Maji cha Ihelele kilichopo Kijiji cha Nyanhomango kinasambaza maji katika Mikoa ya Shinyanga na Tabora:-

Je, ni lini Serikali itapeleka miundombinu ya maji kwenye Kijiji hicho pamoja na vijiji vingine vinavyozunguka chanzo hicho?

SPIKA: Majibu ya swali hilo kutoka kwa Naibu Waziri wa Maji, Mheshimiwa Mhandisi Maryprisca Winfred Mahundi, tafadhali.

NAIBU WAZIRI WA MAJI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwa niaba ya Waziri wa Maji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Alexander Pastory Mnyeti, Mbunge wa Misungwi, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Kijiji cha Nyanhomango kilichopo katika Kata ya Ilujamate, kinapata huduma ya maji katika Skimu yenye chanzo kilichopo katika Ziwa Victoria kwenye bomba la kutoka Mabale kwenda Mbarika. Skimu hiyo inazalisha lita 1,555,200 kwa siku ambapo maji yanayozalishwa yanatosheleza mahitaji ya eneo lote ikiwemo Kijiji cha Nyanhomango. Huduma ya maji inapatikana

kwenye vituo 9 vya kuchotea maji na tanki moja lenye ujazo wa lita 135,000.

Mheshimiwa Spika, Kijiji cha Isesa katika Kata ya Ilujamate kinapata huduma ya maji kupitia skimu yenye chanzo cha kisima kirefu inayozalisha lita 116,000 kwa siku ukilinganisha na mahitaji ya kijiji hicho ambayo ni lita 91,100 kwa siku. Skimu hiyo ina vituo 12 vya kuchotea maji na tanki moja lenye ujazo wa lita 135,000.

Mheshimiwa Spika, katika bajeti ya mwaka 2021/2022, Serikali kupitia *RUWASA* inatekeleza Mradi mkubwa wa Maji Ilujamate – Buhingo utakaonufaisha vijiji 16 vilivyopo karibu na chanzo cha Ihelele. Vijihi hivyo ni Gukwa, Mbalama, Buhunda, Mwagimagi, Kifune, Gulumungu, Lukanga, Nyambiti, Busongo, Ng'hamve, Nyamayinza, Songiwe, Seeke, Buhingo, Kabale na Mwasagela.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa mradi huo unatarajiwu kuanza mwezi Oktoba, 2021. Kazi zitakazofanyika ni ujenzi wa matenki matatu yenye jumla ya ujazo wa lita 850,000, ulazaji wa bomba kuu kilometra 34.4, mabomba ya usambazaji maji kilometra 35 na vituo vya kuchotea maji 25. Kukamilika kwa mradi huo kutaboresha huduma ya maji kutoka asilimia 73 za sasa hadi asilimia 88 mwaka 2023.

SPIKA: Waheshimiwa Mawaziri, najua tumeanza leo lakini kuanzia kesho majibu mafupi, tunarudi kwenye utaratibu wetu. Najua leo tumejisahau kidogo, kila Wizara inayokuja hapa ina majibu marefu.

Mheshimiwa Mbunge wa Misungwi.

MHE. ALEXANDER P. MNYETI: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa nafasi hii. Nianze kwa kusikitika sana kwamba majibu anayoandaliwa Mheshimiwa Naibu Waziri na wataalam mengi ni ya uongo. Anaposema kwamba kule Nyanhomango maji yapo milioni ngapi sijui, ni uongo mtupu.

Mheshimiwa Spika, nataka nikwambie mimi ile lhelele tunayoisema ndyo chanzo kikubwa cha maji kinachopeleka maji Tabora, Nzega, Kahama, Shinyanga na maeneo mengine. Sisi hatuna tatizo na maji yanakwenda wapi; sisi shida yetu ni tupate maji kwenye kijiji hicho na maeneo yanayozunguka. Ni chanzo kikubwa lakini leo ni zaidi ya miaka 15 wananchi bado wanahangaika na maji kwenye eneo hilo.

Mheshimiwa Spika, sasa kinachosikitisha ni hao wataalam wetu walioko huko. Mimi nimemaliza ziara juzi pale; hakuna hata tone la maji. Hizo *DP* anazoisema Mheshimiwa Naibu Waziri ni kwamba ma-DP yamewekwa zaidi ya miaka 10 yanakwenda Mbarika halafu hayatoi hata maji. Sasa majibu haya Wanamisungwi wajue tu kama hamtaki kupeleka maji, lakini majibu haya yametolewa miaka 15 iliyopita yanaendelea kutolewa hayohayo, hatuwezi kufurahishana kwa staili hiyo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, sasa hawa wataalam wanaoanda haya majibu kwenda kwa Naibu Waziri, ni majibu ya uongo na wanatakiwa kuchungwa.

SPIKA: Ahsante sana. (*Kicheko*)

Naona Mheshimiwa Waziri wa Maji amesimama. Kabla hujajibu Mheshimiwa Waziri wa Maji, niku-*caution* kidogo; kwa miaka kumi, Mheshimiwa Charles Kitwanga aliuliza swali hilihili kuhusu kijiji hikihiki cha lhelele na mrithi wake anauliza swali hilihili la kijiji hicho hicho. Nakupa nafasi Mheshimiwa Waziri, hili ni moja ya maswali sugu hapa. (*Makofii*)

WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Spika, kwanza nikushukuru sana na nimpongeze Mheshimiwa Mbunge lakini nataka nimhakikishie kwamba Serikali inafanya jitihada kubwa sana katika Jimbo lake la Misungwi. Hivi karibuni tulikuwa na Mheshimiwa Rais na tumezindua mradi wa bilioni 12 katika kuhakikisha wananchi wanapata huduma ya maji. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, maji hayana mbadala na sehemu kwenye chanzo toshelezi, maelekezo ambayo tumeyatoa sisi kama Wizara ya Maji ni kuhakikisha kwamba kabla hatujapeleka maji maeneo mengine, wananchi wa maeneo husika lazima wapate huduma ya maji.

Kwa hiyo, ninachotaka kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge, nimuombe saa saba tukutane na mimi niko tayari kuongozana naye kufanya ziara ili kwenda kujiona uhalisia na kuweza kutoa msaada katika eneo lile ili wananchi waweze kupata huduma ya maji. Ahsante sana. (*Makofi*)

SPIKA: Mimi nashukuru sana, bora mkaenda pamoja kwa sababu kwa kweli hili ni moja ya maswali sugu, lina miaka 15 swalii hili hili linalarudi wakati kwa wakati, kuhusu kijiji tu. Sasa kama tunaweza kufanya miradi mikubwa kijiji kitatushinda kweli? Nadhani tuvuke hapo. Ndijo maana mnaona Mbunge alikuwa amekasikirika sana na hata Kitwanga aliondoka amekasirika sana, angekuwepo leo hapa sijui ingekuwaje; pangechimbika.

Tunaendelea na Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi na swalii la Mheshimiwa Kavejuri Felix, Mbunge wa Buhingwe. Mheshimiwa Kavejuri, tafadhali.

Na. 7

Ujenzi wa *Standard Gauge Railways* Tabora – Kigoma

MHE. KAVEJURU A. FELIX aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itajenga Standard Gauge Railways kutoka Tabora kwenda Kigoma?

SPIKA: Majibu ya swalii hilo Mheshimiwa Naibu Waziri Ujenzi na Uchukuzi, Mheshimiwa Mwita Mwikwabe Waitara, tafadhali.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. MWITA M. WAITARA) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Kavejuru Aliadory Felix, Mbunge wa Buhigwe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi kupitia Shirika la Reli Tanzania (*TRC*) inaendelea na ujenzi wa Reli ya Kati kwa kiwango cha *Standard Gauge* kwa awamu ya kwanza kutoka Dar es Salaam hadi Mwanza yenyе urefu wa kilomita 1,219. Kutokana na gharama kubwa za ujenzi na ili kurahisisha ujenzi, awamu ya kwanza inajengwa katika vipande vitano ambavyo ni Dar es Salaam – Morogoro (kilometra 300), Morogoro – Makutupora (kilometra 422), Makutupora – Tabora (kilometra 368), Tabora – Isaka (kilometra 165) na Isaka – Mwanza (kilometra 341).

Mheshimiwa Spika, ujenzi katika vipande vitatu vya Dar es Salaam – Morogoro (kilometra 300), Morogoro – Makutupora (kilometra 422) na Mwanza – Isaka (kilometra 341) unaendelea na Serikali inakamilisha taratibu za manunuzi ya makandarasi kwa ajili ya ujenzi wa reli ya *Standard Gauge* kwa vipande vya Makutupora – Tabora (kilometra 368) na Tabora – Isaka (kilometra 165).

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa reli ya Tabora – Kigoma (kilometra 411) Serikali imemua jiri Mshauri Elekezi wa Kampuni ya COWI kwa ajili ya kufanya upembuzi na usanifu wa awali wa ujenzi wa reli hii kwa kiwango cha *Standard Gauge*. Kazi hii inaendelea na inatarajiwa kukamilika Septemba, 2021.

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo, Serikali inaendelea kutafuta fedha kutoka kwa wadau mbalimbali wa maendeleo kwa ajili ya kupata mkopo wenye masharti nafuu kwa lengo la kukamilisha ujenzi wa mtandao mzima wa reli kwa kiwango cha *Standard Gauge* ikiwemo reli ya Tabora – Kigoma (kilometra 411), Kaliua – Mpanda – Karema (kilometra 316.7).

Mheshimiwa Spika, ahsante.

SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Kavejuru Felix, swali la nyongeza.

MHE. KAVEJURU A. FELIX: Mheshimiwa Spika, nina swali moja la nyongeza, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, reli ya kutoka Tabora kwenda Kigoma na ujenzi mzima wa *SGR* kutoka Dar es Salaam hadi Kigoma ni wa muhimu kweli, kwa kuzingatia kwamba nchi ya Congo DRC inaitegemea reli hiyo kwa ajili ya kusafirisha mizigo yake, ambacho ni chanzo kikubwa sana cha uchumi wa nchi yetu. Naomba kujua ni upi mkakati wa Serikali wa kuharakisha ujenzi wa reli hiyo baada ya upembizi huu ambao unakamilika mwezi huu wa Septemba?

SPIKA: Majibu ya swali hilo Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Mheshimiwa Waitara, tafadhalii.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. MWITA M. WAITARA): Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Kavejuru Aliadory Felix, Mbunge wa Buhigwe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza ni kwamba kazi ya upembizi yakinifu inafanyika na inakamilika mwaka huu, Septemba, 2021. Pia nimesema kwenye majibu ya swali la msingi kwamba tunatafuta mkopo wa gharama nafuu usio na masharti magumu ili ujenzi uweze kuanza.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mbunge naomba atupe nafasi tulifanyie kazi jambo hili. Limepewa uzito mkubwa na Mheshimiwa Rais ameshaelekeza kwamba miradi yote ya kimkakati ikiwepo hii *SGR*, kama nilivyotaja kwenye majibu yangu ya msingi, ni lazima ijengwe kwa wakati.

Mheshimiwa Mbunge naomba awe na amani, eneo hili reli itajengwa na watu wa eneo hili watapata huduma ya usafiri. Ahsante sana.

SPIKA: Ahsante sana. Tunaendelea na Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, swali la Mheshimiwa Mwantatu Mbarak Khamis kutoka Baraza la Wawakilishi.

Na. 8

Kuwawezesha Watu Wenye Ulemavu Katika Michezo

MHE. MWANTATU MBARAK KHAMIS aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuwainua Watu Wenye Ulemavu kwa kuwapatia vifaa vyta michezo na walimu ili waweze kushiriki mashindano ya kitaifa na kimataifa.?

SPIKA: Majibu ya swali hilo Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Mheshimiwa Pauline Philip Gekul, tafadhalii.

NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mwantatu Mbarak Khamis, Mbunge kutoka Baraza la Wawakilishi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ili kusimamia sekta ya maendeleo ya michezo kwa weledi, Serikali imetengeneza Mpango Mkakati wa Maendeleo ya Michezo wa Taifa ambao utazinduliwa rasmi mwezi Septemba 2021. Mpango mkakati huo una malengo ya kuendeleza michezo kwa ujumla wake ikiwa ni pamoja na michezo ya watu wenye ulemavu. Mpango huo unaainisha maeneo yote muhimu yakiwemo upatikanaji wa vifaa, ujenzi na ukarabati wa miundombinu, uendelezaji na upatikanaji wa wataalam na walimu wa michezo.

Mheshimiwa Spika, pamoja na uendelezaji wa mpango huo, Serikali kuititia Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo imekuwa ikiwasaidia wana michezo

wenye ulemavu kushiriki katika michezo mbalimbali kwa kuwapatia mahitaji muhimu ikiwa ni pamoja na vifaa vya michezo na wataalam wa mchezo husika. Mathalani mwaka huu wa 2021, Serikali imelipia usafiri, vifaa na posho kwa wachezaji na viongozi wanne kushiriki Michezo ya Paralimpiki inayofanyika nchini Japan – Tokyo kuanzia tarehe 24/08 - 04/09/2021. Zaidi ya milioni 15 zimetumika.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2019, Serikali iligharamia timu yetu ya mchezo wa *wheel Chair* kushiriki mashindano ya Afrika Mashiriki Nairobi Kenya. Mwaka huo huo Serikali iligharamia Timu ya Taifa ya Mpira wa Miguu kwa watu wenye ulemavu kushiriki mashindano ya Bara la Afrika (*CANAF*) yaliofanyika nchini Angola. Timu hiyo ilifuzu kushiriki mashindano ya Dunia ya mchezo huo yatakatofanyika mwaka 2022 nchini Uturuki.

Mheshimiwa Spika, kupitia Mfuko wa Maendeleo ya Michezo uliopo chini ya Baraza la Michezo la Taifa, ni matarajio yetu kuwa tutaendelea kuwasaidia wachezaji wenye ulemavu kwa mahitaji mbalimbali ili waweze kushiriki kikamilifu katika michezo ya Kitaifa na kimataifa kwa kuwapatia maandalizi na kuwa na vifaa mbalimbali pamoja na watalaam pale wanapohitaji msaada huo.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa muuliza swali, Mheshimiwa Mwantatu.

MWANTATU MBARAK KHAMIS: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kabla ya kuuliza swali la nyongeza kwanza nitumie nafasi hii kuipongeza Serikali kwa jitihada za kuona umuhimu wa kusaidia kuimarisha shughuli za michezo kwa watu wenye ulemavu.

Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, naomba kuuliza swali la nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika bajeti ya mwaka 2021/2022, Bunge liliidhinisha shilingi bilioni 1.5 kwa ajili ya shughuli za michezo. Je, kwa bajeti hii, kiasi gani kimetengwa kwa ajili ya kuendeleza shughuli za michezo kwa watu wenye ulemavu? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, swali langu la pili, Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania aliiagiza Wizara kuimarisha michezo kwa wanawake na nimeona katika vyombo vya habari kwamba Wizara inajijanda kutayarisha tamasha ambalo litajumuisha wanamichezo wanawake wa Tanzania nzima. Niipongeze sana Wizara kwa kufanikisha hilo. Swali langu, kwa vile michezo hii inajumusihia wanawake wa Tanzania nzima, je, maandalizi yamezingatia vipi ushiriki wa wanawake wakiwemo wanawake wenye ulemavu kutoka Zanzibar? Ahsante. (*Makofi*)

SPIKA: Majibu ya maswali hayo mawili tafadhali Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANA NA MICHEZO: Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mwantatu Mbarak Khamis, Mbunge kutoka Baraza la Wawakilishi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, jambo la kwanza amehitaji kufahamu katika Mfuko wetu wa Maendeleo ya Michezo ambao Bunge hili Tukufu mmetupitishia zaidi ya *1.5 billion*, je, fedha hizi zitakwenda kuwa-*support* watu wenye ulemavu? Naomba nimjulishe Mheshimiwa Mbunge kwamba watu wenye ulemavu katika Wizara yetu ni watu wa kipaumbele. Kwa hiyo, nimtoe wasiwasi kabisa kwamba pale ambapo watakuwa wanahitaji *support* ya Wizara, hasa kwa michezo ya Kimataifa ndiyo sababu ya fedha hizi kupitishwa na sisi tutaendelea kuwapa kipaumbele.

Mheshimiwa Spika, pia siyo fedha hizi tu tuna fedha kwa ajili ya Mfuko huu kupitia michezo ya bahati nasibu,

maana yake mfuko huu utaendelea kutunishwa. Kabla ya hapo fedha zilikuwa chache, tulikuwa na takribani zaidi ya milioni 200 kwenye Mfuko kwa ajili ya kuwa-*support*, lakini kwa sasa kwa fedha hizi maana yake wao watakapofuzu kupitia kwenye vyama vyao sisi tutaendelea kuwapa kipaumbele watu wenye ulemavu.

Mheshimiwa Spika, swalii la pili, alihitaji kufahamu kwenye tamasha hili la michezo kwa wanawake ambayo Wizara yetu jana pia tumezindua Kamati ya kusimamia tamasha hili ambalo litasimamia michezo kwa wanawake, je, watu wenye ulemavu wamepewa nafasi kiasi gani.

Naomba nimjulishe Mheshimiwa Mbunge kwamba watu wenye ulemavu katika tamasha hili watashiriki kupitia michezo yao ambayo wanacheza. Kwa sasa kuna timu ya mpira wa kikapu na wanariadha watashiriki katika tamasha hili na pia tumeshirikisha wote.

Mheshimiwa Spika, naomba nitoe rai kwa Watanzania wote hili tamasha litakapoanza mwezi huu wa Septemba kuanzia tarehe 16 na kuendelea, tushiriki kwa pamoja ili tuweze kumuenzi Mheshimiwa Rais wetu Mama Samia Suluhu Hassan kwenye suala zima la kunyanya wanawake katika michezo. Nitoe rai kwa Wabunge wenzangu, tutaleta mwaliko kwako Spika, naomba tushiriki. Najua tunacheza *netball*, lakini kamba na michezo mingine wanawake tujitokeze na tamasha hili litakuwa endelevu.

SPIKA: Ahsante sana. Tunakwenda Mambo ya Ndani ya Nchi, swalii limechukua muda mrefu na swalii la Mheshimiwa Saada Monsour Hussein, Mbunge wa Viti Maalum.

Na. 9

Wananchi Kupatiwa Vitambulisho vya Taifa (NIDA)

MHE. SAADA MONSOUR HUSSEIN aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itawapatia Vitambulisho vya *NIDA* wananchi wote waliojiantikisha?

SPIKA: Majibu ya swali hilo, Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Hamza Khamis Khamis, tafadhalii.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Saada Monsour Hussein, Mbunge wa Viti Maalum kutoka Mkoa wa Kaskazini Unguja, kama ifuatayyo: -

Mheshimiwa Spika, Mpango wa Serikali ni kuhakikisha watu wote waliosajiliwa na kupata namba za utambulisho wanazalishiwa na kugawiwa vitambulisho vya Taifa.

Mheshimiwa Spika, hadi kufikia mwezi Agosti, 2021, Serikali kuitia Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (*NIDA*) imefanikiwa kuzalisha na kugawa kwa wananchi jumla ya vitambulisho 8,397,524. Aidha, Mamlaka inaendelea na mpango kazi wa uzalishaji ambapo wananchi wote wenye sifa watazalishiwa na kugawiwa vitambulisho vyao ifikapo tarehe 31 Desemba, 2021. Nakushukuru.

SPIKA: Mheshimiwa Saada.

MHE. SAADA MONSOUR HUSSEIN: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niweze kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Pia nimshukuru Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri.

Mheshimiwa Spika, swali langu la kwanza, je, ni njia zipo kama Serikali mnazitumia kuwajulisha wale ambao hadi leo hawajapatiwa vitambulisho vyao kwenye vituo vya *NIDA*?

Mheshimiwa Spika, je, Serikali inatambua kuwa kwenye ofisi za *NIDA* kuna uhaba wa watumishi? (*Makof!*)

SPIKA: Majibu ya maswali hayo Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani, tafadhalii.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mbunge Saada Mansour Hussein, lakini pia nataka kutumia fursa hii kumpongeza sana kwa kazi nzuri na kubwa ambayo anaifanya katika Mkoa wa Kaskazini ya kuhakikisha kwamba akina mama au wananchi, lakini zaidi akina mama na watoto wanaishi katika mazingira mazuri zaidi.

Mheshimiwa Spika, swalii la kwanza ni njia zipo ambazo tunazichukua kama Serikali kuhakikisha kwamba wale ambao hawajaenda kuchukua vitambulisho vyao taarifa zinawafikia.

Mheshimiwa Spika, kwanza nataka nichukue fursa hii, niwashukuru wananchi na viongozi kwa kuwa wametambua kwamba bado kuna baadhi ya wananchi hawajaenda kuchukua vitambulisho vyao mpaka muda huu, badala yake wanakaa wanalaumu Serikali. Kwa hiyo kikubwa ambacho nataka niseme ni kwamba, zipo njia nyingi ambazo huwa tunazitumia kuwafikishia ujumbe au taarifa kwamba vitambulisho viro na waje.

Mheshimiwa Spika, ya kwanza; huwa tunawatumia ujumbe mfupi, kwa wale ambao namba zao zipo hewani zinapatikana. Pia huwa tunawapigia simu kabisa kuwalishaa. Vile vile kupitia Ofisi za Wakuu wa Wilaya na kupitia Ofisi za Masheha na Watendaji huwa tunatoa taarifa hizo ili wananchi ambao wameshatengenezewa vitambulisho vyao, lakini hawajaenda kuvichukua, waende wakavichukue.

Mheshimiwa Spika, swalii la pili, nikiri kwamba, bado tuna changamoto ya rasilimawatu katika Ofisi zetu za *NIDA*, lakini nimwambie Mheshimiwa aendelee kustahimili, Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, kupitia *NIDA* tupo katika mchakato wa kutengeneza mazingira ya kuajiri vijana, lengo na madhumuni, shughuli za *NIDA* ziweze kwenda vizuri.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru.

SPIKA: Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, swali ni la Mheshimiwa Mariamu Madalu Nyoka, Mbunge wa Viti Maalum. Mheshimiwa Mariamu Nyoka, tafadhalii.

Na. 10

Kufanya Ukarabati Hospitali ya Rufaa - Mkoa wa Ruvuma

MHE. MARIAM M. NYOKA aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuifanyia ukarabati mkubwa Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Ruvuma kwa kuwa ni ya muda mrefu na majengo yake yamechakaa?

SPIKA: Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Mheshimiwa Dkt. Mollel, tafadhalii.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA,
WAZEE NA WATOTO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mariamu Madalu Nyoka, Mbunge Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea na ukarabati wa majengo chakavu katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Ruvuma kwa kubomoa majengo chakavu manne; jengo la Masjala ya zamani, choo cha nje cha wagonjwa, jengo la viungo bandia na jengo la zamani la huduma za kifua kikuu, kwa ajili ya kujenga jengo la kisasa la wagonjwa wa dharura ambalo limefikia asilimia 95. Mradi huu unagharimu jumla ya shilingi 630,340,507.00, ambapo hadi sasa fedha hiyo imetolewa yote. Ujenzi huu unatarajiwa kukamilika ifikapo mwezi Oktoba, 2021. Ahsante.

SPIKA: Mheshimiwa Mariamu Nyoka nimekuona.

MHE. MARIAM M. NYOKA: Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Serikali naomba niulize maswali madogo mawili ya nyongeza. Swali la kwanza; Je, lini Serikali itafanya ukarabati mkubwa kwenye majengo mengine yaliyo chakavu zaidi katika Hospitali hiyo? (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, swalî la pili; uchakavu wa majengo ya hospitali hiyo yanakwenda sambamba pamoja na uchakavu wa vifaa tiba, ikiwemo *ultra sound*, Mashine ya kufulia na vifaa vingine. Je, Serikali haioni umuhimu wa kununua vifaa hivyo katika hospitali hiyo? (*Makof!*)

SPIKA: Majibu ya maswali hayo, Mheshimiwa Naibu Waziri Afya, Mheshimiwa Dkt. Godwin Oloyce Mollel, tafadhalli.

NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza nianze kwa kumshukuru Mheshimiwa Mbunge kwa sababu nilikuwa naongea na Mganga Mfawidhi wa Hospitali hiyo ananiambia alimtembelea juzi kabla ya kuja Bungeni. Kama alivyotembea amejionea yeye mwenyewe kwanza jengo ambalo limejengwa hilo la magonjwa ya dharura, lakini alijionea ukarabati mzuri uliofanyika kwa mapato ya ndani kwenye magonjwa yanayoambukiza ambayo sasa wagonjwa wenyewe matatizo ya kupumua wamelazwa mle ndani na Serikali inaendelea na ukarabati wa majengo mengine kwa mtindo ambao sasa jengo ambalo linamalizika mwezi Oktoba umefanyika.

Mheshimiwa Spika, pia akumbuke kwamba pamoja na hilo kwa juhudî za Wabunge wa Mkoa wa Ruvuma wakiongozwa na Mheshimiwa Jenista Mhagama, walianzisha mchakato wa kupata hospitali mpya kabisa ya mkoa, ambapo kule Mwenge - Mshindo wameweza kupata heka

276 kwa ajili ya kujenga hospitali mpya ya mkoa. Waziri wa Afya alituma watu wa kwenda kuangalia eneo, lakini ikaonekana kuna watu sita walitakiwa kufidiwa na ikafanyika tathmini ikaonekana inatakiwa milioni 700 kwa ajili ya kufidia. Sasa Waziri wa Afya ameagiza hebu tuhakiki hiyo milioni 700 kwa watu sita kwa nyumba za udongo ni nini. Kwa hiyo, mimi na Mheshimiwa Mbunge tutakwenda kuangalia tujihakikishie hilo ili sasa tuanze michakato ya kupata Hospitali mpya kabisa ya Mkoa wa Ruvuma. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, swalilake la pili kuhusu vifaa tiba; Mheshimiwa Mbunge atakumbuka, Bunge liliopita alikuja akilalamika kuhusu *x-ray* iliyoharibika ambayo ilikuwa ina shida ya *battery*na ilikuwa imeagizwa nje na imeshafika sasa na *x-ray* inafanya kazi. Tunampongeza sana Mbunge kwa juhudzi zake hizo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, Rais wetu Mama Samia Suluhu Hassan ameshapeleka milioni 348 *MSD*, zipo *cash* pale ambazo ni fedha, tukimaliza hapa tukutane mimi na Mheshimiwa Mbunge ili tuwasiliane na Uongozi wa Hospitali na Mkoa ili tuweze kupanga kulingana na mahitaji anayoyasema...

SPIKA: Ahsante sana.

NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO: Mheshimiwa Spika, lakini Rais wetu amepeleka *direct* kwenye akaunti yao milioni 110, nayo hiyo haijapangiwa chochote, kwa hiyo tunaweza vilevile kupanga kuelekeza kwenye maeneo anayoyasema.

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, nashukuru ahsante.

NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO: Mheshimiwa Spika, pia kuna milioni 130 kwa ajili ya Kiwanda cha Majitiba, kwa hiyo kazi inaendelea vizuri.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana na Mungu akubariki.

SPIKA: Muda Waheshimiwa haupo upande wangu. Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Mheshimiwa Mohammed Maulid Ali, Mbunge wa Kiembe Samaki. Uliza swali lako Mheshimiwa Mohammed. (*Kicheko*)

Na. 11

**Mgogoro baina ya Wananchi na Kambi ya
JWTZ –Chukwani**

MHE. MOHAMMED MAULID ALI aliuliza:-

(a) Je, Serikali inatambua mgogoro wa ardhi baina ya wananchi na Kambi ya Jeshi la Wananchi iliyopo Chukwani Zanzibar?

(b) Je, Waziri yupo tayari kufuatana na Mbunge ili kukutana na wananchi na kufahamu hali halisi ya mgogoro huo uliodumu kwa muda mrefu?

SPIKA: Majibu ya Swali hilo, Mheshimiwa Hamza Khamisi Khamisi, kwa niaba ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI K.n.y.
WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Maulid Ali Mohammed, Mbunge wa Jimbo la Kiembe Samaki lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Kambi ya Chukwani imepimwa na inatambuliwa kama Kiwanja Namba 787 na ramani yake imepata usajili Namba S.40/07. Eneo hili limepewa Hati Miliki Namba Z.20.2007. Hata hivyo, kuna wananchi wachache wanafanya shughuli za kibinadamu ndani ya eneo la kambi. Wananchi hawa sio wavamizi, wanatakiwa kulipwa fidia kwani ni maeneo yao ya siku nyingi

kabla ya Jeshi kutwaa na kupima eneo hilo, pia ilikubalika waondoke baada ya kufanyiwa uthamini na kulipwa fidia.

Mheshimiwa Spika, Wizara inatambua mgogoro huo na hivi sasa ipo katika mpango wa miaka mitatu wa kuondoa migogoro yote iliyopo katika maeneo yake ikiwemo Kambi ya Jeshi ya Chukwani iliyopo Zanzibar. Mpango huo utajumuisha na kupatiwa Hati Miliki za maeneo yake yote.

(b) Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa alikuwa anauliza kwamba tupo tayari kwenda kuonana na wananchi. Nimwambie tu kwamba tupo tayari kwenda kuonana na wananchi ili tuweze kukaa nao, tujue sasa asili na chanzo cha mgogoro huo na tuwaeleze hatua ambayo tumefikia kama Serikali. Nakushukuru.

SPIKA: Mheshimiwa Mbunge wa Kiembe Samaki, nimekuona.

MHE. MOHAMMED MAULID ALI: Mheshimiwa Spika, ahsante. Nimeridhika na majibu.

SPIKA: Shukrani. Tunaendelea na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, swali la Mheshimiwa Bryceson Magessa Tumaini, Mbunge wa Busanda.

Mheshimiwa Tumaini hayupo. Tunaendelea na swali linalofuata.

MBUNGE FULANI: Mheshimiwa Spika...

SPIKA: Wizara ya Nishati na Madini litaulizwa na Mheshimiwa Zuena Athuman Bushiri, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Zuena.

Na. 13

Umembe wa REA III

MHE. ZUENA A. BUSHIRI aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kusambaza umeme katika Vijiji na Vitongoji kuititia *REA* /// hasa katika maeneo ambayo nguzo zimetelekezwa barabarani zaidi ya miaka miwili?

SPIKA: Majibu la swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati, tafadhali.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Nishati, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Zuena Athumani Bushiri, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali kuititia Wakala wa Nishati Vijijini - *REA* na Shirika la Umeme Nchini (*TANESCO*), inaendelea kutekeleza mpango wake wa kusambaza umeme vijijini awamu ya tatu, mzunguko wa pili katika vijiji vyote nchini. Utekelezaji wa mradi huu ulianza mwezi Machi, 2021 na unatarajiwa kukamilika ifikapo Disemba, 2022.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa Mradi huu unalenga kufikisha umeme katika vijiji 1,956 kati ya vijiji 12,268 ambavyo havijafikiwa na umeme. Kazi ya kupeleka umeme katika vitongoji ni endelevu inayoendelea kutekelezwa kuititia *TANESCO* na *REA* ikiwa ni kazi ya kuendelea kuunganisha huduma ya umeme kwa wananchi.

SPIKA: Mheshimiwa Zuena, swali la nyongeza.

MHE. ZUENA A. BUSHIRI: Mheshimiwa Spika, ahsante pamoja na majibu ya mazuri ya Serikali ninayo maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na changamoto ya miradi kutokukamilika kwa wakati. Nini kauli ya Serikali kwa wakandarasi ambao hawamalizi miradi yao kwa wakati na kuchelewesha huduma kwa wananchi. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, swali langu la pili kumekuwa na wimbi kubwa sana la wizi wa miundombinu ya umeme, mfano kule Moshi Manispaa, katika Kata za Soweto, Boma Ng'ombe, Barabara ya Bonite pamekuwa na wimbi la vijana ambao wanaiba miundombinu hii. Je, Serikali hii inachukua hatua gani kudhibiti uharibifu huu? Ahsante. (*Makofii*)

SPIKA: Majibu ya maswali hayo mawili, Mheshimiwa Naibu Waziri Nishati, Mheshimiwa Byabato Stephen Lujwahuka, tafadhalii.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Zuea maswali mawili ya nyongeza, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kauli ya Serikali kuhusiana na miradi ambayo haijakkamilika ni kwamba, kwanza ifikapo Disemba mwaka huu 2021 miradi yote ambayo siyo ya *REA III round II* itakuwa imekamilika kwa maana ya *REA II* na *REA III round I* itakuwa imekamilika.

Mheshimiwa Spika, tulikuwa na changamoto kidogo zilizopelekea miradi hii kuchelewa, sababu mojawapo ikiwa ni kwamba ni vile vifaa ambavyo vilikuwa vinaagizwa nje ya nchi vilichelewa kufika kwa sababu ya *lockdown* za wenzetu kule kushindwa kuleta vile vifaa kwa wakati. Shida nyingine ilikuwa ni maeneo mengine miundombinu kuharibiwa na mvua kali na hivyo watu wakashindwa kukamilisha kazi zao kwa wakati. Hata hivyo, tumejiwekea utaratibu na tunawaahidi Watanzania kwamba ifikapo Disemba mwaka huu hakutakuwa kuna mradi wowote wa *REA III round I* au *REA II* ambayo inaendelea, itakuwa yote imekwisha. Miradi ambayo itakayokuwa inaendelea ni ya *REA III round II* ambayo nayo Disemba mwakani itakamilika.

Mheshimiwa Spika, ili kuhakikisha mambo haya hayajitokezi tena, Serikali ilielekeza kwamba vifaa vyote vipatikane hapa nchini na kweli vinapatikana. Hiyo inatuongezea *speed* ya kufanya kazi hizi na kuzimaliza mapema.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo Serikali imelifanya ni kuhakikisha sasa inatoka kwenye kufanya kazi hizi kwa mtindo wa *goods* na kuziweka kwenye *works*, kwamba mtu atalipwa baada kukamilisha kipande fulani cha kazi ambacho anatakiwa kukifanya na hiyo inatusaidia kusimamia vizuri maeneo haya.

Mheshimiwa Spika, jambo la tatu ambalo Serikali imelifanya, tumehakikisha sasa tunakwenda kila kanda na kila mkoa kuweka msimamizi wa miradi yetu ya *REA*, akae kule masaa 24 akimsimamia mkandarasi anayefanya kazi kuhakikisha kwamba kazi inakwenda vizuri.

Mheshimiwa Spika, jambo la nne, tumehakikisha kwamba, wale wakandarasi wanaokwenda kwenye maeneo yetu tumewakabidhi kwa Waheshimiwa Wabunge ili na wenyewe wawe wasimamizi namba moja wa kuhakikisha kila siku wanawaona *site* na pale ambapo panatokea hitilafu ya kuwa mzembe mzembe, basi taarifa hizo zinatufikia mara moja. Tunaamini njia hizo zitatusaidia.

Mheshimiwa Spika kwenye jambo la pili; jambo la wizi siyo la mtu mmoja kulikemea, tunawaomba wenzetu tuendelee kushirikiana, sisi kama Wizara tunawapa *support* kubwa sana wakandarasi wanapotoa taarifa za kuibowi, tunasaidiana nao moja kwa moja kuhakikisha kwamba tunafuatilia, kuhakikisha tunawachukulia hatua wale walioiba miundombinu. Pia tunaweka mikakati mingine ya ziada ya kuwasaidia wale wakandarasi kuweka vifaa vyao katika *godownza TANESCO* ili angalau viwe katika usalama zaidi.

Mheshimiwa Spika, vile vile tumewaelekeza, wao ndiyo wenye wajibu wa kuhakikisha mali hizo haziibiwi ili wafikishe mizigo ile na kazi ifanyike kwa wakati. Tunaamini kufikia Disemba mwakani, jambo la kupeleka umeme *REA* // *round II* litakamilika kwa muda uliopangwa kwa mujibu maelekezo ya Serikali. Nashukuru.

SPIKA: Ahsante sana. Tunaendelea na Wizara ya Maliasili na Utalii, swali litaulizwa na Daniel Awack Tlemai Mbunge wa Karatu.

Na. 14

Mgogoro wa Mpaka katika Kata ya Mbulumbulu

MHE. DANIEL A. TLEMAI aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kutatua mgogoro wa mpaka kati ya Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro na Kata ya Mbulumbulu katika Kijiji cha Lositete?

SPIKA: Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Mary Masanja, tafadhali.

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Daniel Awack Tlemai, Mbunge wa Karatu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Mgogoro wa mpaka kati ya Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro na Kata ya Mbulumbulu katika Kijiji cha Lositete ulidumu kwa muda mrefu. Mgogoro huu ulitatuliwa kwa kushirikiana na mamlaka mbalimbali za Serikali zikiwemo:-

(i) Kamati za Ulinzi na Usalama za Wilaya ya Karatu, Monduli na Ngorongoro;

(ii) Wataalam kutoka Ofisi ya Katibu Tawala Mkoa wa Arusha; na

(iii) Wataalam kutoka Ofisi ya Katibu Tawala ya Wilaya za Karatu, Monduli na Ngorongoro; na Wahifadhi kutoka Mamlaka ya Hifadhi Ngorongoro.

Mheshimiwa Spika, Mamlaka hizi zote zilishiriki kutafsiri GN iliyoanzisha mipaka ya maeneo hayo kisheria.

Mheshimiwa Spika, Kijiji cha Lositete kiko katika Wilaya ya Karatu na sio Wilaya ya Ngorongoro ambapo wananchi wa kutoka kijiji hicho walivamia eneo la Hifadhi ya Ngorongoro na taratibu za kuwaondoa zilifanyika na kuwarudisha katika maeneo yao. Pamoja na kuwa Sheria ya Hifadhi ya Ngorongoro inaruhusu matumizi mseto, sheria hii iliwekwa kwa ajili ya wenyejji waliomo ndani ya hifadhi. Aidha, ndani ya hifadhi pia kuna maeneo ambayo yanasmamiwa Serikali ili kulinda uoto wa asili likiwemo eneo hili.

Mheshimiwa Spika, niendelee kutoa msisitizo kwa jamii zote zinazozunguka mipaka ya hifadhi kuheshimu maeneo yote yaliyohifadhiwa kwa faida ya jamii na maslahi ya Taifa kwa ujumla. Ahsante.

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Daniel Awack.

MHE. DANIEL A. TLEMAI: Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwa kuwa Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro ilianzishwa mwaka 1959 na mgogoro uliopo umekuja mwaka 2003 ambao umeweza kuchukua maeneo ya wananchi wa eneo hili la Kata ya Mbulumbulu, Kijiji cha Lositete. Sasa ni nini majibu ya Serikali kwa sababu mwaka 1959 kuanzishwa kwa Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro, hakukuwa na mgogoro, lakini mgogoro umekuja baada ya marekebisho ya mwaka 2003.

Mheshimiwa Spika, swali la pilii; je, ni lini Waziri yuko tayari kuongozana nami ili ajionee katika maeneo ya Kata ya Mbulumbulu, eneo la Lositete ili kuona kwamba wananchi jinsi wanavyopata shida katika eneo hili la Lositete? (*Makof*)

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri Majibu, Mheshimiwa Mbunge anataka mfuatane kwa ruhusa ya Spika.

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza

ya Mheshimiwa Daniel Awack, Mbunge wa Karatu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza naomba nimkumbushe Mheshimiwa Mbunge kwamba wakati hifadhi hizi zinaanzishwa mwaka 1959, wilaya zilikuwa ziko ndani ya wilaya za zamani. Kwa mfano; Karatu ilikua ndani ya Mbulu na sasa hivi Karatu iligawanywa, lakini pia na Ngorongoro ni Wilaya, kuna Monduli na kadhalika. Kama ambavyo nimejibu kwenye jibu langu la msingi, ni kwamba haya maeneo yalienda kutafsiriwa na Kamati za Ulinzi na Usalama za Mkoa pamoja na Wilaya na walishirikishwa wananchi kutambua ile mipaka.

Mheshimiwa Spika, huu mpaka ambao unagombaniwa ni mpaka ambao ni wa muhimu sana kluhifadhi; kwanza unatunza maji, unatunza mazingira, lakini pia, hawa wananchi walioko kwenye maeneo yale wanang'ang'ania kuingia mle kuchunga mifugo yao. Hatari itakayojitokeza ni kwamba maeneo mengi tunaenda kuyamaliza na tutasababisha kuwepo na tatizo la kukosa maji na wananchi katika maeneo yale wataweza kuathirika.

Mheshimiwa Spika, niwaombe wananchi watambue kwamba Serikali ina nia njema ya kutunza vyanzo vya maji kwa ajili ya jamii zinazozunguka maeneo hayo. Pia eneo lile tumelihifadhi kwa ajili ya Hifadhi ya Ngorongoro ambapo kuna eneo ambalo ni msitu ambao unahifadhiwa kwa ajili ya kutunza vyanzo vya maji kwa ajili ya wenyeji waliomo ndani yake. Niwaombe sana wananchi watambue kwamba Serikali ina nia njema na inawapenda ndiyo maana inahifadhi maeneo haya kwa ajili ya maisha yao ya kila siku.

Mheshimiwa Spika, ombi lake la pili la kuongozana na mimi, nimtoe wasiwasi tutaongozana wote kama ambavyo nimefanya kwenye ziara zangu nyingi baada ya Bunge la mwezi wa Sita kuisha, kwa hiyo tutakwenda pamoja. Ahsante.

SPIKA: Ahsante sana. Sasa tumalizie swalii lile la Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi. Nakupa tena nafasi Mheshimiwa Bryceson Magessa Tumaini, Mbunge wa Busanda.

Na. 12

Kupanga matumizi bora ya ardhi kwa Vijiji vyote nchini

MHE. TUMAINI B. MAGESSA aliuliza:-

Je, Serikali imejipangaje katika kupanga matumizi bora ya ardhi kwa Vijiji vyote nchi nzima ili kuondokana na migogoro ya matumizi ya ardhi?

SPIKA: Majibu ya swalii hilo, Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Mheshimiwa Dkt. Angeline Sylvester Mabula, tafadhalii.

NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Bryceson Magessa Tumaini, Mbunge wa Busanda, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Upangaji wa Matumizi ya Ardhi Na. 6 ya Mwaka, 2007 Sura ya 116 Kifungu cha 18, kimebainisha Mamlaka za Upangaji kuwa ni Halmashauri za Vijiji, Wilaya na Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi, ngazi ya Taifa na Mkoa. Jukumu la uandaaji wa Mipango ya Matumizi ya Ardhi ya Vijiji ni la Halmashauri za Vijiji na Wilaya. Wizara ya Ardhi kuititia Tume ya Mipango ina jukumu la kuwajengea uwezo, kusimamia na kuratibu Mamlaka za Upangaji na sekta mbalimbali katika utekelezaji wa mipango hiyo.

Mheshimiwa Spika, ili kuondokana na migogoro ya matumizi ya ardhi, jitihada mbalimbali zimeendelea

kuchukuliwa na Serikali ili kuhakikisha vijiji vyote nchini vinaandaliwa mipango ya matumizi ya ardhi. Jitihada hizo ni pamoja na zifuatazo: -

Kwanza, ni kutenga bajeti kuwezesha uandaaji wa mipango ya matumizi ya ardhi nchini, kupertia Mamlaka za Upangaji na hivyo kuondokana na migogoro ya matumizi ya ardhi.

Pili, kushirikisha wadau mbalimbali wa kimkakati wa matumizi ya ardhi, kuwezesha uandaaji wa mipango ya matumizi ya ardhi katika vijiji mbalimbali nchini.

Tatu, kuendelea kuhamasisha Halmashauri za Wilaya na Mikoa kutenga bajeti ya uandaaji wa mipango wa matumizi ya ardhi katika vijiji kwenye maeneo yao.

Nne, kushirikiana na vyuo vinavyofundisha masuala ya ardhi ikiwemo Chuo cha Ardhi, katika uandaaji wa mipango ya matumizi ya ardhi katika Halmashauri mbalimbali nchini.

Tano, kubuni miradi ya kimkakati itakayowezesha uandaaji, utekelezaji na usimamizi wa mipango ya matumizi nchini.

SPIKA: Mheshimiwa Mbunge wa Busanda.

MHE. TUMAINI B. MAGESSA: Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ardhi, ninayo maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza, kwa vile Wizara ya Ardhi kupertia Tume ya Mipango ya Ardhi inasimamia na kuratibu shughuli za matumizi bora ya ardhi; na kutokana na kwamba Tume hii imeshafanya matumizi bora ya ardhi kwenye hatua tofauti tofauti, lakini maeneo mengi nchini hayajafikishwa kwenye hatua ya mwisho na hivyo kuwachanganya wananchi kwamba, matumizi bora ya ardhi yaanze kutumika au yasitumike: Je, ni nini kauli ya Serikali juu ya kukamilisha matumizi bora ya ardhi kwenye maeneo ambayo wamekwishaanza kuyapanga sasa?

Swali la pili; inaonekana wazi kwamba Wizara inahamasisha Halmashauri zitenge fedha: kwa kuwa Tume hii ambayo sasa inaonekana wanaendelea na huku Wizara inahamasisha tu; na kuhamasisha siyo kumlazimisha mtu, inakuwa siyo wajibu, yaani Halmashauri haiwajibiki moja kwa moja: Je, Serikali haioni kwamba sasa itoe nyaraka ambayo inaweza kuifanya kila Halmashauri itenge fedha hizi kila mwaka kwa ajili ya kutenga matumizi bora ya ardhi katika maeneo waliyonayo?

SPIKA: Majibu ya maswali hayo mawili tafadhali, Naibu Waziri, Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Mheshimiwa, Dkt. Angeline Sylvester Mabula.

NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI: Mheshimiwa Spika, swali lake la kwanza Mheshimiwa Tumaini anasema: Je, Wizara haloni umuhimu wa kukamilisha mpango wa matumizi katika yale maeneo ambayo yamekwishaanza?

Mheshimiwa Spika, ni kweli swalilake ni la msingi. Changamoto tunayoipata ni kwamba katika suala zima la uanzishwaji maeneo mapya, unaweza ukawa na kijiji ambacho tayari kilishafanyiwa mpango wa matumizi na wakaanza kuutumia, lakini baadaye tunapogawa maeneo unakuta tena kile kijiji kinakatwa. Kwa hiyo, ule utekelezaji wa ile mipango ya awali inashindikana kufanyika, inabidi kuanza upya.

Mheshimiwa Spika, nitoe rai tu kwa Halmashauri zote nchini ambazo ndiyo mamlaka za upangaji, pale ambapo vijiji tayari vinakuwa vimeshawekewa mpango wa matumizi, tunaomba sana sana sana visifanyiwe mgawanyiko wowote. Kwa sababu, kitendo cha kugawanya kijiji kile kinaharibu mpango mzima, inabidi kuanza upya. Kwa hiyo, tumejikuta kuna vijiji tayari vilishafanyiwa mpango, lakini matumizi yake sasa yanashindikana kwa sababu kumezaliwa kijiji kingine ndani ya kijiji kingine. Kwa hiyo, naomba hilo liangaliwe katika Mamlaka zetu za Upangaji, nasi Wizara tutakuwa makini katika kufanya ufuatiliaji wa karibu.

Mheshimiwa Spika, swali lake la pili anauliza kuhusu kuzitaka Halmashauri zitenge bajeti; pengine wanajivutavuta katika suala hilo, lakini nataka nimtie tu shime kwamba Wizara hajanyamaza katika hilo. Katika mwaka huu wa fedha tumetenga shilingi 1,500,000,000/=, kwa ajili ya kusaidia katika shughuli hiyo ya upangaji wa matumizi, lakini hii haiondolei Mamlaka husika za Upangaji kutotimiza wajibu wake. Kwa hiyo, bado tunasisitiza kila Halmashauri ya Wilaya ihakikishe katika vitengo vyake, inapopanga bajeti za maendeleo, waikumbuke sekta ya ardhi kuitengea bajeti ya kutosha. Kwa sababu ardhi usipoipangia matumizi ndiko huko ambako migogoro inaanzia.

Mheshimiwa Spika, sisi kama Wizara tunaingia katikati kuweza kusukuma hili jukumu liende, kwa sababu tunasimamia miongozo na nyaraka mbalimbali ambazo ziniasukuma uendelezaji wa sekta ya ardhi. Kwa hiyo, ninachotaka au tunachoelekeza, Halmashauri zenye mamlaka, hili ni jukumu lao la msingi kuhakikisha upangaji, upimaji na umilikishaji unafanyika, kuhakikisha vijiji vyote vinakuwa na mpango wa matumizi ya ardhi, kwa kutenga bajeti stahiki na Wizara tutakuwa tayari kuendelea kuwasaidia. Kama ambavyo sasa hivi tunatoa fedha kwa ajili ya kupanga, kupima na kumilikisha katika maeneo yote.

Mheshimiwa Spika, naomba kwa ridhaa yako unipe nafasi tu kidogo niwaambie Waheshimiwa Wabunge kwamba Wizara imeweka mikakati, mbali na mpango wa matumizi ya ardhi katika maeneo ya vijiji, sasa tunakwenda kufanya zoezi la urasimishaji kwa nchi nzima. Zoezi hili litafanyika kwa nchi nzima bila kuacha mtaa wowote, tukisaidiana na wenzetu wa benki ambao watakwenda kutoa mikopo kwa mtu mmoja mmoja kuanzia kwenye kupima mpaka kumilikishwa. Mwananchi atakabidhiwa hati yake baada ya kuwa amemaliza kulipa mkopo. Mikopo siyo mikubwa kwa viwanja nya urasimishaji.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba sana tutakapokuwa tunaendelea kuhamasisha kwenye Halmashauri zetu, kwenye Wilaya zetu, tulipe kipaumbele ili

tuwawezeshe wananchi wetu. Mheshimiwa Rais amesharidhia zoezi hilo lifanyike na tayari makubaliano na *NMB Benki*, Wizara imeshainglia nao. Tumeshaanza kama *pilot area* eneo la Mbarali. Kwa hiyo, tutafuata wapi, ni jitihada za Halmashauri wenyewe kuweza kuwawezesha. Ahsante.

SPIKA: Ahsante sana. Maswali ya leo yamekamilika. Naomba tu kuanzia kesho kuendelea, wauliza maswali yawe mafupi, Waheshimiwa Mawaziri nao waje na majibu mafupi na maswali ya nyongeza yawe mafupi.

Sasa, naomba nitoe maelezo mafupi kuhusu uendeshaji wa Mkutano huu wa Nne wa Bunge. Waheshimiwa Wabunge, kama jinsi nilivyowasilisha jana kwenye Mkutano wetu wa *Briefing*, kwa kuzingatia azma tulyonayo ya kujikinga na Maambukizi ya UVIKO 19, utaratibu wa kuendesha Mkutano huu wa Nne wa Bunge utakuwa kama ifuatavyo: -

Kwanza, tutafupisha masaa ya kufanya kazi kwa lengo la kupunguza muda wa kukusanyika pamoja katika eneo moja. Kwa hiyo, vikao vyta Bunge kuanzia kesho vitaanza saa 8:00 mchana na kuendelea hadi saa 1:00 usiku Bunge litakapoahirishwa hadi siku inayofuata saa 8:00 ya mchana tena. Hii itatufanya tutumie masaa matano badala ya masaa saba na nusu kwa siku ambayo ndiyo huwa utaratibu wa kawaida.

Aidha, kipindi cha maswali kitatumia muda wa dakika 60 badala ya dakika 90. Ili kuwezesha hili, mara baada ya maelezo yangu nitamwita Waziri wa Nchi, ili atengue Kanuni zinazohusika ili ziendane na maelezo yangu haya. Kabla sijamwita Mheshimiwa Waziri, naomba niseme kwamba, kwa lengo la kupunguza msongamano, tutatumia kumbi mbili kuendesha shughuli za Bunge ambapo Ukumbi wa Msekwa utawezeshwa na kuwafanya Wabunge watakaokaa katika ukumbi huo kushiriki shughuli za Bunge sawa sawa na watakaokuwa katika ukumbi huu mkubwa.

Kwa maana hiyo, Mbunge atawenza kuuliza swali akiwa Ukumbi wa Msekwa, atawenza kuchangia hoja, atawenza kuomba mwongozo, atawenza kuomba swali la nyongeza na mambo mengine kwa kutumia mfumo uliouunganishwa moja kwa moja na ukumbi mkubwa wa Bunge.

Utaratibu huu utaanza kutumika kesho na orodha husika itakuwa inatolewa na Katibu wa Bunge kwa kila Kikao. Kwa hiyo, kabla hujafika kujua ni ukumbi upi unaenda, ni vizuri ukajua kwa kuangalia kishikwambi chako kwamba uko katika ukumbi upi?

Aidha, Kanuni zote za Bunge zinazotumika katika ukumbi mkubwa zitatumika pia katika Ukumbi wa Msekwa ikiwemo uvaaji wa mavazi rasmi. Tatu, tunasisitiza uvaaji wa barakoa wakati wote tukiwa katika maeneo ya Bunge na hususani ndani ya kumbi za mikutano. Jukumu hili ni letu sote isipokuwa kwa wale wachache wenye shida ya kiafya zinazokinzana na uvaaji wa barakoa ambapo hata hivyo itabidi tupate taarifa zao na wawe na idhini ya Spika ya kutovaa barakoa.

Wageni Bungeni; katika Mkutano huu hatutaruhusu wageni mbalimbali wanaokuja kwa ajili ya kutembelea Bunge au kwa ziara za mafunzo. Wageni pekee watakaoruhusiwa kuingia katika maeneo ya Bunge ni wale wenye shida za kiofisi, Maafisa wa Serikali wanaofuatilia shughuli za Bunge na waandishi wa habari.

Baada ya maelezo haya mafupi sasa, Katibu.

NDG. NENELWA MWIHAMBI, *ndc* – KATIBU WA BUNGE:

HOJA YA KUTENGUA KANUNI ZA BUNGE

SPIKA: Naomba nimwite sasa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Mheshimiwa Jenista Mhagama ili aweze kuwasilisha hoja ya kutengua Kanuni. Mheshimiwa Waziri, karibu.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU: Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Natoa maelezo haya ya kutengua kanuni chini ya Kanuni ya 174(1) na Kanuni ya 34(1), (2) na (3) na Kanuni ya 50(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Mwaka, 2020.

KWA KUWA, Mkutano wa Nne wa Bunge umeanza leo tarehe 31 Agosti, 2021 na umepangwa kumalizika tarehe 10 Septemba, 2021;

NA KWA KUWA, nchi yetu ipo katika mapambano ya kudhibiti maambukizi ya ugonjwa wa *UVIKO* 19 na Serikali imetangaza hatua mbalimbali za kuchukua ili kupunguza kasi ya maambukizi ya ugonjwa huu hatari; sisi kama Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, tutaendelea kutekeleza hatua zillizotangazwa na Serikali katika kudhibiti maambukizi ya ugonjwa huu;

NA KWA KUWA, katika kutekeleza hatua za kudhibiti maambukizi ya *UVIKO* 19, Bunge limeamua kupunguza muda wa vikao kwa kuanza Vikao vya Bunge saa 8:00 mchana hadi saa 1:00 usiku na pia kupunguza muda wa kipindi cha Maswali kutoka dakika 90 hadi dakika 60;

NA KWA KUWA, ili Bunge liweze kutimiza azima hiyo, Kamati ya Uongozi katika kikao chake cha tarehe 30 Agosti, 2021 ilikubali kwamba Kanuni ya 34 (1) na (2) inayohusu muda wa Vikao vya Bunge na Kanuni ya 50(1) inayohusu muda wa kipindi cha maswali vitenguliwe ili kuwezesha Bunge kukaa kwa muda mfupi wakati huo huo kutekeleza shughuli zote zilizopangwa kufanyika katika Mkutano;

HIVYO BASI, ili kuwa na utekelezaji bora wa shughuli za Bunge katika Mkutano huu wa Nane, Bunge linaazimia kwamba Kanuni ya 34(1) na (2) ambayo kwa ujumla wake inaelekeza Bunge kuanza saa 3:00 asubuhi hadi saa 7:00 mchana na kurejea saa 11:00 jioni na kuendelea hadi saa 1:45 usiku, itenguliwe na badala yake Bunge lianzesha kazi zake saa 8:00 mchana hadi saa 1:00 usiku. Aidha, Kanuni ya 50(1)

ambayo inaelekeza kwamba kipindi cha Maswali kwa mikutano isiyokuwa ya bajeti ni dakika 90, itenguliwe na sasa kipindi cha maswali kiwe dakika 60.

Mheshimiwa Spika, kwa heshima kabisa naomba kutoa hoja.

WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:
Mheshimiwa Spika, naafiki

(Hoja llitolewa lamuliwe)

SPIKA: Hoja imeungwa mkono. Tunakushukuru sana Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge, Kazi, Ajira, Vijana na Watu wenye Ulemavu kwa kuwasilisha hoja hiyo.

Ili kuiamulia hoja hiyo, naomba sasa niwahoji.

(Hoja iliamuliwa na Kufikiwa)

SPIKA: Wabunge wote wameafiki hoja hii. Nawashukuruni sana. (*Makofi*)

Baada ya mabadiliko hayo, sasa tunaendelea, Katibu.

NDG. NENELWA MWIHAMBI, ndc – KATIBU WA BUNGE:
Miswada ya Sheria ya Serikali.

MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI

NDG. RAMADHAN ISSA ABDALLAH – KATIBU MEZANI:

Muswada wa Sheria kwa ajili ya kufanya Marekebisho katika Sheria ya Jeshi la Zimamoto na Uokoaji kwa lengo la kuondoa upungufu ambao umebainika katika Sheria hiyo wakati wa utekelezaji wake, pamoja na kufanya marekebisho katika Sheria nyingine ili ziendane na marekebisho yanayopendekezwa katika Sheria hii. (*A Bill for An Act to*

Amend the Fire and Rescue Act for the purpose of addressing the shortcomings observed during the implementation of Law and to effect Amendments to other Laws to be in line with the proposed changes).

(Kusomwa Mara ya Kwanza)

NDG. JOSHUA CHAMWELA – KATIBU MEZANI:

Muswada wa Sheria kwa ajili ya kufanya Marekebisho katika Sheria Mbalimbali zipatazo Tisa kwa lengo la kuondoa upungufu ambao umejitokeza katika Sheria hizo wakati wa utekelezaji wa baadhi ya masharti katika Sheria hizo (*A Bill for An Act to Amend Certain Written Laws in order to keep the Laws updated with some challenges observed in its implementation*).

(Kusomwa Mara ya Kwanza)

SPIKA: Ahsante. Kwa hiyo, naelekeza sasa Sheria ile ya Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Jeshi la Zimamoto na Uokoaji ya Mwaka 2021, itashughulikiwa na Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama, ambapo Mwenyekiti wake ni Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu na Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria mbalimbali (Na. 5) wa Mwaka 2021, utashughulikiwa na Kamati ya Katiba na Sheria inayoongozwa na Mheshimiwa Najma Murtaza Giga.

Kwa maana hiyo, muanze kufanya taratibu za kuanza kupitia sheria hizi mapema iwezekanavyo. Kama tulivyoshauriana jana, Wabunge wengine wote mnaruhusiwa kufuatilia kwa karibu, mnaruhusiwa kushiriki baadhi ya hivi vikao ili mradi kwenye maamuzi Kamati yenyewe ndiyo itakuwa na maamuzi. Kwa sababu kipindi cha asubuhi hatukutani, basi Kamati hizi zitatumia muda wa asubuhi kuweza kupitia Miswada hii. Wabunge ambao mna muda mnaweza mkafika huko na kuona ni nini kinachoendelea katika uchakataji wa sheria hizi na kipindi cha kuwasikiliza wadau na kadhalika.

Katibu.

NDG. JOSHUA CHAMWELA – KATIBU MEZANI:

HOJA ZA KAMATI

SPIKA: Hoja za Kamati, namwita sasa Mwenyekiti wa Kamati ya Maadili na Madaraka ya Bunge. Mheshimiwa Mwakasaka, karibu sana. Kwa kadri mlivyojipanga ili kuweza kuwasilisha kwa utulivu, tumewatengea saa moja. Mnaweza mkatumia wastani wa nusu saa kwa hoja moja na nusu saa kwa hoja ile ile lakini upande wa pili. Hoja ni moja tu, ila ina mambo mawili tofauti. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, karibu.

MHE. EMMANUEL A. MWAKASAKA – MWENYEKITI WA KAMATI YA BUNGESA – MAADILI NA MADARAKA YA BUNGESA: Mheshimiwa Spika, ahsante, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Maadili na Madaraka ya Bunge kuhusu tuhuma zinazomkabili Mheshimiwa Josephat Mathias Gwajima, Mbunge za kuvunja haki za Bunge, kudharau mamlaka ya Bunge na kugonganisha Mihimili.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 4(2) na (3) ya Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020, naomba kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu, Taarifa ya Kamati kuhusu tuhuma zinazomkabili Mheshimiwa Josephat Mathias Gwajima za kuvunja haki za Bunge, kudharau mamlaka ya Bunge na kugonganisha mihimili.

Mheshimiwa Spika, napenda kukushukuru wewe binafsi kwa busara na hekima zako katika kuliongoza Bunge letu kwa ufanisi mkubwa. Aidha, tunakushukuru kwa namna unavyosimamia, kuulinda na kuutetea Mhimili huu muhimu na juhudhi zako za kuhakikisha Bunge linathaminiwa na kuheshimiwa na kila mtu hivyo kutekeleza majukumu yake ya kikatiba na kisheria bila kudhalilishwa, kuvunjiwa heshima na hadhi linayostahili.

Mheshimiwa Spika, aidha, napenda kumshukuru Naibu Spika na Wenyeviti wote wa Bunge letu kwa namna wanavyokusaidia katika kutekeleza majukumu yako.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilikutana tarehe 23 Agosti, 2021 na 27 Agosti, 2021 kwa ajili ya kushughulikia suala hilo kwa mujibu wa Kanuni ya 4(1)(a) na (b) ya Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni 2020. Kwa urahisi wa rejea ninanukuu kifungu hicho;

"4(1) Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge itatekeleza majukumu yafatayo:-

(a) Kuchunguza na kutoa mapendekezo kuhusu masuala yote ya Haki, Kinga na Madaraka ya Bunge yatakayopelekwa na Spika;

(b) Kushughulikia mambo yanayohusu maadili ya Wabunge yatakayopelekwa na Spika."

Mheshimiwa Spika, Chimbuko la Shauri, shauri hili linatokana na kauli mbalimbali zilizotolewa na Mheshimiwa Josephat Gwajima kwa nyakati tofauti ambazo ni tarehe 25 Julai, 2021, 1 Agosti, 8 Agosti na 15 Agosti, 2021 akiwa maeneo ya Ubungo Jijini Dar es Salaam. Kauli hizo zilinukuliwa katika vyombo mbalimbali vya habari na mitandao ya kijamii yaani Twitter, YouTube, WhatsApp na Facebook.

Mheshimiwa Spika, wakati naendelea naomba taarifa yangu yote iingie kwenye kumbukumbu za Bunge yaani Hansard.

Mheshimiwa Spika, zifuatazo ni mionganoni mwa kauli zilizotolewa na shahidi ambaye katika kesi hii ni Mheshimiwa Josephat Mathias Gwajima; na nukuu kauli zake:

(a) "Juzi juzi kukawa na kauvumi, uvumi ka-twitter sijui kalikuwa kanani kale kanasema eti Gwajima hataruhusiwa kuingia Bungeni mpaka achanjwe kwanza, kalikuwa kanatembea.

(b) *Baadaye Mheshimiwa, Ofisi ya Spika wakakanusha wakasema hiyo siyo twitter yetu, ni uongo. Nikawa nasema mimi hata kama ingekuwa kweli, mimi kuchanjwa ng'oo! Hachanjwi mtu hapa! Hachanjwi mtu hapa! Hata kama, hata kama ingekuwa kweli kwamba usiingie hachanjwi mtu hapa. Hata kwa dakika moja, yaani niko macho hivi. Hata kwenye ndoto hunichanji.*

(c) *Baadaye nimeona Ofisi ya Spika wakakanusha wakasema siyo kweli, lakini mimi nilikuwa nimejijanda tu sina wasiwasi. Bunge linaanza kesho. Kamati zinaanza kesho, mimi sina wasiwasi.*

(d) *Hachanjwi mtu hapa! Ikishindikana narudi hapa nyumbani. Mnanielewa eeh? Ubunge ni mzuri, Ubunge ni kusaidia Wananchi, Ubunge una heshima, Ubunge ni jambo zuri lila kuchanja, hakuna! Mimi nikisema imeshakuwa..." mwisho wa kunukuu.*

Mheshimiwa Spika, kauli nyingine zilizotolewa na Mheshimiwa Josephat Gwajima naomba ninukuu:

(a) *"Unayeona anabisha amepewa hela, nataka mwanasayansi ambaye hajachukua hela aje hapa tujadiliane, wale ambao mmeshachukua hela ya kidampa hamna haja ya kuniambia chochote, mwanasayansi ambaye hajachukua hela ambaye hajala hela kwa ajili ya kuchanjwa, aliyechukua hela utaniambia nini?*

(b) *Mmekula hela za watu unataka uwatimizie watu sawasawa na hela yao na mimi siwezi kukubali kutoa watu kupata kafala Watanzania eti tuishi mahali hakuna Taifa, watu hawazai, watu vichaa, watu wendawazimu halafu madini yetu na mali yetu vichukuliwe..."*

(c) *Naendelea kunukuu "Mnajuliza tunalazimishia nini? Kama ni hela kiasi gani? Kwa ajili ya roho za watu? Ni nini hiki mnafanya? Nataka mnijibu na mimi nasema atakayenisemesha nitamsemesha mara mbili"*

(d) "Bahati nzuri niko kule Bungeni, nasema humu nasema na kule, nasema rje nasema ndani, sema juu ya paa, popote, nitafyatua mtu mjengoni, namfyatua mtu rje, hakuna msamaha it is between we lose of our Nation or we have our Nation, we can't negotiate in that perspective"

(e) "Chanjo ya china haina chuma ndani ila wao. Sisi hatuwezi kuchagua chanjo ya Cuba wala China kwa sababu chanjo yao haina hela.... ya Johnson & Johnson baba lao inatanguliza dola mbele la Modenga, Astrazanac baba lao lina dola kwanza ulainike kabisa unajiliza niikatae, mtakoma kama mmekula vya watu"

(f) "Huwezi kuamua kwa maamuzi mepesi namna hii, we require time to research ya kutosha na ifanywe na Watanzania Madaktari ambao hawajapokea pesa, ukimuona, mwambie pesa hlyo, mwambie pesa, pesa, pesa, mbadala wa chanjo ambazo ni za kimila kama ya China, ya Cuba kwa sababu ambazo watu hawawezi kukubali kwa sababu hazina hela".

(g) "Kwanza watakaoanza na mimi ni watu wa makanisa ambao nao wamelipwa, wengine utawasikia huyo Gwajima kwanza ni Mbunge, wa Kanisa ukiwaona mtu anasema Gwajima sema pesa, pesa, pesa".

Mheshimiwa Spika, Mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Spika, kufuatia maelekezo yako ya kumuita Mheshimiwa Josephat Gwajima (Mb) aliiwa kwa njia ya Hati ya Wito yaani *Summons chini* ya kifungu 15 na 16 cha Sheria ya Haki, Kinga na Madaraka ya Bunge Sura ya 296. Vifungu hivyo, vinatoa mamlaka kwa Bunge kumuita mtu ye yote kufika mbele ya Bunge au Kamati kutoa ushahidi kuhusu jambo lolote kama litakavyokuwa limefafanuliwa katika Hati ya Wito.

Mheshimiwa Spika, Uchambuzi wa Shauri, Bunge lina mamlaka kisheria ya kusikiliza na kutoa hukumu kwa makosa yanayovunja Haki za Bunge ambayo si jinai chini ya Sheria

hii. Mamlaka hayo yapo chini ya Kifungu cha 13 cha Sheria ya Kinga, Madaraka na Haki za Bunge, Sura ya 296.

Mheshimiwa Spika, Uchambuzi wa hoja za msingi, Kamati ilifanya uchambuzi wa malalamiko yanayomkabili Mheshimiwa Josephat Gwajima ili kupata ukweli utakaoiwezesha Kamati kufikia uamuzi katika uchambuzi. Kamati ilijielekeza katika kupata majibu yafuatayo:-

(a) Mheshimiwa Josephat Gwajima alitoa kauli zinazolalamikiwa na je, kauli hizo:-

(i) Zinadhalilisha nafasi ya Mbunge na kushusha heshima ya Bunge, Wabunge na viongozi?

(ii) Je, zinachonganisha Mhimili wa Bunge dhidi ya Mhimili wa Serikali, Serikali na Wananchi, Bunge?

(iii) Zinaonesha dharau na kushusha heshima ya Bunge, Shughuli za Bunge na Uongozi wa Bunge?

Mheshimiwa Spika, katika kujibu hoja ya kwanza, Kamati ilipitia na kuchambua ushahidi ufuatao: -

(a) Picha za Video zilizosambazwa katika vyombo vya habari na mitandao ya kijamii yaani *Twitter, YouTube, WhatsApp na Facebook* vikimnukuu Mheshimiwa Josephat Mathias Gwajima katika nyakati tofauti ambazo ni tarehe 25 Julai, 2021, 1 Agosti, 2021, 8 Agosti, 2021 na 15 Agosti, 2021 akiwa maeneo ya Ubungo katika Jijini la Dar es Salaam akitoa kauli zinazolalamikiwa.

(b) Ushahidi wa maelezo ya mdomo wa Mheshimiwa Josephat Mathias Gwajima alioutoa mbele ya Kamati.

Mheshimiwa Spika, Kamati iliona ushahidi wa picha za video zilizonukuliwa ambazo zilisambazwa kwenye mitandao ya kijamii. Ushahidi unamwonesha Mheshimiwa Josephat Gwajima akitoa kauli zinazolalamikiwa katika shauri hili.

Mheshimiwa Spika, ushahidi wa *video* ni ushahidi wa kielektroniki ambao unakubalika kisheria kwa mujibu wa kifungu cha 40A (a) na (b) cha Sheria ya Ushahidi *yaani The Evidence Act, Cap 6.* Naomba nikinuu Kifungu 40A kinasema:- *"In any criminal proceedings: -*

(a) an information retrieved from computer system, networks or servers;

(b) the records retrieved from computer systems, networks or servers; or records obtained through surveillance of means of preservation of information including facsimile machines, electronic transmission and communication facilities; shall be admissible in evidence." (Makofi)

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Josephat Gwajima alifika mbele ya Kamati na kuhojiwa siku ya Jumatatu tarehe 23 Agosti, 2021 na siku ya Jumatano tarehe 25 Agosti 2021. Katika mahojiano hayo, shahidi alikiri kwa kinywa chake kuwa kauli zote zinazolalamikiwa alizitamka, kwa maneno yake alisema; namnukuu alisema:

"Mheshimiwa mwenyekiti kauli hizi ni zangu hundred percent (100%) zote kama zilivyo na kauli hizi ni mahubiri ya Kanisani Askofu anazungumza na watu wake;" Mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Spika, katika utetezi wake, alieleza kuwa alichokisema ni mahubiri ya Kanisani na haoni uhalali wa kauli zinazotolewa makanisani kujadiliwa mbele ya Kamati. Katika ushahidi wake alieleza kama ifuatavyo naomba kunukuu:-

"...niliyasema nikiwa kanisani nasema kama Askofu wa Kanisa, kauli yangu ni Kanisani wanafundishwa Neno la Mungu.

Niseme kweli kosa kubwa linalofanyika ni kujaribu kuyakosoa mahubiri ambayo mimi nayahubiri hili ni kosa; hayo ni mahubiri yatatafsirika kwa namna ya doctrine ya kanisa huwezi ku-question mahubiri nielezee mbele ya Kamati

niliyohubiri kanisani. Makanisa mangapi yanakuja kuelezea mahubiri yao kwenye Kamati ya Bunge, hii sio sawa..." Mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilitafakari kuhusu utetezi huo na kujiuliza kama kauli zinazotolewa katika nyumba za ibada zina kinga ya kuhojiwa na Kamati. Katika kuliangalia jambo hili Kamati ilijielekeza katika Masharti ya Ibara ya 19 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, 1977, inayohusu uhuru wa mtu kuamini dini aitakayo.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilijiridhisha kuwa, Katiba imetamka kuwa mtu yejote anao uhuru wa kuabudu lakini pia imeelekeza kufuatwa kwa sheria za nchi ili kulinda usalama na amani katika jamii, maadili na umoja wa kitaifa. Ibara hiyo inaeleza ifuatavyo: (*Makofi*)

"Ibara ya 19 (1) Kila mtu anastahili kuwa na uhuru wa mawazo, imani na uchaguzi katika mambo ya dini, pamoja na uhuru wa mtu kubadilisha dini au imani yake.

Kifungu Kidogo cha (3) Hifadhi ya haki zilizotajwa katika ibara hii itakuwa chini ya taratibu zilizowekwa na sheria ambazo ni muhimu katika jamii ya kidemokrasia kwa ajili ya usalama wa jamii, amani katika jamii, maadili ya jamii na umoja wa kitaifa."

Mheshimiwa Spika, Kamati iliendelea kutafakari kuhusu suala la haki na uhuru wa watu kwa mujibu wa Katiba. Ibara ya 30 ya Katiba inaweka mipaka kuhusu haki na uhuru wa watu chini ya Katiba. Naomba nikuu Ibara 30(1) na (2):

"(1) Haki na uhuru wa binadamu ambavyo misingi yake imenorodheshwa katika Katiba hii havitatumiwa na mtu mmoja kwa maana ambayo itasababisha kuingiliwa kati au kukatizwa kwa haki na uhuru wa watu wengine au maslahi ya umma.

(2) Ifahamike kwamba masharti yaliyomo katika Sehemu hii ya Katiba, yanafafanua misingi ya haki, uhuru na

wajibu wa binadamu, hayaharamishi sheria yoyote iliyotungwa wala kuzuia sheria yoyote kutungwa au jambo lolote halali kufanywa kwa mujibu wa sheria hiyo.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia mipaka ya haki na uhuru uliowekwa chini ya Katiba, Kamati inaona kuwa Masharti ya Ibara ya 30 ya Katiba ni muhimu yazingatiwe ili kulinda na kudumisha ulinzi, usalama, amani katika jamii, maadili ya jamii, au maslahi mengine ya umma.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilijiridhisha kuwa mahubiri yanayotolewa katika mikusanyiko ya dini au nyumba za ibada yanapaswa kuzingatia sheria za nchi na taratibu zilizowekwa kulinda Amani, usalama na maslahi ya umma. Hivyo, kauli zinazotolewa katika mikusanyiko hiyo iwe wakati wa mahubiri au kwa vyovyote itakavyokuwa haziwezi kuwa na kinga ya kuhojiwa.

Mheshimiwa Spika, Kamati iliangularia shauri la jinai liliomkabili Mchungaji Melkizedeki Bubelwa. Mchungaji huyu alihukumiwa kifungo cha miezi sita jela na kulipa faini ya shilingi milioni moja kwa kosa la kuwazuia watoto wake kwenda shule kwa madai kuwa neno la Mungu linakataza watoto kupata elimu dunia. Shauri hilo ni kesi namba 35 ya Mwaka 2021 ilioamuriwa katika Mahakama ya Wilaya ya Bukoba. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, baada ya Mbunge kuapishwa anaendelea kutumikia nafasi hiyo hadi Ubunge wake utakapokoma. Upo ugumu wa kutenganisha cheo cha Mbunge na nyadhifa nyingine ambazo Mbunge anazitumikia katika mazingira tofauti. Mheshimiwa Josephat Gwajima ni Mbunge wa Jimbo la Kawe hivyo haupo uwezekano wa kudai kwamba kuna nyakati Ubunge wake unawekwa pemberi naye kutumika kama kiongozi wa dini. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, Kamati ilijiridhisha kuwa mara baada ya kuapishwa, Mbunge huendelea kushika nafasi ya Ubunge kwa kipindi cha miaka mitano iwapo hatakoma kuwa Mbunge. Hivyo, Mheshimiwa Josephat Gwajima wakati

anatoa kauli zinazolalamikiwa, alizitoa alikuwa ni Mbunge.
(Makofii)

Mheshimiwa Spika, shahidi alikiri hayo wakati wa mahojiano alipoulizwa swali iwapo kofia ya uongozi wa dini inatenganishwa na Ubunge au vinakwenda pamoja. Kwa maneno yake alisema yafuatayo naomba kunukuu:

"zinakwenda pamoja, ndiyo maana Bungeni hadhi yangu nipo nimesajiliwa kama Mheshimiwa Askofu Josephat Mathias Gwajima, kanisani nilitaja Ubunge kwa sababu kuna issue nilikuwa nahitaji ku-address kwa washirika wangu wanaojuu mimi ni Askofu lakini pia ni Mbunge" Mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Josephat Gwajima ni Mbunge na kiongozi. Kwa nafasi hiyo anatakiwa kuwa mfano bora wa kuigwa na wananchi. Kiongozi yoyote anatakiwa kujiepusha na vitendo vya kudharau na kudhalilisha Bunge, Mamlaka ya Spika, Serikali na Viongozi wa Serikali. Vile vile kiongozi awajibike kuzingatia sheria, Kanuni na taratibu za uendeshaji wa Bunge na Serikali kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, tuhuma za kuchonganisha Mhimili wa Bunge dhidi ya Mhimili wa Serikali, Serikali na wananchi, Bunge na wananchi, zinajidhahirisha wazi katika kauli za Mheshimiwa Josephat Gwajima. Nanukuu kwa kauli hiyo ya Mheshiwa Josephat Gwajima anasema:

Mwanasayansi ambaye hajachukua hela, ambaye hajala hela kwa ajili ya kuchanjwa aliyechukua hela ataniambia nini? Mmekula hela vya watu unataka uwatimizie watu sawasawa na hela yao na mimi siwezi kukubali kutoa watu kafara, Watanzania eti tuishi mahali hakuna Taifa watu hawazai, watu vichaa watu wendawazimu halafu madini yetu ni mali yetu vichukuliwe, mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Spika, hali kadhalika kauli za Mheshimiwa Josephat Gwajima zinagonganisha, zinchonganisha na

kufarakanisha Serikali na wananchi, kwa kuwaaminisha kuwa Serikali inawalazimisha wananchi kuchanja wakati jambo hilo ni la hiari.

Mheshimiwa Spika, kauli zinazotolewa mathalani kwamba anayekubali chanjo amepokea pesa kutoka nje ya nchi na kampuni zinazozalisha chanjo jambo linalotafsiriwa kuwa ni rushwa. Kauli hizi zinaathiri mahusiano kati ya nchi yetu na nchi nyingine, jambo hili ni dosari kwa kiongozi anayetumia nafasi ya Mbunge.

Mheshimiwa Spika, katika kumhoji Shahidi Kamati ilitaka kufahamu Shahidi anaziona changamoto zinazotokana na kauli zake ikiwemo kudhalilisha Bunge na Wabunge pamoja na kuleta migongano kati ya Serikali, Bunge na wananchi, Shahidi huyo alijibu kwamba yeye hajutii kauli zake na kwamba ataendelea kutoa kauli za kusisitiza kwamba anachokieleza ndiyo ukweli.

Mheshimiwa Spika, baada ya Kamati kujibu hoja hizo ilijielekeza katika kujibu hoja nyingine kwamba Je, kauli hizo zinakiuka kifungu cha 13(1) 26(d) na (e) cha Sheria ya Kinga, Haki na Madaraka ya Bunge Sura ya 296 Toleo la 2020 na Kanuni ya 85(1) (g) ya Kanuni za Kudumu za Bunge za mwaka 2020.

Mheshimiwa Spika, Kamati imejiridhisha kuwa kauli zilizotolewa na Mheshimiwa Josephat Gwajima zinadhalilisha nafasi ya Mbunge, zinashusha heshima ya Bunge, Wabunge na Viongozi, zinachonganisha Mhimili wa Bunge dhidi ya Mhimili wa Serikali. Serikali na wananchi, Bunge na wananchi.

Mheshimiwa Spika, vilevile kauli hizo zinaonesha dharau na kushusha heshima ya Bunge, shughuli za Bunge na uongozi wa Bunge. Kwa mantiki hiyo, kauli hizo zinakiuka Kifungu cha 26 (d) na (e) ambacho kinamzuia mtu yejote kudharau, kudhalilisha, kushusha hadhi na heshima ya Bunge, shughuli za Bunge au mtu yejote anayeendesha shughuli hizo.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilitafakari na kupima kauli zilizotolewa na Mheshimiwa Josephat Gwajima iwapo zinakiuka Kanuni ya 85(1) (g) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, inaweka masharti kuhusu utovu wa nidhamu uliokithiri. Kamati ilitafakari kauli zifuatazo zilizolenga Bunge na zinazoilenga Serikali. Nanukuu kutoka kwenye kauli za Mheshimiwa Josephat Gwajima kama ifuatavyo: "*Mimi nikisema, imeshakuwa. Bahati nzuri niko kule Bungeni, nasema humu nasema na kule, nasema nje nasema na ndani, nasema juu ya paa, popote. Nafyatua mtu mjengoni, namfyatua mtu nje hakuna msamaha*"

Mheshimiwa Spika, Bunge linaongozwa kwa mujibu wa Katiba na Sheria na Kanuni ambapo kiongozi wake ni wewe Mheshimiwa Spika, kitendo cha Mheshimiwa Josephat Gwajima kutoa kauli zinazoonesha kuwa hakuna wa kumzuia na kwamba wakati wowote atatoa kauli anavyotaka kwa maneno kwamba nikisema imeshakuwa ni utovu wa nidhamu uliokithiri kwa nafasi yake kama Mbunge na ni kiongozi katika Taifa ambaye hapaswi kuongozwa na sheria za uongozi wake. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Josephat Gwajima alishindwa kuthibitisha kauli zake na wala hakuwa na kielelezo chochote cha kauli zake licha ya kuuaminisha umma kuwa anao ushahidi.

Naomba nirudie sehemu hiyo. Mheshimiwa Josephat Gwajima alishindwa kuthibitisha kauli zake na wala hakuwa na kielelezo chochote cha kauli zake licha ya kuuaminisha umma kuwa anao ushahidi. Shahidi huyu alisema uongo kwa kuwaaminisha watu kwamba chanjo pekee iliyoingizwa nchini ni *Johnson and Johnson* na kuwa chanjo kutoka China hajaingizwa nchini. Kamati ilibaini chanjo zaidi ya *Johnson and Johnson* zipo nchini ambazo chanjo toka China zipo Zanzibar. Vilevile, suala la viongozi kupewa rushwa hakutoa ushahidi wowote.

Mheshimiwa Spika, vitendo hivyo vinakiuka kifungu cha 26(d) na (e) cha Sheria ya Kinga, Haki na Madaraka ya

Bunge vilevile kauli hizo zinaonesha utovu wa nidhamu uliokithiri chini ya Kanuni ya 85(1)(g) ya Kanuni za Kudumu za Bunge.

Mheshimiwa Spika, Kamati kwa kauli moja ilimtia hatiani Mheshimiwa Josephat Gwajima. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kutafakari kauli zilitolewa na ushahidi mbele ya Kamati pamoja na vifungu vyta sheria vinavyozua vitendo alivyofanya na kujiridhisha, Kamati ilijielekeza katika kujibu hoja kuhusu hatua za kisheria zinazopaswa kuchukuliwa dhidi yake.

Mheshimiwa Spika, kuhusu adhabu kwa kosa la utovu wa nidhamu uliokithiri, Kamati ilijielekeza katika Kanuni ya 85(3) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Juni, 2020. Kanuni hii inaweka adhabu kwa Mbunge anayekiuka Kanuni hii kuwa asihudhurie Mikutano ya Bunge mfululizo isiyopungua miwili au isiyozidi mitatu. Kanuni inaeleza Kanuni ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge itashughulikia shauri hilo na ikithibitika Mbunge husika alitenda kosa inaweza kushauri kwamba Mbunge huyo asihudhurie mikutano mfululizo isiyopungua miwili au isiyozidi mitatu.

Mheshimiwa Spika, pia tulienda kwenye mashauri ambayo yameshawahi kuamuliwa na Bunge hili ambalo kauli zilitolewa ndani ya sehemu ya kuabudia. Tuliangalia pia shauri la Mheshimiwa Saed Kubenea ambaye alikuwa Mbunge katika Bunge la Kumi na Moja, alitoa kauli za kudharau Bunge akiwa kanisani. Kamati ilichunguza na kutoa mapendekezo kuhusu hatua za kuchukua.

Mheshimiwa Spika, vitendo vyta sheria Shahidi wakati wa usikilizaji wa shauri lake. Kamati ilifanya tathmini ya mwenendo na tabia ambazo shahidi alizionesha mara alipofika kuhojiwa mbele ya Kamati.

Kamati ilishangazwa na vitendo alivyofanya na hivyo imeona kuwa shahidi ni mjeuri ambaye aliletu dharau kwa Kamati. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tarehe 23 Agosti, Shahidi alifika mbele ya Kamati, alipokaribishwa kuketi kwenye kitit cha Shahidi alikataa kwa kusema hawezi kukalia kitit hicho na akachukua kitit kingine, Kamati iliona siyo shida ikamruhusu. Baada ya hapo, Kamati ilipomtaka azungumze alikataa kutumia kipaza sauti kilichokuwepo na kudai kibadilishwe, Kamati pia iliona ikidhi matakwa ya moyo wake ikambadilishia.

Mheshimiwa Spika, kama hiyo haitoshi, tarehe 25 Agosti, 2021 Shahidi alifika tena mbele ya Kamati alipoitwa kuendelea kutoa Ushahidi, alilingia ndani ya ukumbi kama alivyotakiwa, alipoelekezwa kuketi alikataa akidai anapenda kuzungumza akiwa amesimama. Hata katika hili Kamati iliona imvumilie.

Mheshimiwa Spika, pamoja na vituko hivyo, ushahidi wa Mheshimiwa Josephat Gwajima hakutoa ushirikiano wa kuridhisha kwa sababu sehemu kubwa hakuwa akijibu maswali kama alivyoulizwa, majibu yake kwa maswali hata yaliyokuwa ya kawaida aling'ang'ania kueleza masuala ya imani yake na kusisitiza kuwa aliongea kama kiongozi wa Kimataifa wa kanisa lake na hotuba zake zilisambaa Duniani kote na siyo Tanzania pekee. Zaidi ya hivyo, majibu yake yalijikita kwamba Kamati haina mamlaka ya kuhoji mahubiri ya kanisani.

Mheshimiwa Spika, Kamati iliona kuwa shahidi hakuitendea haki Kamati kwa vitendo alivyofanya, Kamati inaeleza hivyo kwa sababu Shahidi anaelewa vema utaratibu unaozingatiwa na Kamati wakati wa kuendesha mashauri kwa kuzingatia kuwa akiwa ni Mjumbe wa Kamati, alikuwepo wakati Kamati inapata mafunzo kuhusu masuala ya uendeshaji wa mashauri ya Kamati.

Mheshimiwa Spika, maoni na mapendekezo ya jumla ya Kamati kuhusu shauri hili. Pamoja na kushughulikia suala la Mheshimiwa Josephat Gwajima, Kamati imebaini masuala mbalimbali ambayo yanapaswa kufanyiwa kazi ili kuhakikisha amani na utulivu wa nchi unaendelea kudumishwa. Kutokana

na kauli mbalimbali anazozitoa Mheshimiwa Josephat Gwajima, Kamati inashauri kama ifuatavyo;

Mheshimiwa Spika, kwanza, vyombo nya kisheria vifuatilie na kuchunguza mwenendo wa vitendo nya Mheshimiwa Josephat Mathias Gwajima kwa kuwa vinaashiria uwepo wa jinai na uvunjivu wa amani na usalama wa nchi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mbili, suala hili lishughulikiwe pia kwa mujibu wa sheria na maadili ya viongozi wa umma, lifikishwe kwenye chama anachotoka ili aweze kuchukuliwa hatua kwa mujibu wa maadili ya chama chake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, huu ndiyo uchunguzi wa Kamati kuhusu shauri linalomkabili Mheshimiwa Josephat Mathias Gwajima, hivyo tunaomba Bunge liutafakari na liuzingatie wakati wa kuitisha Azimio la kuchukua hatua dhidi ya Mheshimiwa Gwajima.

Mheshimiwa Spika, hitimisho. Mwisho napenda kukushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi hii kuwasilisha maoni ya Kamati kwa niaba ya Kamati ya Kudumu ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge. Napenda nitumie nafasi hii tena kukupongeza kwa dhati kwa jinsi unavyoongoza Bunge hili ambalo ni chombo cha wawakilishi cha wananchi kusimamia na kushauri Serikali ili kuhakikisha kuwa ustawi wa wananchi unakuwa ndiyo kipaumbele cha kwanza.

Mheshimiwa Spika, kipekee nawashukuru wajumbe wa Kamati ambao wameorodheshwa wote wako pale. Aidha, tunamshukuru Mheshimiwa Naibu Spika kwa jinsi ambavyo mmekuwa mkisaidiana kuliendeleza Bunge letu Tukufu.

SPIKA: Twende kwenye Azimio sasa.

MHE. EMMANUEL A. MWAKASAKA – MWENYEKITI WA KAMATI YA BUNGE YA HAKI, MAADILI NA MADARAKA YA

BUNGE: Mheshimiwa Spika, naomba sasa niende kwenye Azimio la Kamati.

Mheshimiwa Spika, Azimio la Bunge kuhusu hatua za kuchukua dhidi ya kauli za Mheshimiwa Josephat Mathias Gwajima za kuvunja haki za Bunge, kudharau mamlaka ya Bunge na kugonganisha mihimili. Imetolewa chini ya Kifungu cha 33(1) cha Sheria ya Kinga, Madaraka na Haki za Bunge.

Mheshimiwa Spika, Kwa Kuwa Bunge a Jamhuri ya Muungano wa Tanzania linaongozwa kwa mujibu wa Katiba, Sheria na Kanuni za Kudumu za Bunge ambazo zilitungwa na Bunge lenyewe kwa ajili ya kuliongoza katika kutekeleza shughuli zake;

Na Kwa Kuwa, mnamo tarehe 21 Agosti, Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Job Ndugai kwa mujibu wa Kanuni ya 4 Fasili ya kwanza (a) ya Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge aliagiza Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge ikutane ili kufanya uchunguzi wa kauli za Mheshimiwa Josephat Mathias Gwajima za kuvunja haki za Bunge, kudharau mamlaka ya Bunge na kugonganisha Mihiimili;

Na Kwa Kuwa, Mheshimiwa Josephat Mathias Gwajima kwa nyakati tofauti tarehe 25, tarehe 01, tarehe 08 na tarehe 15 Agosti akiwa maeneo ya Ubungo Jijini Dar es Salaam alitoa kauli zilizonukuliwa katika vyombo mbalimbali nya habari na mitandao ya kijamii;

Na Kwa Kuwa, kauli zake zinalalamikiwa kuwa (a) kwanza zinadhalilisha nafasi ya Bunge na kushusha heshima ya Bunge, Wabunge na viongozi, (b) zinachonganisha Mhimili wa Bunge dhidi ya Mhimili wa Serikali, Serikali na wananchi na Bunge na wananchi, na (c) zinaonesha dharau na kushusha heshima ya Bunge, shughuli za Bunge na uongozi wa Bunge;

NA KWA KUWA, kufuatia maelezo ya Mheshimiwa Spika Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge

ilikutana kuanzia tarehe 23 Agosti, tarehe 27 Agosti na tarehe 30 Agosti, hapa Dodoma kufanya uchunguzi wa shauri la Mheshimiwa Josephat Mathias Gwajima;

NA KWA KUWA, tarehe 23 na tarehe 25 Agosti, 2021 Mheshimiwa Mathias Gwajima Mbunge alifika mbele ya Kamati na kuhojiwa kuhusiana na kauli alizotoa na katika mahojiano Mheshimiwa Josephat Gwajima alikiri kuwa kauli zinazolalamikiwa ni za kweli na kwamba ndiye aliyetoa kauli hizo;

NA KWA KUWA, Kamati ilifanya uchunguzi wa kina kuhusu kauli zilizotolewa na Mheshimiwa Josephat Mathias Gwajima na kubaini kuwa kauli hizo zinadhalilisha nafasi ya Mbunge, kushusha heshima ya Bunge, Wabunge na Viongozi. Vilevile zinachonganisha Mhimili wa Bunge dhidi ya Serikali, Serikali na wananchi pamoja na Bunge na wananchi, zinaonesha dharau na kushusha heshima ya Bunge, shughuli za Bunge na uongozi wa Bunge na zinakiuka Kifungu 26 (d) na (e) cha Sheria ya Haki, Kinga na Madaraka ya Bunge Sura 296, Toleo la 2020 na Kanuni ya 85 (1) (g) ya Kanuni za Bunge Toleo la 2020;

NA KWA KUWA, Mheshimiwa Josephat Mathias Gwajima akiwa mbele ya Kamati hakukiri wala kujutia makosa yake, alionesha dharau wala hakujutia kauli zake zinazolalamikiwa kudhalilisha nafasi ya Mbunge na kushusha heshima ya Bunge, kushusha hadhi ya Wabunge na Viongozi, kuchonganisha Mhimili wa Bunge dhidi ya Mhimili wa Serikali, Serikali na wananchi pamoja na Bunge na wananchi,

HIVYO BASI, Kamati imemtia hatiani.

NA KWA KUWA, Kanuni ya 61, (1), (2) na (3) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la 2020 inalipa Bunge mamlaka ya kupokea na kujadili mapendekezo ya Kamati hii na kisha kufanya uamuzi kwa njia ya Azimio la Bunge;

KWA HIYO BASI, Bunge linaazimia kwamba Mheshimiwa Josephat Mathias Gwajima apewe adhabu ya

kutohudhuria mikutano ya Bunge miwili mfululizo isipokuwa siku ya mwisho..... Samahani Mheshimiwa Spika naomba nirudie.

KWA HIYO BASI, Bunge linaazimia kwamba Mheshimiwa Josephat Mathias Gwajima apewe adhabu ya kutohudhuria mikutano miwili mfululizo ya Bunge baada ya kupitishwa kwa Azimio hili.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

MHE. SHALLY J. RAYMOND: Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)*

**TAARIFA YA KAMATI YA HAKI, MAADILI NA MADARAKA YA
BUNGE KUHUSU TUHUMA ZINAZOMKABILI
MHE. JOSEPHAT MATHIAS GWAJIMA (MB)
ZA KUVUNJA HAKI ZA BUNGE, KUDHARAU MAMILAKA YA
BUNGE NA KUGONGANISHA MIHIMILI - KAMA
ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

1.0 UTANGULIZI

1.1 **Mheshimiwa Spika**, Kwa mujibu wa Kanuni ya 4(2) na (3) ya Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020, naomba kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu, Taarifa ya Kamati kuhusu tuhuma zinazomkabili **Mhe. Josephat Mathias Gwajima (Mb)** za kuvunja haki za Bunge, kudharau mamlaka ya Bunge na kugonganisha mihimili.

1.2 **Mheshimiwa Spika**, napenda kukushukuru wewe binafsi kwa busara na hekima zako katika kuliongoza Bunge letu kwa ufanisi mkubwa. Aidha, tunakushukuru kwa namna unavyosimamia, kuulinda na kuutetea Mhimili huu muhimu na juhudhi zako za kuhakikisha Bunge linathaminiwa na kuheshimiwa na kila mtu hivyo kutekeleza majukumu yake ya kikatiba na kisheria bila kudhalilishwa, kuvunjiwa heshima na hadhi linayostahili.

1.3 **Mheshimiwa Spika**, aidha, napenda kumshukuru Naibu Spika na Wenyeviti wote wa Bunge letu kwa namna wanavyokusaidia katika kutekeleza majukumu yako.

1.4 **Mheshimiwa Spika**, mnamo tarehe 20 Agosti 2021 kwa Mamlaka uliyonayo chini ya Kanuni ya 4(1) (a) na (b) ya Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020, uliiagiza Kamati yangu kukutana kwa ajili ya kushughulikia suala la tuhuma dhidi ya **Mhe Josephat Gwajima (Mb)** kudharau, kudhalilisha na kushusha heshima ya Bunge na kugonganisha mihimili. Katika maelekezo yako ultiitaka Kamati hii kufanya uchunguzi ili kubaini kama ni kweli Mhe Josephat Mathias Gwajima alihusika na tuhuma hizo na kupendekeza hatua za kuchukua dhidi yake.

1.5 **Mheshimiwa Spika**, Kamati ilikutana tarehe 23 Agosti, 2021 hadi 27 Agosti, 2021 kwa ajili ya kushughulikia suala hilo kwa mujibu wa Kanuni ya 4(1) (a) na (b) ya Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni 2020. Kwa urahisi wa rejea nanukuu kifungu hicho:

“4(1) Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge itatekeleza majukumu yafatayo:-

(c) Kuchunguza na kutoa mapendekezo kuhusu masuala yote ya Haki, Kinga na Madaraka ya Bunge yatakayopelekwa na Spika;

(d) Kushughulikia mambo yanayohusu maadili ya Wabunge yatakayopelekwa na Spika.

2.0 CHIMBUKO LA SHAURI

2.1 **Mheshimiwa Spika**, shauri hili linatokana na kauli mbalimbali zilizotolewa na **Mhe. Josephat Gwajima** kwa nyakati tofauti ambazo ni tarehe 25 Julai, 2021, 1 Agosti, 2021, 8 Agosti, 2021 na 15 Agosti, 2021 akiwa maeneo ya Ubungo Jijini la Dar es Salaam. Kauli hizo zilinukuliwa katika vyombo mbalimbali vyaa habari na mitandao ya kijamii (*Twitter, YouTube, WhatsApp na Facebook*).

2.2 **Mheshimiwa Spika**, zifuatazo ni mionganini mwa kauli zinazolalamikiwa:

(a) "Juzi juzi kukawa na kauvumi uvumi ka-twitter sijui kalikuwa kanani kale kanasema eti Gwajima hataruhusiwa kuingia Bungeni mpaka achanjwe kwanza, kalikuwa kanatembea..."

(b) *Baadaye Mheshimiwa Ofisi ya Spika wakakanusha wakasema hiyo siyo twitter yetu, ni uongo. Nikawa nasema mimi hata kama ingekuwa kweli, mimi kuchanjwa ng'oo! Hachanjwi mtu hapa! Hachanjwi mtu hapa! Hata kama, hata kama ingekuwa kweli kwamba usiingie hachanjwi mtu. Hata kwa dakika moja, yaani niko macho hivi. Hata kwenye ndoto hunichanji ...*

(c) *Baadaye nimeona Ofisi ya Spika wakakanusha wakasema siyo kweli, lakini mimi nilikuwa nimejiandaa tu sina wasiwasi. Bunge linaanza kesho. Kamati zinaanza kesho. Mimi sina wasiwasi.*

(d) *Hachanjwi mtu hapa! Ikishindikana narudi hapa nyumbani. Mnanielewa eeh? Ubunge ni mzuri, Ubunge ni kusaidia Wananchi, Ubunge una heshima, Ubunge ni jambo zuri ila kunichanja, hakuna! Mimi nikisema imeshakuwa..."*

2.3 **Mheshimiwa Spika**, kauli nytingine zilizotolewa na Mheshimiwa Josephat Gwajima ni:

(a) "...Unayeona anabisha amepewa hela, nataka mwanasayansi ambaye hajachukua hela aje hapa tujadiliane, wale ambao mmeshachukua hela ya kidampa hamna haja ya kuniambia chochote, mwanasayansi ambaye hajachukua hela ambaye hajala hela kwa ajili ya kuchanjwa aliyechukua hela utaniambia nini?

(b) *Mmekula hela vya watu unataka uwatimizie watu sawasawa na hela yao na mimi siwezi kukubali kutoa watu kupata kafala Watanzania eti tuishi mahali hakuna Taifa, watu hawazai, watu vichaa, watu wendawazimu halafu madini yetu na mali yetu vichukuliwe..."*

(c) “....Mnajuliza tunalazimishia nini? Kama ni hela kiasi gani? Kwa ajili ya roho za watu? Ni nini hiki mnafanya? Nataka mnijibu, na mimi nasema atakayenisemesha nitamsemesha mara mbili...”

(d) “....Bahati nzuri niko kule Bungeni nasema humu nasema na kule, nasema nje nasema ndani, sema juu ya paa, popote, nitafyatua mtu mjengoni, namfyatua mtu nje, hakuna msamaha... it is between we loose of our Nation or we have our Nation, we can't negotiate in that perspective”

(e) “*Chanjo ya china haina chuma ndani ila wao.... Sisi hatuwezi kuchagua chanjo ya Cuba wala China kwa sababu chanjo yao haina hela.... ya Johnson Johnson baba lao inatanguliza dola mbele la Mondenga, Astrazanac baba lao lina dola kwanza ulainike kabisa unajiuliza niikatae, mtakoma kama mmekula vya watu...*”

(f) “*Huwezi kuamua kwa maamuzi mepesi namna hii, we require time na research ya kutosha na ifanywe na Watananzania Madaktari ambaao hawajapokea pesa, ukimwona ... mwambie pesa hiyo, mwambie pesa, pesa, pesa, mbadala wa chanjo ambazo ni za kimila kama ya China, ya Cuba kwa sababu ambazo watu hawawezi kukubali kwa sababu hazina hela*”.

(g) “*Kwanza watakaoanza na mimi ni watu wa makanisa ambaao nao wamelipwa, wengine utawasikia huyo Gwajima kwanza ni Mbunge..., wa Kanisa ukiwaona mtu anasema Gwajima sema pesa, pesa, pesa*”.

2.4 **Mheshimiwa Spika**, kufuatia maelekezo yako ya kumuita Mhe Josephat Gwajima (Mb) aliiwa kwa njia ya Hati ya Wito (*Summons*) chini ya kifungu 15 na 16 cha Sheria ya Kinga, Haki na Madaraka ya Bunge Sura ya 296. Vifungu hivyo, vinatoa mamlaka kwa Bunge kumuita mtu yejote kufika mbele ya Bunge au Kamati kutoa ushahidi kuhusu jambo lolote kama litakavyofafanuliwa katika Hati ya Wito.

2.5 **Mheshimiwa Spika**, Hati ya Wito ilimtaka shahidi kutoa maelezo juu ya kuhusika au kutohusika kwake na tuhuma zinazomkabili za:

(a) kudhalilisha nafasi ya Mbunge na kushusha heshima ya Bunge, Wabunge na viongozi.

(b) kugonganisha Mhimili wa Bunge dhidi ya Mhimili wa Serikali, Serikali na Wananchi, Bunge na Wananchi, na

(c) kuonesha dharau na kushusha heshima ya Bunge, Shughuli za Bunge na Uongozi wa Bunge.

2.6 **Mheshimiwa Spika**, aidha hati ilimtaka Mhe. Josephat Gwajima aeleze kama ikibainika ni kweli, ni kwanini asichukuliwe hatua kwa kukiuka Kifungu cha 26(d) na (e) cha Sheria ya Kinga, Haki na Madaraka ya Bunge Sura ya 296 na Kanuni ya 85(1)(g) ya Kanuni za Kudumu za Bunge. Sheria na Kanuni hizo zinakataza mtu ye yeyote kufanya vitendo alivyotuhumiwa kuvifanya.

3.0 UCHAMBUZI WA SHAURI

3.1 **Mheshimiwa Spika**, Bunge lina mamlaka kisheria ya kusikiliza na kutoa hukumu kwa makosa yanayovunja Haki za Bunge ambayo si jinai chini ya Sheria hii. Mamlaka hayo yapo chini ya Kifungu cha 13 cha Sheria ya Kinga, Madaraka na Haki za Bunge, Sura ya 296. Kifungu kinaeleza ifuatavyo:-

“13 (1) It is declared for avoidance of doubt that subject to the constitution and standing Orders of the Assembly, the Assembly has all such powers and jurisdiction as may be necessary for inquiring into, judging and pronouncing upon commission of any act, matter or thing, not amounting to an offence under this Act, which is a breach of Parliamentary privileges.”

3.2 **Mheshimiwa Spika**, katika kufanya uchunguzi Kamati imefanya rejea ya nyaraka zifuatazo:

- (i) Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977;
- (ii) Sheria ya Kinga, Haki na Madaraka ya Bunge Sura ya 296;
- (iii) Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020;
- (iv) Erskine May, Treaties on the Law, Privileges, Proceedings and Usage of Parliament, Erskine May, 22nd Edition, Butterworth, London 1983;
- (v) Machapisho ya mitandao ya kijamii na picha za video yenye sehemu zinayoonyesha Mhe. Josephat Mathias Gwajima (Mb) akitoa kauli zinazolalamikiwa; na
- (vi) Mashauri mbalimbali yaliyowahi kuamuliwa na Bunge (*Precedent*).

3.3 Uchambuzi wa hoja za msingi

3.3.1 Mheshimiwa Spika, Kamati ilifanya uchambuzi wa malalamiko yanayomkabili Mhe. Josephat Gwajima ili kupata ukweli utakaoiwezesha Kamati kufikia uamuzi. Katika uchambuzi, Kamati illijielekeza katika kupata majibu ya maswali yafuatayo:

- (a)Je, Mheshimiwa Josephat Gwajima (Mb) alitoa kauli zinazolalamikiwa na je, kauli hizo-
 - (i) Zinadhalilisha nafasi ya Mbunge na kushusha heshima ya Bunge, Wabunge na viongozi?
 - (ii) Zinagonganisha Mhimili wa Bunge dhidi ya Mhimili wa Serikali, Serikali na Wananchi, Bunge na Wananchi?
 - (iii)Zinaonesha dharau na kushusha heshima ya Bunge, Shughuli za Bunge na Uongozi wa Bunge?
- (b)Je, kauli hizo zinakiuka Kifungu cha 13(1) na (2), 26(d) na (e) cha Sheria ya Kinga, Haki na Madaraka ya Bunge, Sura

ya 296 Toleo la 2020 na Kanuni ya 85 (1)(g) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020?

(c) Ikiwa hoja (a) na (b) zitathibitika, ni hatua gani zinapaswa kuchukuliwa kwa mujibu wa Sheria na Kanuni za Bunge?

3.3.2 **Mheshimiwa Spika**, katika kujibu hoja ya kwanza, Kamati ilipitia na kuchambua ushahidi ufuatao:-

(a) Picha za Video zilizosambazwa katika vyombo vya habari na mitandao ya kijamii (*Twitter, YouTube, WhatsApp na Facebook*) vikimnukuu Mhe. Josephat Mathias Gwajima katika nyakati tofauti ambazo ni tarehe 25 Julai, 2021, 1 Agosti, 2021, 8 Agosti, 2021 na 15 Agosti, 2021 akiwa maeneo ya Ubungo katika Jijini la Dar es Salaam akitoa kauli zinazolalamikiwa.

(b) Ushahidi wa maelezo ya mdomo wa Mhe. Josephat Mathias Gwajima alioutoa mbele ya Kamati.

3.3.3 **Mheshimiwa Spika**, Kamati iliona Ushahidi wa picha za video zilizonukuliwa ambazo zilisambazwa kwenye mitandao ya kijamii. Ushahidi unamwonesha Mhe. Josephat Gwakima akitoa kauli zinazolalamikiwa katika shauri hili.

Mheshimiwa Spika, ushahidi wa video ni ushahidi wa kielektroniki ambao unakubalika kisheria kwa mujibu wa kifungu cha 40A (a) na (b) cha Sheria ya Ushahidi (*The Evidence Act, Cap 6*). Kifungu hicho kinaeleza ifuatavyo:

"40A. In any criminal proceedings-

- (a) an information retrieved from computer system, networks or servers;*
- (b) the records retrieved from computer systems, networks or servers; or records obtained through surveillance of means of preservation of information including facsimile machines, electronic transmission and communication facilities;*
- (c)*

shall be admissible in evidence.

3.3.4 **Mheshimiwa Spika**, Mheshimiwa Josephat Gwajima alifika mbele ya Kamati na kuhojiwa siku ya Jumatatu tarehe 23 Agosti, 2021 na siku ya Jumatano tarehe 25 Agosti 2021. Katika mahojiano hayo, shahidi alikiri kwa kinywa chake kuwa kauli zote zinazolalamikiwa alizitamka. Kwa maneno yake alisema:

"Mheshimiwa mwenyekiti ...kauli hizi ni zangu hundred percent (100%) zote kama zilivyo na kauli hizi ni mahubiri ya Kanisani Askofu anazungumza na watu wake; ..."

3.3.5 **Mheshimiwa Spika**, baada ya kuzingatia ushahidi wa picha za video na kukiri kwa Mhe. Josephat Gwajima kuwa alitamka kauli zinazolalamikiwa. Kamati ilijiridhisha bila shaka ye yote kuwa shahidi huyu ndiye aliyetamka kauli hizo.

3.3.6 **Mheshimiwa Spika**, katika utetezi wake, alieleza kuwa allichokisema ni mahubiri ya Kanisani na haoni uhalali wa kauli zinazotolewa makanisani kujadiliwa mbele ya Kamati. Katika ushahidi wake alieleza ifuatavyo:

"...niliyasema nikiwa kanisani nasema kama Askofu wa Kanisa ...kauli yangu ni kanisani wanafundishwa Neno la Mungu..."

...niseme kweli kosa kubwa linalofanyika ni kujaribu kuyakosoa mahubiri ambayo mimi nayahubiri hili ni kosa; hayo ni mahubiri yatatafsirika kwa namna ya doctrine ya kanisa huwezi ku- question mahubiri nielezee mbele ya Kamati niliyohubiri kanisani. Makanisa mangapi yanakuja kuelezea mahubiri yao kwenye Kamati ya Bunge, hii sio sawa..."

3.3.7 **Mheshimiwa Spika**, Kamati ilitafakari kuhusu utetezi huo, na kujiuliza kama kauli zinazotolewa katika nyumba za ibada zina kinga ya kuhojiwa na Kamati. Katika kuliangalia jambo hili Kamati ilijielekeza katika Masharti ya Ibara ya 19 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, 1977, inayohusu uhuru wa mtu kuamini dini aitakayo.

3.3.8 **Mheshimiwa Spika**, Kamati ilijiridhisha kuwa, Katiba imetamka kuwa mtu ye yote anao uhuru wa kuabudu lakini

pia imeelekeza kufuatwa kwa sheria za nchi ili kulinda usalama na amani katika jamii, maadili na umoja wa kitaifa. Ibara hiyo inaeleza ifuatavyo:

"19.- (1) Kila mtu anastahili kuwa na uhuru wa mawazo, imani na uchaguzi katika mambo ya dini, pamoja na uhuru wa mtu kubadilisha dini au imani yake.

(2)

(3) Hifadhi ya haki zilizotajwa katika ibara hii itakuwa chini ya taratibu zilizowekwa na sheria ambazo ni muhimu katika jamii ya kidemokrasia kwa ajili ya usalama wa jamii, amani katika jamii, maadili ya jamii na umoja wa kitaifa."

3.3.9 **Mheshimiwa Spika**, aidha, Kamati iliendelea kutafakari kuhusu suala la haki na uhuru wa watu kwa mujibu wa Katiba. Ibara ya 30 ya Katiba inaweka mipaka kuhusu haki na uhuru wa watu chini ya Katiba. Ibara hiyo inaeleza:

"30.- (1) Haki na uhuru wa binadamu ambavyo misingi yake imenorodheshwa katika Katiba hii havitatumwa na mtu mmoja kwa maana ambayo itasababisha kuingiliwa kati au kukatizwa kwa haki na uhuru wa watu wengine au maslahi ya umma.

(2) Ifahamike kwamba masharti yaliyomo katika Sehemu hii ya Katiba hii, yanayofafanua misingi ya haki, uhuru na wajibu wa binadamu, hayaharamishi sheria yoyote iliyotungwa wala kuzuia sheria yoyote kutungwa au jambo lolote halali kufanywa kwa mujibu wa sheria hiyo, kwa ajili ya-

(a) kuhakikisha kwamba haki na uhuru wa watu wengine au maslahi ya umma haviathiriwi na matumizi mabaya ya uhuru na haki za watu binafsi;

(b) kuhakikisha ulinzi, usalama wa jamii, amani katika jamii, maadili ya jamii, afya ya jamii... au maslahi mengineyo yoyote kwa nia ya kukuza manufaa ya umma;"

3.3.10 **Mheshimiwa Spika**, kwa kuzingatia mipaka ya haki na uhuru uliowekwa chini ya Katiba, Kamati inaona kuwa Masharti ya Ibara ya 30 ya Katiba ni muhimu yazingatiwe ili kulinda na kudumisha ulinzi, usalama, amani katika jamii, maadili ya jamii, au maslahi mengineyo ya umma.

3.3.11 **Mheshimiwa Spika**, Kamati ilijiridhisha kuwa mahubiri yanayotolewa katika mikusanyiko ya dini au nyumba za ibada yanapaswa kuzingatia sheria za nchi na taratibu zilizowekwa kulinda Amani, usalama na maslahi ya umma. Hivyo, kauli zinazotolewa katika mikusanyiko hiyo iwe wakati wa mahubiri au kwa vyovyote itakayyokuwa haziwezi kuwa na kinga ya kuhojiwa.

3.3.12 **Mheshimiwa Spika**, wakati wa majadiliano, Kamati ilitoa mifano mbalimbali kuhusu kauli na matukio yanayovunja sheria yaliyofanywa na viongozi wa dini na imani mbalimbali katika mikusanyiko ya dini au nyumba za Ibada. Kamati ilijiridhisha kwamba viongozi wote waliota kauli zinazokiuka sheria walichukuliwa hatua stahiki kwa mujibu wa sheria. Aidha, ilibainika kuwa utetezi wa viongozi hao ulikuwa kwamba wanatekeleza maagizo ya Mungu au wanaongea na wafiasi wao au wapo ndani ya nyumba za ibada, utetezi wa namna hiyo haukulbaliki.

3.3.13 **Mheshimiwa Spika**, Kamati iliangalia shauri la jinai liliomkabili Mchungaji Melkizedeki Bubelwa. Mchungaji huyu alihukumiwa kifungo cha miezi sita jela na kulipa faini ya shilingi milioni moja kwa kosa la kuwazuia watoto wake kwenda shule kwa madai kuwa neno la Mungu linakataza watoto kupata elimu dunia. Shauri hilo ni kesi namba 35/2021 ilioamuriwa katika Mahakama ya Wilaya ya Bukoba.

3.3.14 **Mheshimiwa Spika**, baada ya Kamati kuweka msimamo kuwa kauli zinazotolewa katika nyumba za ibada hazina kinga, Kamati iliendelea kufanya uchambuzi wa hoja nyingine kwamba, Je, kauli hizo zinashusha hadhi na heshima ya Bunge? Je, zinadharau Mamlaka ya Spika na zinachonganisha Mhimili wa Bunge na Serikali, Serikali na Wananchi na Wananchi na Bunge hali kadhalika kati ya Wananchi na Viongozi?

3.3.15 **Mheshimiwa Spika**, Kamati ilianza kuchambua tuhuma dhidi ya Mhe. Josephat Gwajima kuhusu kudhallishaa nafasi ya Mbunge na kushusha heshima ya Bunge, Wabunge

na viongozi, pamoja na hoja ya dharau na kushusha heshima ya Bunge, Shughuli za Bunge na Uongozi wa Bunge.

3.3.16 **Mheshimiwa Spika**, baada ya kuapishwa Mbunge anaendelea kutumikia nafasi hiyo hadi ubunge wake utakapokoma. Upo ugumu wa kutenganisha cheo cha Mbunge na nyadhifa nyingine ambazo Mbunge anazitumikia katika mazingira tofauti na ubunge. Mhe. Josephat Gwajima ni Mbunge wa Jimbo la Kawe hivyo haupo uwezekano wa kudai kwamba kuna nyakati ubunge wake unawekwa pembeni naye kutumika kama kiongozi wa dini.

Kamati ilijiridhisha kuwa mara baada ya kuapishwa, Mbunge huendelea kushika nafasi ya Ubunge kwa kipindi cha miaka mitano iwapo hatakoma kuwa Mbunge. Hivyo, Mhe. Josephat Gwajima wakati anatoa kauli zinazolalamikiwa, alizitoa akiwa ni Mbunge.

3.3.17 **Mheshimiwa Spika**, shahidi alikiri hayo wakati wa mahojiano alipoulizwa swali iwapo kofia ya uongozi wa dini inatenganishwa na ubunge au vinakwenda pamoja. Kwa maneno yake alisema yafuatayo:

"zinakwenda pamoja, ndiyo maana Bungeni hadhi yangu nipo nimesajiliwa kama Mheshimiwa Askofu Josephat Mathias Gwajima...kanisani nilitaja ubunge kwa sababu kuna issue nilikuwa nahitaji ku address kwa washirika wangu wanaojua mimi ni Askofu lakini pia ni Mbunge..."

3.3.18 **Mheshimiwa Spika**, kauli zote zilizotolewa na Mhe. Josephat Gwajima alizitoa kama Mbunge, jambo hili hata ye ye aliwa anatambua hivyo. Hali hiyo inatoa taswira potofu kwa Umma kuwa kauli zake ndiyo zinaweza kuwa msimamo wa Bunge na Wabunge jambo ambalo si sahihi. Kauli za namna hii zinashusha heshima ya Bunge:

3.3.19 **Mheshimiwa Spika**, Mheshimiwa Josephat Gwajima ni Mbunge na kiongozi. Kwa nafasi hiyo anatakiwa kuwa mfano bora wa kuigwa na Wananchi. Kiongozi yoyote anatakiwa kujiepusha na vitendo vya kudharau na kudhalilisha Bunge, Mamlaka ya Spika, Serikali na Viongozi

wa Serikali. Vile vile kiongozi awajibike kuzingatia sheria, Kanuni na taratibu za uendeshaji wa Bunge na Serikali kwa ujumla.

3.3.20 **Mheshimiwa Spika**, tuhuma za kuchonganisha Mhimili wa Bunge dhidi ya Mhimili wa Serikali, Serikali na Wananchi, Bunge na Wananchi, zinajidhihirisha wazi katika kauli za Mhe. Josephat Gwajima zifuatazo:

...Unayeona anabisha amepewa hela, nataka mwanasayansi ambaye hajachukua hela aje hapa tujadiliane, wale ambao mmeshachukua hela ya kidampa hamna haja ya kuniambia chochote, mwanasayansi ambaye hajachukua hela ambaye hajala hela kwa ajili ya kuchanjwa ...

...aliyechukua hela utaniambia nini? Mmekula hela nya watu unataka uwatimizie watu sawasawa na hela yao na mimi siwezi kukubali kutoa watu kafala Watanzania eti tuishi mahali hakuna Taifa, watu hawazai, watu vichaa, watu wendawazimu halafu madini yetu na mali yetu vichukuliwe...

...Mnajiuliza tunalazimishia nini? Kama ni hela kiasi gani? Kwa ajili ya roho za watu? Ni nini hiki mnafanya? Nataka mnijibu, na mimi nasema atakayenisemsha nitamsemesha mara mbili... ukimwona ... mwambie pesa hiyo, mwambie pesa, pesa, pesa, mbadala wa chanjo ambazo ni za kimila kama ya China, ya Cuba kwa sababu ambazo watu hawawezi kukubali kwa sababu hazina hela ...

...watu wa makanisa ambao nao wamelipwa, wengine utawasikia huyo Gwajima kwanza ni Mbunge..., wa Kanisa ukiwaona mtu anasema Gwajima sema pesa, pesa, pesa".

3.3.21 **Mheshimiwa Spika**, ni wazi kuwa kauli hizo zinachonganisha Mhimili wa Bunge dhidi ya Mhimili wa Serikali kwa sababu aliyezitoa ni Mbunge na yeypote aliyezisikia anaweza kudhani Mhe. Josephat Gwajima alikuwa akiwakilisha Bunge, Wabunge au uongozi wa Bunge katika suala hilo. Aidha, kauli hizo zinaweza kudhaniwa kuwa ni Bunge linapeleka ujumbe kubeza maamuzi na juhudzi za

Serikali katika kuhakikisha wananchi wanakuwa salama. Kauli hizi pia zinagongonisha Serikali na Wananchi kwa kuonesha Serikali inawalazimisha kuchanja kwa kuwa imewatoa kafala ili ipate pesa.

3.3.22 **Mheshimiwa Spika**, hali kadhalika kauli za Mhe. Josephat Gwajima zinagonganisha, zinachonganisha na kufarakanisha Serikali na Wananchi kwa kuwaaminisha kuwa Serikali inawalazimisha Wananchi kuchanja wakati jambo hilo ni la hiyari.

3.3.23 **Mheshimiwa Spika**, kauli zilizotolewa, mathalani kwamba anayekubali chanjo amepokea pesa toka nje ya nchi na kampuni zinazozalisha chanjo jambo linalotafsiriwa kuwa ni rushwa, kauli hizi zinaathiri mahusiano kati ya nchi yetu na nchi nyingine. Jambo hili ni dosari kwa kiongozi anayetumikia nafasi ya Mbunge.

3.3.24 **Mheshimiwa Spika**, katika kumhoji shahidi, Kamati ilitaka kufahamu iwapo shahidi anaziona changamoto zinazotokana na kauli zake ikiwemo kudhalilisha Bunge na Wabunge pamoja na kuleta migongano kati ya Serikali, Bunge na Wananchi. **Shahidi huyu alijibu kwamba ye ye hajutii kauli zake na kwamba ataendelea kutoa kauli za kusisitiza kwamba anachokieleza ndiyo ukweli.**

3.3.25 **Mheshimiwa Spika**, baada ya Kamati kujibu hoja hizo ilijielekeza katika kujibu hoja nyingine kwamba Je, kauli hizo zinakiuka Kifungu cha 13(1), 26(d) na (e) cha Sheria ya Kinga, Haki na Madaraka ya Bunge, Sura ya 296 Toleo la 2020 na Kanuni ya 85 (1)(g) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020?

3.3.26 **Mheshimiwa Spika**, Kamati imejiridhisha kuwa, kauli zilizotolewa na Mhe. Josephat Gwajima zinadhalilisha nafasi ya Mbunge, zinashusha heshima ya Bunge, Wabunge na viongozi, zinachonganisha Mhimili wa Bunge dhidi ya Mhimili wa Serikali, Serikali na Wananchi pamoja na Bunge na Wananchi.

3.3.27 **Mheshimiwa Spika**, vilevile kauli hizo zinaonesha dharau na kushusha heshima ya Bunge, Shughuli za Bunge na Uongozi wa Bunge. Kwa mantiki hiyo kauli hizo zinakiuka kifungu cha 26(d) na (e) ambacho kinachozuia mtu yejote kudharau, kudhalilisha, kushusha hadhi na heshima ya Bunge, shughuli za Bunge au mtu yejote anayeendesha shughuli hizo. Kifungu hicho kinaeleza:

26. Any person shall be guilty of an offence who-

(a).....

(b).....

(c).....

(d)shows disrespect in speech or manner towards the Speaker.

(e) does any other act of intentional disrespect to or with reference to the proceedings of the Assembly or to any person presiding at such proceedings".

3.3.28 **Mheshimiwa Spika**, Kamati ilitafakari na kupima kauli zilizotolewa na **Mhe. Josephat Gwajima** iwapo zinakiuka Kanuni ya 85(1)(g) ya Kanuni za Kudumu za Bunge inayoweka masharti kuhusu utovu wa nidhamu uliokithiri. Kamati ilitafakari kauli zifuatazo zililenga Bunge na zinazoilenga Serikali:

"...Mimi nikisema imeshakuwa....Bahati nzuri niko kule Bungeni nasema humu nasema na kule, nasema nje nasema ndani, sema juu ya paa, popote, nitafyatua mtu mjengoni, namfyatua mtu nje, hakuna msamaha..."

...it is between we lose of our Nation or we have our Nation, we can't negotiate in that perspective...

"...Huwezi kuamua kwa maamuzi mepesi namna hii, we require time na research ya kutosha na ifanywe na Watanzania Madaktari ambao hawajapokea pesa..."

...Mnajiuliza tunalazimishia nini? Kama ni hela kiasi gani? Kwa ajili ya roho za watu?

...Ni nini hiki mnafanya?... Nataka mnijibu, na mimi nasema atakayenisemesha nitamsemesha mara mbili..."

3.3.29 **Mheshimiwa Spika**, Bunge linaongozwa kwa mujibu wa Katiba, Sheria na Kanuni ambapo kiongozi wake ni wewe Mhe. Spika. Kitendo cha Mheshimiwa Josephat Gwajima kutoa kauli zinazonesha kuwa hakuna wa kumzuia na kwamba wakati wowote atatoa kauli anazotaka kwa maneno kwamba nikisema imeshakuwa ni utovu wa nidhamu uliokithiri kwa nafasi yake kama Mbunge na kiongozi katika Taifa ambaye hupaswa kuongozwa na sheria na uongozi wake. Kanuni 85(l)(g) inaeleza:-

"(1) Mbunge atakuwa ametenda kosa la utovu wa nidhamu uliokithiri ikiwa-

(g) atakiuka Kanuni hizi kwa namna nyngine yoyote ambayo, kwa maoni ya Spika, ataona kuwa ni utovu wa nidhamu uliokithiri".

3.3.30 **Mheshimiwa Spika, Mhe Josephat Gwajima** alishindwa kuthibitisha kauli zake na wala hakuwa na kielelezo chochote cha kauli zake licha ya kuuaminisha umma kuwa anao ushahidi. Shahidi huyu alisema uongo kwa kuwaaminisha watu kwamba chanjo pekee ilioingizwa nchini ni Johnson Johnson na kuwa chanjo kutoka China haijaingizwa nchini. Kamati ilibaini kuwa chanjo zaidi ya Johnson Johnson zipo nchini ambapo chanjo toka China zimewasili Zanzibar. Vilevile suala la viongozi kulipewa rushwa hakutoa ushahidi wowote

3.3.31 **Mheshimiwa Spika**, kwa ushahidi huo Kamati imejiridhisha kuwa ni kweli alitoa kauli zinadhalilisha nafasi ya Mbunge, zinazoshusha heshima ya Bunge, Wabunge na viongozi. Vile vile zinazochonganisha Mhimili wa Bunge dhidi ya Mhimili wa Serikali, Serikali na Wananchi, Bunge na Wananchi pamoja na kudharau na kushusha heshima ya Bunge, Shughuli za Bunge na Uongozi wa Bunge.

3.3.32 **Mheshimiwa Spika**, vitendo hivyo vinakiuka kifungu cha 26 (d) na (e) cha sheria ya Kinga, Haki na Madaraka ya Bunge. Vilevile kauli hizo zinaonesha utovu wa nidhamu uliokithiri chini ya Kanuni ya 85(1)(g) ya Kanuni za Kudumu za Bunge.

3.3.33 **Mheshimiwa Spika, Kamati kwa kauli moja ilimtia hatiani Mhe. Josephat Gwajima** baada ya kutafakari kauli zilizotolewa, ushahidi mbele ya Kamati pamoja na vifungu vyta Sheria vinavyozuia vitendo alivyovifanya.

3.3.34 **Mheshimiwa Spika**, baada ya kujiridhisha kuwa shahidi alitenda kosa alilolalamikiwa, Kamati ilijielekeza katika kujibu hoja kuhusu hatua za kisheria zinazopaswa kuchukuliwa dhidi yake. Kamati ilizingatia masharti ya Kifungu cha 33(1) cha Sheria ya Kinga, Madaraka na Haki za Bunge, Sura ya 296 kinachotoa mamlaka kwa Bunge kuitia Azimio kutoa adhabu kwa Mbunge anayekutwa na hatia ya kukiuka masharti ya Kifungu cha 26 au kinginecho. Kifungu kinaeleza: *"33-(1) Where any Member commits any contempt of the Assembly whether specified in section 26 or otherwise, the Assembly may, by resolution, either direct the Speaker to reprimand such Member or suspend him from the service of the Assembly for such period as it may determine. Provided that, such period shall not extend beyond the last day of the session next following that which the resolution was passed or of the session in which the resolution is passed as the Assembly may so determine".*

3.3.35 **Mheshimiwa Spika**, kuhusu adhabu kwa kosa la utovu wa nidhamu uliokithiri, Kamati ilijielekeza katika Kanuni ya 85(3) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni 2020. Kanuni hii inaweka adhabu kwa Mbunge anayekiuka Kanuni hii kuwa ni **asihudhurie mikutano ya Bunge mfululizo isiyopungua miwili au isiyozidi mitatu**. Kanuni inaeleza: *"Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge itashughulikia shauri hilo na ikithibitika kuwa mbunge husika alitenda kosa inaweza kushauri kwamba Mbunge huyo asihudhurie mikutano mfululizo isiyopungua miwili au isiyozidi mitatu"*

Aidha, Kanuni ya 85(4) inaeleza kwamba Kamati inaweza kulipatia Bunge ushauri mwingine wowote kuhusu adhabu anayostahili kupewa Mbunge aliyejuki masharti ya Kanuni inayohusu utovu wa nidhamu uliokithiri.

4.0 UZOEFU WA KAMATI KATIKA KUSHUGHULIKIA MASHAURI YA NAMNA HII

Kamati imewahi kufanya uchunguzi wa mashauri mbalimbali kama ifuatavyo:

- i) Shauri la **Mhe. Saed Kubenea** ambaye alikuwa Mbunge katika Bunge la 11, alitoa kauli za kudharau Bunge akiwa Kanisani. Kamati ilichunguza na kutoa mapendekezo kuhusu hatua za kuchukua.
- ii) Shauri liliomhusu **Mhe. Freeman Mbowa** na linguine liliomhusu **Mhe. Halima Mdee** kwa nyakati tofauti katika Bunge la 11, Waheshimiwa Wabunge hao walitoa kauli za kudhalilisha Bunge wakiwa nje ya Vikao vya Bunge ambazo zilinukuliwa na vyombo vya habari na mitandao ya kijamii. Kamati iliwaitia hatiani kutokana na vitendo hivyo vya kudhalilisha na kudharau Bunge.
- iii) Shauri liliomhusu **Prof. Musa Assad** aliyekuwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. Kamati ilichunguza kauli zilizonukuliwa na vyombo mbalimbali vya habari zilizotoa shutuma na dharau kwa Bunge. Kamati ilimpata na hatia na kupendekeza hatua za kuchukuliwa.
- iv) Shauri liliomhusu **Ndg. Paul Makonda** na lingine liliomhusu **Ndg. Alexander Mnyeti**. Hawa walikuwa ni viongozi wa Serikali Mkuu wa Mkoa na Mkuu wa Wilaya kwa mtawalia ambao kauli zao zilinukuliwa na mitandoa ya jamii, ambazo zilionesha dharau na kudhalilisha Bunge, Kamati ilifanya uchunguzi na kumtia hatiani kisha kutoa mapendekezo.

5.0 VITENDO VYA SHAHIDI WAKATI WA USIKILIZAJI WA SHAURI LAKE

5.1 Mheshimiwa Spika, Kamati ilifanya tathmini ya mwenendo au tabia ambazo shahidi alizonesha mara alipofika kuhojiwa mbele ya Kamati. Kamati ilishangazwa na vitendo alivyofanya na hivyo imeona kuwa ni shahidi mjeuri ambaye alileta dharau kwa Kamati.

5.2 **Mheshimiwa Spika**, tarehe 23 Agosti, 2021 shahidi alifika mbele ya Kamati. Alipokaribishwa kuketi kwenye kiti cha shahidi alikikataa kwa kusema hawezি kukalia kiti hicho na akachukua kiti kingine, Kamati iliona sio shida ikamruhusu. Baada ya hapo, Kamati ilipomtaka azungumze, alikataa kutumia kipaza sauti iliyokuwepo na kudai ibadilishwe. Kamati pia iliona ikidhi matakwa ya moyo wake ikambadilishia.

5.3 **Mheshimiwa Spika**, kama hiyo haitoshi, tarehe 25 Agosti, 2021 shahidi alifika tena mbele ya Kamati. Alipoitwa kuendelea kutoa ushahidi aliiingia ndani ya ukumbi kama ilivyotakiwa. Alipoelekezwa kuketi alikataa, akidai anapenda kuzungumza akiwa amesimama. Hata katika hili, Kamati iliona imvumilie tu.

5.4 **Mheshimiwa Spika**, pamoja na vituko hivyo, katika ushahidi wake **Mhe. Josephat Gwajima** hakutoa ushirikiano wa kuridhisha kwa sababu kwa sehemu kubwa hakuwa akijibu maswali kama alivyoulizwa. Majibu yake kwa maswali hata yaliyokuwa ya kawaida aling'ang'ania kuelezea masuala ya imani yake na kusisitiza kuwa aliongea kama kiongozi wa kimataifa wa kanisa lake na hotuba zake zilisambaa Duniani kote na siyo Tanzania pekee. Zaidi ya hivyo, majibu yake yaliyikita kwamba Kamati haina mamlaka ya kuhoji mahubiri ya kanisani.

5.5 **Mheshimiwa Spika**, Kamati iliona kuwa shahidi hakuitendea haki Kamati kwa vitendo alivyovifanya. Kamati inaeleza hivyo kwa sababu shahidi anaelewa vema utaratibu unaozingatiwa na Kamati wakati wa kuendesha mashauri kwa kuzingatia kuwa, akiwa ni mjumbe wa Kamati, alikuwepo wakati Kamati inapata mafunzo kuhusu masuala ya uendeshaji wa mashauri kwenye Kamati.

6.0 Maoni na mapendekezo ya jumla ya Kamati kuhusu shauri hili

Mheshimiwa Spika, pamoja na kushughulikia suala la **Mhe. Josephat Gwajima** Kamati imebaini masuala mbalimbali ambayo yanapaswa kufanyiwa kazi ili kuhakikisha amani na

utulivu wa nchi unaendelea kudumishwa. Kutokana na kauli mbalimbali anazozitoa **Mhe. Josephat Gwajima**, Kamati inashauri yafuatayo:

- i) Vyombo vyta kisheria vifuutilie na kuchunguza mwenendo na vitendo vyta **Mhe. Josephat Mathias Gwajima** kwa kuwa vinaashiria uwepo wa jinai na uvunjifu wa amani na usalama wa nchi; na
- ii) Suala hili lishughulikiwe pia kwa mujibu wa sheria na maadili ya viongozi wa umma lifikishwe kwenye chama anachotoka ili aweze kuchukuliwa hatua kwa mujibu wa maadili ya chama chake.

Mheshimiwa Spika, huu ndio uchunguzi wa Kamati kuhusu shauri linalomkabili Mhe. Josephat Mathias Gwajima hivyo, tunaomba Bunge liutafakari na liuzingatie wakati wa kupitisha Azimio la kuchukua hatua dhidi ya **Mhe. Josephat Gwajima**.

6.0 HITIMISHO

6.1 **Mheshimiwa Spika**, mwisho, napenda kukushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi hii kuwasilisha maoni ya Kamati kwa niaba ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge na napenda nitumie nafasi hii tena kukupongeza kwa dhati kwa jinsi unavyoliongoza Bunge hili ambalo ni chombo cha uwakilishi wa Wananchi kuisimamia na kuishauri Serikali ili kuhakikisha kuwa ustawi wa wananchi unakuwa ndio kipaumbele cha kwanza.

6.2 **Mheshimiwa Spika**, kipekee, nawashukuru Wajumbe wote wa Kamati, kwa kazi nzuri ya kujadili na kuchambua kwa umakini mkubwa shauri hili kwani katika kutekeleza jukumu hili walizingatia misingi ya haki. Kwa heshima naomba niwatambue kwa majina kama ifuatavyo:-

1. Mhe. Stela Alex Ikupa, Mb. - M/Mwenyekiti
2. Mhe. Omari Mohamed Kigua, Mb.
3. Mhe. Japhet Ngailonga Hasunga, Mb.
4. Mhe. Tarimba Abbas Gulam, Mb.

5. Mhe. Joseph Anania Tadayo, Mb.
6. Mhe. Lemburis Saputu Mollel Noah, Mb.
7. Mhe. Deodatus Philip Mwanyika, Mb.
8. Mhe. Tunza Issa Malapo, Mb.
9. Mhe. Juma Hamad Omar, Mb.
10. Mhe. Margaret Simwanza Sitta, Mb.
11. Mhe. Mariamu Madalu Nyoka, Mb.
12. Mhe. Agnes Elias Hokororo, Mb.
13. Mhe. Ali Hassan Omar King, Mb.
14. Mhe. Othman Hija Juma, Mb.
15. Mhe. Bahati Kenneth Ndingo, Mb.
16. Mhe. Zahor Mohammed Haji, Mb.
17. Mhe. Shally Josepha Raymond, Mb.
18. Mhe. Dkt. Christine Gabriel Ishengoma, Mb.
19. Mhe. Naghenjwa Livingstone Kaboyoka, Mb.
20. Mhe. Ali Juma Mohamed, Mb.

6.3 **Mheshimiwa Spika**, Aidha, napenda kumshukuru kwa dhati Katibu wa Bunge, Ndg. Nenelwa Mwihambi, *ndc*, kwa kuisaidia Kamati kutekeleza majukumu yake ipasavyo. Kipekee, nawashukuru Ndugu Pius T. Mboya, Mkurugenzi wa Idara ya Huduma za Sheria, Ndg. Leocardo Kapongwa Mkurugenzi Msaidizi wa Idara ya Huduma za Sheria, kwa ushauri wa Kisheria waliloutoa katika kuisaidia Kamati. Aidha napenda kuwashukuru Ndg. Maria Mdulugu, Ndg. Rehema Kipera na Ndg. Thomas Shawa Makatibu wa Kamati, Ndg. Kelvin Kiwango Sekretarieti upande wa *Hansard*pamoja Ndg. Imelda Ntimba msaidizi wa Kamati kwa kuratibu vyema kazi za Kamati na kuhakikisha kuwa Taarifa hii inakamilika mapema.

6.4 **Mheshimiwa Spika**, mwisho kabisa ni matarajio yangu kuwa Waheshimiwa Wabunge wataipokea na kwa kauli moja wataikubali hoja iliyopo mbele ya Bunge kuhusu matokeo ya Taarifa ya Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge ya uchunguzi kuhusu kauli za **Mhe. Josephat Gwajima**.

Mheshimiwa Spika, wajumbe wote tunalo jukumu la kuimarisha nidhamu ya Bunge letu Tukufu na kuhakikisha kuwa sisi wabunge wote tunatekeleza vema wajibu wetu kwa

Wananchi kwa kuheshimu na kuzingatia Sheria za nchi, Kanuni na taratibu zinazohusu maadili ya Wabunge.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

Mhe. Emmanuel Adamson Mwakasaka, Mb.

MWENYEKITI

KAMATI YA HAKI, MAADILI NA MADARAKA YA BUNGE

30 Agosti, 2021

SPIKA: Hoja imetolewa na imeungwa mkono, Mwenyekiti endelea na utaratibu kama unasaidiwa au unaendelea mwenyewe haya. Mtatuongoza.

MHE. EMMANUEL A. MWAKASAKA – MWENYEKITI WA KAMATI YA BUNGE YA HAKI, MAADILI NA MADARAKA YA BUNGE: Mheshimiwa Spika, hii ni Taarifa ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge kuhusu uchunguzi wa tuhuma kuvunja haki za Bunge na kusema uwongo zinazomkibili Mheshimiwa Jerry William Silaa.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 4, 2 na 3 ya Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge lako Tukufu, Taarifa ya Kamati kuhusu uchunguzi wa tuhuma zinazomhusu Mheshimiwa Jerry William Silaa, Mbunge, kuhusu kuvunja haki za Bunge na kusema uwongo.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote napenda kukushukuru wewe binafsi kwa weledi, busara na hekima katika kuliongoza Bunge letu kwa ufanisi mkubwa. Aidha, napenda kumshukuru Mheshimiwa Naibu Spika na Wenyeviti wote wa Bunge letu kwa namna wanavyokusaidia kutekeleza majukumu yako.

Mheshimiwa Spika, mnamo tarehe 20 Aosti na tarehe 21 Agosti kwa mamlaka uliyonayo chini ya Kanuni ya 4(1)a ya Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Juni 2020 uliagiza Kamati yangu kukutana kwa ajili ya

kuchunguza tuhuma zinazomkabili Mheshimiwa Jerry William Silaa na kutoa mapendekezo kuhusu hatua za kuchukuliwa. Kufuatia agizo lako, Kamati ilikutana rasmi tarehe 24 Agosti 2021, tarehe 26, tarehe 27 na tarehe 30 Agosti 2021 kwa ajili ya kushughulikia suala hilo.

Mheshimiwa Spika, chimbuko la shauri hili lilitokana na kauli zilizosambaa kwenye vyombo vya habari na mitandao ya kijamii mnamo tarehe 23 Julai, 2021 ikimnukuu Mheshimiwa Jerry William Silaa (Mb). Mheshimiwa huyu alinukuliwa wakati anazungumza na wananchi katika Jimbo la Ukonga, Jijini Dar es Salaam, kuwa mishahara ya Wabunge haikatwi kodi. Kauli zake zilikuwa na maneno yafuatayo, naomba kumnuuu:-

(a) *"Mimi nimeanza Ubunge juzi, mwaka jana mwezi wa kumi na moja. Kwa hiyo nimekuta hayo yanayosemwa mengine yameshaptishwa tayari Bungeni. Na katika hili mimi niungane na Mheshimiwa wa Kinondoni, Mheshimiwa Abbas Tarimba, kwamba vikiliwa vya mwali na vya kungwi viliwe!"*

(b) *"Ni wakati muafaka kwa sisi Waheshimiwa Wabunge, ili tupate moral integrity, ili tupate uwezo wa kusimama mbele za watu kuwaambia walipe kodi na sisi tuanze kulipa kodi kwenye mishahara yetu. Hakuna sababu ya kuwa na wengine wanaolipa na wengine hawalipi. ukishakuwa hulipi unakosa ile nguvu ya kumwambia mwenzako aliipe"*

Mheshimiwa Spika, mwisho wa kumnuuu.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusoma hati ya wito Kamati ilianza kwa kujadili kauli zinazolalamikiwa katika shauri hilo. Mheshimiwa Abbas Tarimba (Mb) ambaye ni mijumbe wa Kamati hii alieleza Kamati kwamba, jina lake limetajwa katika kauli inayofanyiwa uchunguzi na Kamati. Japokuwa alikana kuhusika na maelezo yaliyokuwa katika *twitter* ambayo Mheshimiwa Jerry Silaa (Mb) alimnukuu kwamba yeche, Mheshimiwa Abbas Tarimba, aliyasema aliiomba Kamati, kwamba misingi ya utendaji wa haki inamtaka ajitoe

katika kusikiliza shauri hilo ili kuepuka kuonekana anaegemea upande wowote. Kamati iliona hoja ya Mheshimiwa Abbas Tarimba ni ya msingi, hivyo Kamati iliridhia kujitoa kwake. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, Mbunge anayewakilisha Bunge kwenye chombo kingine cha uwakilishi au Mjumbe wa Bunge la Afrika Mashariki alieleza kuwa tuhuma hizo iwapo zitathibitika ni ukiukaji wa Kifungu cha 26(d) na (e) cha Sheria ya Kinga, Haki na Madaraka ya Bunge na Kanuni ya 85(1)(g) ya Kanuni za Kudumu za Bunge zinazokataza mtu ye yote kufanya vitendo alivyotuhumiwanavyo.

Mheshimiwa Spika, Uchambuzi wa Shauri. Bunge limepewa mamlaka kisheria ya kusikiliza na kutoa hukumu kwa makosa yanayovunja Haki za Bunge ambayo si jinai chini ya sheria hii. Mamlaka hayo yapo chini ya Kifungu cha 13 cha Sheria ya Kinga, Madaraka na Haki za Bunge, Sura ya 296.

Mheshimiwa Spika, kwa utekelezaji bora wa mamlaka hayo, Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge iliundwa na kupewa jukumu hilo chini ya Kanuni ya 4(1) (a), (b) na (c) ya Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni 2020.

Mheshimiwa Spika, ushahidi mwingine uliofanyiwa kazi na Kamati hii ni wa Mheshimiwa Jerry Silaa alioutoa mbele ya Kamati siku ya tarehe 24 Agosti, 2021. Wakati wa mahojiano, Mheshimiwa Jerry Silaa alikiri kuwa yeye ndiye aliyetoe kauli zinazolalamikiwa. Shahidi huyu alifafanua kuwa alitoa kauli hizo alipokuwa anahutubia wananchi wa Jimbo la Ukonga, Jijini Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, maelezo ya shahidi yalikuwa kama ifuatavyo; na ninanukuu:-

"Mheshimiwa Mwenyekiti kwa ujumla ninakiri yapo sahihi, isipokuwa kwenye paragraph ya kwanza, kama Kamati yako itaridhia, mkutano wa wananchi ulifanyika

tarehe 22 na siyo 23; mengine yote ni sawa” Mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Spika, kutokana na ushahidi wa kukiri mbele ya Kamati pamoja na ushahidi wa video iliyosambaa katika mitandao mbalimbali ya kijamii na vyombo vyaa habari kuanzia tarehe 23 Julai, 2021 Kamati imejiridhisha kuwa kweli Mheshimiwa Jerry Silaa ndiye aliyetoa kauli zinazolalamikiwa.

Mheshimiwa Spika, katika kupata majibu ya hoja hii, Kamati ilimhoji Mheshimiwa Jerry Silaa ili kupata maelezo ya kuthibitisha ukweli kuhusu kauli yake ya kwamba mishahara ya Wabunge haikatwi kodi. Kwa kuanzia Kamati ilitaka maelezo yake iwapo anazifahamu stahili zake kama Mbunge na iwapo anaufahamu mshahara wa Mbunge.

Mheshimiwa Spika, shahidi alieleza Kamati kwamba, baada ya kupata Ubunge alipewa maelezo ya stahili za Mbunge na hivyo anafahamu vizuri sana mshahara wa Mbunge. Swali lingine aliloulizwa ni iwapo mshahara wake unakatwa kodi. Wakati wa kujibu Shahidi aliomba kwamba ikae kwenye kumbukumbu za Kamati, kwamba katika mshahara anaopokea kuna kiasi kinakatwa kodi na kuna kiasi hakikatwi kodi. Alipoulizwa kuhusu kufafanua ni kiasi kipi kinakatwa kodi na kiasi kipi hakikatwi kodi, alieleza kuwa katika mshahara wa Mbunge eneo la *basic salary* linakatwa kodi (*P.A. Y.E*).

Mheshimiwa Spika, sehemu ya maelezo yake ni kama yafuatayo; naomba kumnuuu:

“Ukiondoa basic salary ambayo ndiyo inatengeneza sehemu ya mshahara wa Mbunge kuna posho inaitwa Bunge Allowance ambayo inajumuisha vitu mbalimbali. Katika vitu vile vinavyojumuishwa ni pamoja na posho ya mafuta, posho ya matengenezo ya gari, OC ya Jimbo, mishahara ya wasaidizi wa Jimbo na posho za ziara siku kwa 10 jimboni ambazo ni za kujikimu, ambazo kwenye Sheria ya Kodi zinafahamika kama personal allowances. Hizo hazilipiwi kodi.”

Mheshimiwa Spika, naendelea kumnukuu shahidi:-

"Nirudie pale awali kwenye mkanganyiko baina ya basic salary, mshahara na personal income. Narudia suala langu la awali, na ikae kwenye kumbukumbu, kwamba nimeelezea kwamba, personal income ndio mshahara. Muundo wa basic salary na posho mbalimbali National Service Compass."

Mheshimiwa Spika, mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Spika, katika kuelewa vema jambo hili, Kamati ilijielekeza kwenye ushahidi uliotolewa na Ndugu Layson Mwanjisi. Shahidi huyu ni mtaalam anayesimamia malipo ya stahili mbalimbali za Wabunge ikiwemo posho na mishahara. Shahidi huyu alieleza Kamati kuwa yeye ni Mhasibu Mkuu katika Sekretarieti ya Bunge na amefanya kazi hiyo katika Sekretarieti ya Bunge kuanzia mwaka 2015. Shahidi alifafanua kuwa kwa kipindi chote alichohudumu katika ofisi hiyo mishahara ya Wabunge inakatwa kodi. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, aidha, Ndugu Layson Mwanjisi alipohojiwa alitofautisha malipo ya mishahara na malipo ya posho wanayolipwa Wabunge. Shahidi alieleza kwamba, posho zinazolipwa kwa Wabunge hazikatwi kodi kwasababu Wabunge wanalipwa posho kwa ajili ya kuwawezesha kufanya kazi za Kibunge na kuendesha shughuli za ofisi zao katika majimbo yao. Alifafanua zaidi kuwa utaratibu wa kutokata kodi katika posho ndio unaotumika Serikalini kote. Vile vile alidokeza kwamba, kati ya mwaka 2017–2018 alikaguliwa na maafisa kutoka *TRA* waliotaka kujihakikishia iwapo Wabunge wanatakiwa kukatwa kodi katika stahili zao zaidi ya wanavyokatwa katika mishahara yao. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, Shahidi huyu alieleza kuwa wakaguzi hao walizingatia sheria, nyaraka na vielelezo walivyopatiwa na kisha timu hiyo ilijiridhisha kuwa Wabunge hawapaswi kukatwa kodi katika posho zao isipokuwa mishahara pekee. Ndugu Layson Mwanjisi alipoulizwa iwapo Mheshimiwa Jerry William Silaa anakatwa kodi katika stahili

zake, alijibu kuwa Mheshimiwa Jerry Silaa anakatwa kodi katika mshahara wake. Vilevile Shahidi huyu alieleza Kamati kuwa posho anazolipwa Mheshimiwa Jerry Silaa hazikatwi kodi. Katika kuthibitisha hilo, aliipatia Kamati hati ya mshahara (*salary slip*) ili kuithibitishia Kamati juu ya maelezo aliyojatoa. Hati hiyo ilipokelewa kama kielelezo A.

Mheshimiwa Spika, baada ya Kamati kuchambua ushahidi wa Mheshimiwa Jerry Silaa na ushahidi wa Ndugu Layson Mwanjisi, Kamati ilijielekeza katika Sheria ya Usimamizi wa Bunge, Sura ya 115. Sheria hiyo inaweka masharti kuhusu malipo ya mishahara na posho kwa Wabunge. Kifungu cha 20 kinaeleza wazi kuwa mshahara wa Mbunge ndio utakatwa kodi. Kifungu kinaeleza kama ifuatavyo:-

20, -(1) A Member of Parliament shall be entitled to such salary as the President may, by order published in the Gazette, determine.

(2) There shall be paid to a Member of Parliament the following allowances at such rates as the President may in writing determine.

(3) The allowances given under this section shall be exempt from income tax.

Mheshimiwa Spika, katika kuthibitisha hilo, wakati wa mahojiano Mheshimiwa Jerry Silaa alikiri kuwa kauli zake zimeleta tafrani kwenye jamii.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa ushahidi wa sheria katika shauri hili unathibitisha kwamba Mheshimiwa Jerry Silaa alikuwa na nia ovu ya kulidharau na kulidhalilisha Bunge pamoja na kuchonganisha Wabunge, Serikali, uongozi wa Bunge na wananchi kwa kusema uongo.

Mhesimiwa Spika, Kamati inaona kuwa Mheshimiwa Jerry Silaa amekiuka Kifungu cha 26(c), (d) na (e) cha Sheria ya Kinga, Madaraka na Haki za Bunge, Sura ya 296. Masharti ya kifungu hiki yanakataza mtu yejote kufanya kwa makusudi

kitendo chochote chenye kudharau shughuli za Bunge au mtu yejote anayeendesha shughuli hizo.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilimtia hatiani Mheshimiwa Jerry Silaa kwa kusema uongo. Hatua hiyo ni baada ya kuzingatia ushahidi uliokuwepo mbele ya Kamati pamoja na sheria zinazosimamia mishahara ya Wabunge.

Kamati iliona kuwa jambo hilo ni dharau kwa Bunge, Spika na shughuli za Bunge; vilevile kwa kuchonganisha Wabunge, Serikali, Uongozi na Wananchi. Kosa hilo ni kinyume na Kifungu cha 26(c), (d) na (e) cha Sheria ya Kinga, Madaraka na Haki za Bunge, Sura ya 296.

Mheshimiwa Spika, aidha, Kanuni ya 85(1)(g) ya Kanuni za Kudumu za Bunge inaeleza kuhusu utovu wa nidhamu uliokithiri kuwa ni pamoja na makosa ambayo kwa maoni ya Spika ni utovu wa nidhamu uliokithiri. Kutokana na kitendo cha Mheshimiwa Jerry Silaa cha kutokusahihisha kauli yake alioitoa kwenye mukitano wa hadhara licha ya kutakiwa na Mheshimiwa Spika kuomba radhi hadharani ambapo maelekezo ya Spika yalikuwa aombe radhi kupitia vyombo vya habari na mitandoa ya kijamii alioitumia kusema uongo; na kwamba kwa kuwa Mheshimiwa Jerry Silaa alikiri kuwa alipata maelekezo yako ya kumtaka aombe radhi kwa upotoshaji alioufanya kupitia vyombo vya habari; lakini pamoja na maelekezo hayo Mheshimiwa Jerry Silaa alikaidi maelekezo yako; na hivyo basi katika suala hili, Kamati imejiridhisha kuwa kitendo alichokifanya ni utovu wa nidhamu uliokithiri.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilitafakari hoja kwamba, je, ni hatua gani za kisheria zinazopaswa kuchukuliwa dhidi ya Mheshimiwa Jerry Silaa?

Mheshimiwa Spika, katika kujibu hoja hii, Kamati ilizingatia sheria na kanuni zinazotawala masuala ya Bunge na kutafakari kwa kina kuhusu ushahidi wa Mheshimiwa Jerry Silaa mbele ya Kamati.

Mheshimiwa Spika, kuhusu adhabu kwa kosa la utovu wa nidhamu uliokithiri, Kamati ilijielekeza katika Kanuni ya 85(3) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni 2020. Kanuni hii inaweka adhabu kwa Mbunge anayekiuka Kanuni hii kuwa ni asihudhurie mikutano ya Bunge mfululizo isiyopungua miwili au isiyozidi mitatu.

Mheshimiwa Spika, Mwenendo wa Shahidi Wakati wa Usikilizaji wa Shauri. Kamati ilipata wasaa wa kufanya tathmini ya mwenendo wa Shahidi alipofika mbele ya Kamati, vitendo vya Shahidi wakati wa usikilizaji wa shauri hili pamoja na ushirikiano wa Shahidi mbele ya Kamati; hivyo vyote vimeisaidia katika kuandaa taarifa.

Mheshimiwa Spika, Shahidi aliitikia wito wa kufika mbele ya Kamati tarehe 24 Agosti, 2021 kwaajili ya kuhojiwa. Wakati wa mahojiano shahidi hakuwa tayari kujibu maswali kikamilifu, jambo ambalo liliifanya Kamati kutumia muda mrefu kupata majibu ya masuala ambayo majibu yake yalikuwa wazi. Kwa ufupi Shahidi hakutoa ushirikiano kwa Kamati kwa kutojibu kikamilifu maswali alioulizwa.

Mheshimiwa Spika, kabla ya mahojiano kuanza Shahidi alikumbushwa kuhusu utaratibu wa kisheria wa usikilizaji wa mashauri ya Kamati hii kwa faragha. Pamoja na kuwa na taarifa hizi, Shahidi alikuwa anachukua kumbukumbu za shauri kwa kuandika katika shajara yake (*diary*). Kamati ilimtaka aache shajara hadi shauri litakapohitimishwa. Shahidi alikataa kuiacha shajara hiyo na badala yake alisema atachana kurasa alizoandika. Baada ya maelezo hayo alichana na kukabidhi kwa sekretarieti.

Mheshimiwa Spika, lakini Shahidi ameandika uongo katika barua yake kwa Katibu wa Bunge kwa kusingizia kwamba Kamati ndio iliyochana shajara yake, na kwamba, kwasababu hiyo hakuweza kuikumbuka tarehe aliyoomriwa kurudi mbele ya Kamati.

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila
kufuata utaratibu)*

Mheshimiwa Spika, baada ya mahojiano Kamati iliahirisha usikilizaji wa shauri hilo na kumtaka Shahidi arudi mbele ya Kamati siku ya tarehe 26 Agosti ili kuendelea na mahojiano. Tarehe 25, Shahidi aliwasilisha kwa Katibu wa Bunge barua ya tarehe 24 Agosti, 2021, ambapo alimtaka Katibu wa Bunge aififikishe kwenye Kamati. Barua hiyo ilikuwa na malalamiko kwamba wakati wa kusikiliza shauri lake Kamati hajamtenda haki, haikumsikiliza, ilikuwa batili, ilikuwa kinyume cha sheria, ilikuwa na upendeleo na Kamati hiyo ilikosa weledi wa kusikiliza shauri lake. Sehemu ya maelezo yake katika barua hiyo ni kama ifuatavyo; naomba kunukuu sehemu ya barua yake:-

"Kamati imejijendesha unconstitutionally, impartial, biased, unlawful, unprofessional na kwa kifupi sijapata haki yangu kama Shahidi. Kamati imekataa kupokea ushahidi wangu, nimekataliwa kusema, nimewekewa maneno mdomoni, nimenyimwa haki za msingi ikiwemo freedom of speech."

Mheshimiwa Spika, mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Spika, halikadhalika barua yake ilikuwa na maneno mengine yafuatayo:-

1. *"Nawasilisha ushahidi wangu wa maandishi nakukutaka kutumia mamlaka yako kuyafikisha kwa Mwenyekiti na kumshauri athari za kisheria za vitendo walivyofanya leo."*

Mheshimiwa Spika, naendelea kunukuu:-

2. *"Nimehesabu leo sijasikilizwa na Kamati na aidha Kamati ichukue mchango wangu wa maandishi na yenye we iniandikie kwa maandishi hoja zao na shauri hili liendeshwe kwa utaratibu wa maandishi."*

3. *"Nimejulishwa kufika mbele ya Kamati, sitafika kwani sina wito rasmi na sehemu nilipoandika tarehe na saa wamechana diary yangu na kubaki nayo kwa kisingizio cha siri."*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine katika barua yake ni kuwa alihoji kwa nini Kamati ilimdadisi iwapo anajiona anafaa kwenye nafasi aliyochanguliwa na Bunge kuliwakilisha Bunge katika Bunge la *PAP*. Shahidi huyu amelalamika kwamba, hata Spika aliongelea suala la uwakilishi wake siku ya tarehe 17 Agosti, wakati wa semina ya Wabunge wote akiwa hayupo.

Shahidi alieleza kwamba, atashangaa iwapo kutakuwa na mtu anayeona ujumbe wake wa *PAP*ni hisani. Alisitsiza kuwa, ujumbe wake ni kwa mujibu wa masharti ya Kanuni za Bunge. Aidha, alieleza kuwa uvumilivu wake umefika mwisho, hivyo, atashitaki kwenye Mahakama ya Umma; namnukuu:-

"Katika mahojiano wajumbe waliniuliza juu ya ujumbe wangu wa Bunge la Afrika. Sikuwepo siku ya Jumanne tarehe 17 Agosti, wakati Mheshimiwa Spika anazungumza kwenye semina ya Wabunge, na hivyo nachelewa sana kusema naye alisema kuhusu ujumbe wangu wa PAP. Nitashangaa sana kama kuna mtu anaona ujumbe wangu wa PAP ni hisani na hautokani na Kanuni za Kudumu za Bunge, Kanuni ya 14 ya nyongeza ya pili."

Mheshimiwa Spika, mwisho wa kumnukuu.

Mheshimiwa Spika, Kamati iliona kuwa amesema uongo kwenye Kamati ya Maadili. Kwa tabia hiyo, Kamati iliamini kuwa, ni wazi kuwa atawezekana kusema uongo katika Bunge la *PAP*.

Mheshimiwa Spika, Kanuni za Kudumu za Bunge, Kanuni ya 4 (1)(c), inayotoa mamlaka kwa Kamati ya Maadili kushughulikia shauri linalomhusu Mbunge anayewakilisha Bunge kwenye chombo kingine cha uwakilishi au mjambe wa Bunge la Afrika Mashariki; Kanuni inaeleza, naomba kuinukuu:

SPIKA: Kwa maslahi ya muda, Mwenyekiti nenda kwenye Maazimio.

MHE. EMMANUEL A. MWAKASAKA – MWENYEKITI WA KAMATI YA BUNGE YA HAKI, MAADILI NA MADARAKA YA BUNGE: Mheshimiwa Spika, ahsante.

Mheshimiwa Spika, Azimio la Bunge kuhusu hatua za kuchukua dhidi ya Mheshimiwa Jerry William Silaa, Mbunge, kwa Kutoa Kauli za Uongo. Limetolewa chini ya Kifungu cha 33(1) cha Sheria ya Kinga, Madaraka na Haki za Bunge.

KWA KUWA Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania linaongozwa kwa mujibu wa Katiba, Sheria na Kanuni za Kudumu za Bunge ambazo zilitungwa na Bunge lenyewe kwa ajili ya kuliongoza katika kutekeleza shughuli zake;

NA KWA KUWA mnamo tarehe 23 Julai, 2021, Mheshimiwa Jerry William Silaa alinukuliwa na vyombo mbalimbali vya habari ikiwemo mitandao ya kijamii wakati anazungumza na wananchi wa Jimbo la Ukonga Jijini Dar es Salaam alipotoa kauli kwamba mishahara ya Wabunge haikatwi kodi;

NA KWA KUWA kauli za Mheshimiwa Jerry Silaa zilikuwa za uongo ambazo zimeupotosha umma, zimeshusha hadhi na heshima ya Bunge, zimedharaulisha mamlaka ya Bunge na kuchonganisha Serikali na wananchi na vilevile Bunge na wananchi;

NA KWA KUWA tarehe 20 Agosti 2021 Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Job Ndugai kwa mamlaka aliyopewa chini ya Kanuni ya 4(1)(a) ya Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge aliagiza Kamati ya Maadili na Madaraka ya Bunge ikutane na kufanya uchunguzi kuhusu kauli zilizotolewa na Mheshimiwa Jerry William Silaa ambazo zilinukuliwa na vyombo vya habari;

NA KWA KUWA kufuatia maelekezo ya Mheshimiwa Spika, Kamati ya Haki na Maadili na Madaraka ya Bunge ilikutana kuanzia tarehe 23 Agosti hadi tarehe 27 Agosti, 2021

na tarehe 30 Agosti, 2021 Dodoma na kufanya uchunguzi wa shauri la Mheshimiwa Jerry William Silaa;

NA KWA KUWA mnamo tarehe 24 Agosti, Mheshimiwa Jerry William Silaa alifika mbele ya Kamati na kuhojiwa kuhusu kauli zake na kuwa Kamati ilahirisha kusikiliza shauri lake hadi tarehe 26 Agosti, 2021;

NA KWA KUWA Mheshimiwa Jerry William Silaa hakufika siku ya tarehe 26 Agosti, 2021 ambayo Kamati ilipanga kuendelea kusikiliza shauri lake lakini kwa makusudi Mheshimiwa Jerry William Silaa alikaidi wito wa Kamati hivyo kudharau amri halali ya Kamati jambo liliofanya Kamati kuomba kwa Mheshimiwa Spika kutumia madaraka yake kuidhinisha Hati ya Kumkamata;

NA KWA KUWA baada ya kukaidi amri halali iliyomtaka kufika mbele ya Kamati tarehe 26 Mheshimiwa Jerry Silaa alifika tarehe 27 Agosti, 2021;

NA KWA KUWA Mheshimiwa Jerry William aliandika barua kwa Katibu wa Bunge na kinyume na taratibu kumtaka afikishe kwenye Kamati na kwamba barua hiyo ilikuwa inaikashifu Kamati na kutoa maelezo ya uwongo yenye maudhui yananyopotosha na kudhalilisha Kamati;

NA KWA KUWA wakati Kamati inamsikiliza ilijiridhisha kuwa katika ushahidi wake Mheshimiwa Jerry William Silaa hakuomba radhi wala hakujutia makosa aliyoyafanya ya kutoa kauli za uongo jambo ambalo ni dharau kwa Bunge, Spika na shughuli za Bunge na vilevile kuchonganisha Wabunge, Serikali Uongozi wa Bunge na wananchi;

NA KWA KUWA, kauli za Mhe. Jerry William Silaa zinakiuka kifungu cha 26(b)(d) na (e) cha Sheria ya Kinga, Haki na Madaraka ya Bunge, Sura ya 296 na Kanuni ya 18(1) (b),(4) (b) na 85(1)(g) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020;

NA KWA KUWA Mheshimiwa Jerry William Silaa amekuwa na mwenendo usiofaa na unaodhalilisha hadhi ya nafasi ya Mbunge kwa kusema uongo;

NA KWA KUWA Mheshimiwa Jerry William Silaa (Mb) akiwa mbele ya Kamati hakukiri wala kujutia makossa yake, alionyesha dharau, kudhalilisha nafasi ya Mbunge na kushusha heshima ya Bunge, kushusha hadhi ya Wabunge na viongozi, kuchonganisha Bunge na wananchi, Serikali na wananchi kwa kusema uongo, hivyo Kamati imemtia hatiani;

NA KWA KUWA Kanuni ya 61(1) (2) na (3) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la 2020 inalipa Bunge Mamlaka ya kupokea na kujadili mapendekezo ya Kamati hii na kisha kufanya uamuzi kwa njia ya Azimio la Bunge;

HIVYO BASI, Bunge linaazimia kuwa Mheshimiwa Jerry William Silaa:

(a) Asimamishwe kuhudhuria Mikutano ya Bunge Miwili mfululizo; na

(b) Aondolewe kwenye nafasi ya Uwakilishi wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika Bunge la Afrika (PAP). (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. (*Makof*)

MHE. OMARI M. KIGUA: Mheshimiwa Spika, naafiki.

SPIKA: Hoja imetolewa na imeungwa mkono, tunakushukuru sana Mwenyekiti, sasa unaweza ukarudi kwenye kitit chako ili usikilize michango ya Waheshimiwa Wabunge.

Kwanza, niwashukuru sana wajumbe wa Kamati hii ya Maadili kwa kazi kubwa ambayo wameifanya, wiki nzima hii wamekuwa wakihangaika na mambo haya mawili na hata jana sijui wamemaliza usiku saa ngapi naona hata Mwenyekiti anavyosoma usingizi na hata macho hayako

sawa kwa sababu amekesha kwa ajili ya mambo haya. Kwa hiyo, tunashukuru sana kwa kazi kubwa ambayo mmeifanya na poleni sana kwa yote. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti wa Maadili, naomba ukae hapa maana wewe ni mtoha hoja ili usikilize Waheshimiwa Wabunge wanachosema.

Waheshimiwa Wabunge wote wawili wanaojadiliwa hapa tulivateua pale mwanzo nao ni sehemu ya Kamati ya Maadili tulidhani kwamba uzoefu wao unaweza ukatusaidia. Kwa hiyo, hata wajumbe wanaoleta taarifa hii wamewajadili wajumbe wenzao yaani hawa ni wenzao. Hebu fikiria wewe ni mjumbe wa Kamati halafu wenzako wanakuona hivi, kwa hiyo, anayeona tofauti kwa kweli huyo naye ana matatizo. Sasa tumewasimamisha kwenye Kamati ya Maadili kwa sababu hawangeweza kujadili kesi inayowahusu wao wenywewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti tu hukutuambia tuliona mabegi na vitabu vingi sijui vilisaidia kiasi gani? Sasa hukutuambia labda wajumbe watatuambia huko mbele. (*Kicheko*)

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na uchangiaji, namwomba Mheshimiwa Omari Mohamed Kigua atufungulie na Mheshimiwa Shally Josepha Raymond atafuata. Tukichangia kwa dakika zisizozidi saba siyo mbaya kwa kila mmoja kwa sababu walioomba kuchangia ni wengi kidogo. Italia kengele moja tu baada ya dakika saba.

MHE. OMARI M. KIGUA: Mheshimiwa Spika, nikushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuwa mchangiaji wa mwanzo kabisa kwenye suala la Waheshimiwa au mashahidi kwenye jambo ambalo liko mbele yetu hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ni mjumbe wa Kamati hii kwa muda mrefu kidogo. Kwa uhakika naweza kusema kwa uzoefu mdogo ambao nilikuwa nao katika Kamati hii nimeshudia vituko vya ajabu kabisa kabisa.

Mheshimiwa Spika, Kamati yako inafanya kazi kwa mujibu wa taratibu na kanuni ambazo tumezitunga sisi wenyewe Wabunge na tunategemea kabisa wewe kama Mbunge umeaminiwa na wananchi na siyo Mbunge tu wa Jimbo ni Mbunge wa Tanzania nzima. Mwenendo wako, kauli zako, tabia zako lazima zifanane na nafasi uliyopewa. Kwa hiyo, siku zote unapozungumza lazima utafakari wewe ni nani? Unazungumza na akina nani? Hayo ndiyo yatakayokusaidia kuепuka haya ambayo leo tunayazungumza mbele ya Bunge lako Tukufu. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, nikianza na shahidi namba moja, ndugu yetu Mheshimiwa Josephat Gwajima, mimi namuita ni shahidi kwa mujibu wa taratibu tulizojiwekea. Hakika hakuitendea haki hata mara moja Kamati hii, hakuwa na nidhamu, hakuwa na heshima hata mara moja, hata ujio wake mbele ya Kamati ilikuwa inaonyesha dhahiri kabisa kwamba alikuja kwa kejeli na dharau iliyopitiliza. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, nitoe mfano mmoja tu, tulipomuuliza ni wapi unapotenganisha shughuli za Kanisa na shughuli za Ubunge hakuweza kutoa jibu la moja kwa moja, hakuwa na jibu. Aliiambia Kamati kwamba anazungumza na waumini wake kwenye Makanisa zaidi ya 140 duniani. Tulipomuuliza ni wapi unaweza ukabana taarifa zako kwamba hizi ziwfikie waumini wako na wananchi duniani kwa ujumla hakuweza kutoa majibu hayo. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, suala la kusema kwamba wapo watumishi wamepewa pesa, alipoulizwa hakutoa majibu. Pia tulijuliza heshima ya chombo hiki na heshima ya mihimili mingine inalindwa na wewe, tulipomuuliza hilo hakujibu hata mara moja.

Mheshimiwa Spika, lakini tupime athari ya kauli zake toka ameanza, mimi niungane na ushauri wa Kamati hii kwamba ukiacha Maazimio leo ambayo mimi naunga mkono vyombo vingine viende vikatazame athari ya kauli zake ni nini. Nani asiyejua hapa kwamba wananchi wa Tanzania wanakufa kwa *Corona* na ni kiongozi gani wa Serikali

amesema kwamba kuchanja ni lazima lakini yeye kauli zake zinathibitisha na zinaonyesha kwamba viongozi wetu wa Serikali wamelazimisha wananchi wachanjwe. Hili jambo kwa kweli halina afya kwa maendeleo ya nchi yetu na lazima tusimame imara tulinde chombo hiki. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, suala la ndugu yetu Mheshimiwa Jerry Silaa mimi na Waheshimiwa wenzangu wajumbe wa Kamati hii tulijiuliza huyu ni Mbunge mgeni kweli, lakini huyu ameshika nafasi kadhaa katika nchi yetu katika nafasi ya kuwa Meya wa Jiji la Dar es Salaam. Pia ulimpa nafasi aombe au arekebishe maneno yake hakufanya hivyo, hii ni dharau kwa Bunge na ni dharau kubwa kwako wewe Spika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini alipofika mbele ya Kamati kwa kuonyesha kwamba alidhamiria alichodhamiria na alisimamia kwa kile alichokuwa amekizungumza alikuja na ushahidi wa vitabu zaidi ya kumi, hakuwa na dhamira ya kuomba radhi.

Mheshimiwa Spika, wewe ni shahidi zimekwishaletwa kesi nydingi tu na kwa sababu Kamati hii ni ya kwako ulisamehe watu wengi hata Kamati imesamehe watu wengi lakini kwa jinsi alivyokuja mbele ya Kamati alikuja na msimamo kwamba alichokizungumza ni sahihi. Jambo hili siyo sahihi hata kidogo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini nikumbushe hakutii wito wa Kamati kwa sababu hata katika taratibu za kawaida unapokuwa una kesi ukipewa *summons* ya kwanza hupewi *summons* nydingine hakufika mbele ya Kamati. Kibaya zaidi alipoona kuna wito wa kukamatwa na Polisi aliamua kufika saa 12 asubuhi ndani ya ukumbi wa Kamati kinyume cha utaratibu wa kuendesha shughuli zetu pale. Pia huo ni uvunjifu na ukosefu wa adabu wa Mheshimiwa Silaa. (*Makofi/ Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, tunapochaguliwa tuna taratibu tunapewa mafunzo na watumishi wetu, hata kwenye *iPad* kuna mada zipo hapa za kuonyesha stahili zetu, Kamati

ilimuuliza Shahidi Mheshimiwa Jerry Silaa, je, unajua kwamba *allowance* hizi hazikatwi kodi? Anasema hajui. Aliposomewa akakiri kwamba leo ndiyo amefahamu kwamba *allowance* hazikatwi kodi. Sasa leo unawezaje kumuamini na kumpa nafasi hiyo kuwa Mjumbe wa *PAP* mtu ambaye hajui hata sheria kwamba *allowance* za kibunge hazikatwi kodi. Kwa hiyo, kwa utaratibu ule ule anakosa sifa za kuwa mjumbe wa *PAP*. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, ili kuweka utaratibu ulio imara na sifa kwa Bunge lako Tukufu wakati mwininge tunapowapa Wabunge nafasi za uwakilishi tuwapime katika viwango tofauti tofauti. Sisi imetuulia vigumu sana kuwazungumza Wabunge wenzetu ambao ni wajumbe wa Kamati. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, basi baada ya kusema hayo, nakushukuru, naunga mkono hoja. (*Makofii*)

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Shally Raymond atafuatiwa na Mheshimiwa Kirumbe Ng'enda.

MHE. SHALLY J. RAYMOND: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa nafasi hii. Kipekee namshukuru Mungu sana kutuweka hapa ili tuongee masuala muhimu haya kwa maslahi ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, amani, amani, amani, nikiuliza hapa mna amani? Wote mtasema ndiyo na ndiyo maana mko chini ya jengo hili mkisikiliza na mkitafakari na mkifanya kazi nzuri hizi kwa wananchi wenu. Amani ni kitu muhimu sana kwa mtu mwenyewe kwenye nafsi yake na kwa mtu na watu wake na Taifa na viongozi wa juu na wananchi wao.

Mheshimiwa Spika, nimesimama hapa kuzungumza machache. Mimi ni mjumbe wa Kamati hii na mashahidi ninaowazungumzia ni wajumbe wenzangu. Kwa heshima na taadhima, naomba niseme kwamba matamko yaliyotoka kutoka kwa wenzetu hawa yaliletta mtafaruku kwenye nchi yetu. Naanza na Mheshimiwa Josephat Mathias Gwajima, yeeye ni Mbunge mwenzetu, ni mtu tunayemsikiliza, ni mtu

tunayeishi naye lakini pia alituambia yeye ni Mchungaji au ni kile cheo kingine hapa nchini na kwa mataifa mengine.

Mheshimiwa Spika, aliposema mataifa mengine na akaleta ushahidi pale kwetu akisema kwamba anapozungumzia chanjo anazungumzia hapa na anaikataza hapa, nikajuliza na bado najuliza kama waumini wake wako nchini hapa na nchi nydingine haya mambo yaliyvoanza nchi nydingine kwa nini hakuzungumzia nchi hizo? Kwa nini linakuja kuzungumziwa hapa leo? Kweli yeye Kanisa lake ni kubwa lakini chanjo zimeanzia nje ndiyo zikaja hapa, kwa nini hakukataza kule kwa nini anakuja kukataza hapa? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, jambo hili la chanjo katika nchi yetu ni hiari mtu uamue uchanje au usichanje lakini anapolitamka yeye na analitamka kwenye nyumba yake ya ibada au kwingineko anakataza, anapokataza anakwaza, anapokwaza ni kwamba anamnyima mtu uhuru wake. Unaposema imani ni kitu *very sensitive*, imani yako ndiyo inakupa wewe ujisikie unajiamini na unakuwa huru. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa katika kujadili jambo hili kwenye Kamati mengi yamezungumzwa na Mwenyekiti wangu na mimi ni sehemu ya yale yaliyozungumzwa. Jambo gani limenifanya nisimame na kuomba kuchangia ni kwamba mtu mmoja au watu wachache wasiingilie uhuru wa mtu. Wahenga walisema hiari yashinda utumwa ndiyo maana Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan alipotuambia tuchanje alisema hiyo ni hiari yenu hatukulazimishwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sasa inatia uchungu, inakera na unajua kwamba mimi nimesimama hapa kama kiongozi wa wanawake nikijua jinsi gani wanawake wanaimani na wanapenda kusikiliza viongozi wao, tutakavyobweteka tukasema ameongea kiongozi yule tusijilinde, tusilinde wengine tunakwenda kuhatarisha familia zetu. Naunga mkono adhabu zilizotolewa kuhusu shahidi huyu kwa sababu yeye alitukwaza alipokuwa akisema kwamba anazungumza kwa kuoteshwa au kwa kufuata Roho Mtakatifu. Mimi ni Mkristo Roho Mtakatifu ndiyo tunavyobatizwa, tunabatizwa

kwa maji na Roho Mtakatibu. Huyu Roho Mtakatifu asiyetaka utakatifu anataka vitu basi huyu siyo Roho Mtakatifu bali Roho Mtakavitu. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, jambo la pili ni suala la Shahidi Mheshimiwa Jerry Silaa, haihitaji *rocket science* kuzungumza na kusema kwamba mshahara unakatwa kodi. Kodi ni kitu ambacho kiko kwa mujibu wa sheria na kuna kodi nyingi sana katika nchi hii na hii kodi ya mshahara ipo. Wabunge wanalipwa mshahara kama *public servants* na *Pay As You Earn* inakatwa, sasa sioni ni kwa jinsi gani mtu mwelewa kama Mbunge anakwenda kwenye mikutano yake ya hadhara anapigiwa makofi, anapata mihemko na anazungumza zaidi ambavyo angetakiwa.

Mheshimiwa Spika, nasikitika sana kwamba Mheshimiwa mwanangu huyu alisema hatukatwi kodi na aliulizwa, je, wewe ulikuwa unakatwa kodi ulipokuwa Mstahiki Meya? Akasema yeye alikuwa anapata posho na alikuwa hakatwi kodi. Sasa kama hivyo ndivyo kwa nini wakati ule hakuliona ni tatizo amekuja kuona ni tatizo leo hapa? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mtu unakaa unajiuliza Bunge hili lillianzishwa miaka mingi nyuma toka enzi za mkoloni na yanayofanyika hapa yalikuwa yanafanyika, kwa nini hao wote waliopita miaka hiyo hawakuona, inakuja kuonekana leo, unajiuliza hapa kuna jambo gani? Kwa nini limeleta simanzi na tataruki? Unajiuliza hivi hii ni sawa, tunyamaze? Hatukuweza kunyamaza, naunga mkono adhabu zilizotolewa.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Shally Raymond. Mheshimiwa Kirumbe Ng'enda atafuatiwa na Mheshimiwa Tunza Malapo.

MHE. KILUMBE S. NG'ENDA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii. Nataka niseme kwamba sina kawaida sana ya kuzungumzia mambo hasa

ninayoona yananitia uchungu kwa watu ninaowafahamu vizuri na hasa Wabunge wenzangu, lakini mnapofika mahala mnataka kutengeneza chombo ni lazima mkubali kwamba, kama yuko mtu anapasua mtumbwi ili mzame, basi bora azame yeye lakini chombo kiendelee kufanya kazi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sisi Wabunge tuliomo humu tumeletwa na vyama vyetu kupitia kura za wananchi, vyama vyetu vina katiba na miongozo, chama kikongwe kama CCM kina mpaka Kanuni za Maadili na Uongozi, zinazoonyesha miiko, zinazoweka makatazo na utaratibu. Kwa bahati mbaya, niseme kwa mfano Shahidi Mbunge mwenzetu Mheshimiwa Gwajima, labda muda wake wa kuwepo kwenye CCM umekuwa ni mfupi sana, labda mambo haya hajapata nafasi nzuri ya kuyasoma. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, si hilo tu, tukishachaguliwa tukifika hapa, hatuanzi kazi mpaka tubebe Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na tuape kuitii, kuitetea kwa mujibu wa sheria. Katiba hiyo inayo mambo ambayo yanatutaka lazima tuyafanye kwa sababu tumeapa, unashangaa na unajuliza na unapata shaka, hivi hawa wenzangu wanapata nafasi ya kupita hii miongozo. Kama wangefahamu vizuri nadhani tusingefika huku tulipofika. Alipoanza Mbunge mwenzetu Mheshimiwa Gwajima, alianza kama anatoa ushauri hivi, akaeleza kuhusu hizo chanjo na nini, halikuwa jambo bayo na wakati huo Rais wetu mpendwa alikuwa ameunda Kamati ya Wataalam kumshauri kuona namna ya kuliendea jambo la kupambana na *COVID*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hata kama unaamua kumshauri Rais, Katiba ulioapa nayo Ibara ya 37 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, inayoeleza majukumu ya Rais, inaonyesha kwamba Rais yuko huru katika kazi yake, halazimiki kufuata ushauri, ukimpa anaweza akauchukua au asiuchukue na atatimiza wajibu wake. Kama Rais alikuwa ameshaunda Kamati ya Wataalam hana lazima ya kusikiliza ushauri wa Askofu, maana jambo lenyewe la ugonjwa ni la kitaalam.

Mheshimiwa Spika, tuache Katiba na miongozo ya chama, ndugu yetu huyu ni mtumishi wa Mungu, Askofu, imeshafika mahali jambo liko kwenye mamlaka ya Rais analishughulikia, unawezaje kufika mahali ukaanza tena kuhoji, kwenda mbele kuchochea watu, hasomi hata Biblia yenyeewe inasemaje? Kwamba mtii mamlaka maana hakuna mamlaka isiyotoka kwa Mungu (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, haya ya Kanuni, ya Katiba yamempita na ya Biblia yamempita? Si hilo tu hata sisi tunaoamini katika Uislamu imeandikwa *atwiu-Allah, waatwiu rasuli wauli-l-amri minkum*, kwamba tumtii Mwenyezi Mungu, tumtii Mtume na tuwatii wenye mamlaka mionganoni mwetu. Huu aliouonesha mwenzetu siyo utii kwa mamlaka. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa bahati mbaya, tunapokuwa hapa ni vizuri tujue viwango vyetu, umeingia siasa jana, Ubunge una miezi sjui sita au tisa, lakini hata huko kwenye Biblia, si tuyashi maneno ya Bwana Yesu. Ukiilikwa kwenye harusi usikae viti vya mbele, maana mwenye harusi anaweza akaja na watu muhimu akakupeleka nyuma, kaa viti vya nyuma ili kama ye ye atakuona wa muhimu akulete mbele maana ajikwezae hushushwa na ajishushae hupandishwa na haya maneno hayajui? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sasa amekuja hapa Mheshimiwa Gwajima amekaa viti vya mbele, hata sisi tuliookaa siku nyingi humu kwenye chama hiki tunamwangalia, lakini basi umefika mahali umekaa viti vya mbele, unaanza tena kupiga mawe kitu cha bwana harusi na sisi tukuangalie tu haiwezekani. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Wabunge karibu wengi ambaao tumekutana huko nje tunazungumza juu la tukio hili la mwenzetu, kila mmoja anasema kwa kweli huyu bwana kafanya vibaya. Sasa ukiwaliza mbona hamkemei, wanasema hapana tunaogopa, atapanda madhabahuni kwenda kutuchapa pale kutukashfu. Mheshimiwa Gwajima, Mbunge mwenzangu, mimi nimejitoa kama dhabihu, nipeleke kwenye madhabahu siku ya jumapili, nichape

ujuavyo, lakini mwachie Mama Samia na Serikali yake wafanye kazi. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, narudia tena nimejitoa, nikwambie kwa nia ya kukurekebisha kama Mbunge mwenzetu, twende pamoja, ukiamua kwenda kutumia jukwaa la Mungu badala ya kuongoza kondoo kuanza kuwasema watu, endelea hivyo ila ujuwe Mungu anakupa muda. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Kilumbe Ng'enda.

MHE. KILUMBE S. NG'ENDA: Mheshimiwa Spika, naomba dakika moja.

SPIKA: Haya malizia.

MHE. KILUMBE S. NG'ENDA: Mheshimiwa Spika, mimi nimechukulia wito wa mama yetu na juhudhi alizozifanya Mheshimiwa Rais wetu, tena nimenukuu maisha ya Nabii Nuhu, alipoona watu wake wanatenda makosa mengi kwa Mungu na Mungu akamletea ufunuo kwamba, mimi nataka kugharikisha, alikwenda akawasihi watu wote, jamani tutengeneze safina tupande, Mungu analeta gharika kutokana na makosa tuliyofanya, sasa tujisalimishe tukae kwenye safina. Wako baadhi ya watu mpaka ya wa familia yake walimpinga. Kilichotokea gharika ilikuja na wote waliompinga waliangamia. Mama ametutaka tuchanje na akatuomba kwa hiari anayetaka achanje, asiyetaka aache, sisi tulioamua kuchanja tunasubiri safina iwe tayari, wale ambaao wamekataa litakapotokea gharika ya Mungu shauri yao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hivi kweli angekuwa Mheshimiwa hayati Magufuli ndiyo Rais leo, Mheshimiwa Gwajima angeweza kusema hayo aliyyoyasema? Wakati wa mwalimu Julius Kambarage Nyerere, mwaka wa 1979, alikuwepo Mjumbe mmoja wa Halmashauri tena Mjumbe wa Kamati Kuu na alikuwa Mkuu wa Idara ya *Organization*, namkumbuka alikuwa mtu wa kwetu, mzee wetu, ameshatangulia mbele ya haki, Mungu amuweke mahali

pema, alikua anaitwa Tuwakali Karangwe. Iliwekwa karantini ya kipindupindu alipokwenda kule Kigoma akakuta *ma-barrier* watu wanazuila wasiende huku kwa imani tu ya kutaka watu wala sio kwa kiburi, akawaambia fungueni watu waende wakapate huduma, kipindupindu kikaathiri watu wakafa, alilazimika kujiuzulu nafasi zake zote za uongozi.

(*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mtu anachochea watu wasichanjwe na kushambulia wale wanaohamasisha na wanaoleta chanjo, katika CCM hii ninayojua adhabu bado.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja, nakitaka chama kiangalie vizuri adhabu hii. Ahsante sana.

(*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Kilumbe Ng'enda. Mheshimiwa Tunza Malapo atafuatiwa na Mheshimiwa Joseph Anania Tadayo.

MHE. TUNZA I. MALAPO: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii. Awali ya yote kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu na nataka kuwaambia umma wa Watanzania kwamba Mheshimiwa Gwajima Josephat ameshindwa kuthibitisha mbele ya Kamati, kuleta kielelezo chochote cha zile tuhuma nzito ambazo amezitoa kwa Viongozi Wakuu wa Nchi hii. Alisema ana vielelezo, atakuja kusema, nawaambia hakuja hukusema jambo lolote la msingi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba Watanzania kwanza watambue hilo, amekuja pale na vituko tu, mara hataki kiti, mara hataki microphone, mara leo nasimama, lakini hakuleta kielelezo chochote, tulimhoji maswali na sisi tulikuwa *sober*, inawezekana angetusaidia jambo kuna jambo analijua, lakini kwa masikitiko makubwa hajui lolote. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, amesema chanjo ya J&Jimeletwa kwa sababu watu wamekula pesa. Tukamwambia tunaomba Ushahidi, hana. Akasema watu watakao chanjwa watakuwa

vichaa, watakuwa hawazai, sijui tutatembea barabarani tunaongea wendawazimu, tuletee Ushahidi, hana.

Mheshimiwa Spika, akatoka hapo tulipomwambia hivi haya mambo unayoyasema wewe huoni kama unaleta tahiruki kwenye nchi. Halafu mbaya zaidi huyo kiongozi aliyeiyazungumza haya yupo kwenye chama chako, kwa nini usitafute *venue* ya kwenda kuongea naye ukamshauri, unakuja kuyatoa mbele ya umma? Kwa masikitiko makubwa alisema hivi; yale ameyasema, atasema akiwa ndani ya Bunge, atasema akiwa nje ya Bunge, atasema akiwa juu ya dari na atakayemsemesha atasema zaidi ya mara mbili.

Mheshimiwa Spika, nakupa taarifa, Mheshimiwa Gwajima alitwambia kwenye Kamati kwamba, ataendelea kusema, sasa kazi kwenu ninyi wenye mamlaka. Yeye amesema ataendelea kusema, amesema mbele ya Kamati na *Hansard* zipo zimerekodi vizuri sana, kwa hiyo tujiandae. Leo jumatatu, tusubiri jumapili inayokuja hatujui kitakwenda kusemeka kitu gani. (*Makofii/Kichekoj*)

Mheshimiwa Spika, naomba sasa niongee suala la Mheshimiwa Jerry Silaa. Hapa mkononi mwangu nimechukua *salary slip*, hii ni ya kwangu mimi Tunza Issa Malapo. Siwezi kutaja mshahara wangu, mshahara ni siri, siwezi kutaja *figure*, naogopa na mimi ndiyo nitarudi kule kule kwa mwenzangu, lakini nataka kuwaambia Watanzania, nitakupa hii ya kwangu kwa ridhaa yangu uione labda inawezekana hujapata muda wa kuangalia, mimi hii ya kwangu nakatwa kodi. Ni Mbunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, tena nakatwa kodi ya kutosha tu, ukilinganisha na watumishi wengine wa umma, sisi Wabunge tunakatwa kodi kubwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, tulipokuwa kwenye Kamati tunashangaa, huyu mwenzetu haya mambo ameyapata wapi? Tukajua basi angalau atajirudi, aseme labda niliteleza, kama aliteleza basi tumwinue, twende naye, lakini mwenzetu ndiyo kwanza ametuletea vitabu mpaka vimemziba hatumwoni. Sasa yale ya vitabu sisi tukayavumilia kwa

sababu, jamani Waheshimiwa Wabunge tunaongea leo tunaongea kwa *fact*, hivi hili suala la Jerry lilipaswa lifike hapa liliopofika? (*Kicheko*)

WABUNGE FULANI: Wala, hapana.

MHE. TUNZA I. MALAPO: Mheshimiwa Spika, katika hali tu ya kawaida, kwa sababu binadamu yeote kukosea ni jambo la kawaida na ndiyo maana tunaenda Misikitini na Makansani tunaenda kuomba msamaha. Hili suala lake mimi kwa akili yangu ya kawaida tu ndogo, ni kwamba mwenzetu mimi nilichukulia ameteleza, sasa kama ameteleza mwenye mamlaka Mkuu wa Mhimili alimwambia, *you just go there*, kawaambie watu kwamba niliteleza kwa sababu ushahidi si upo. Hapa hatupigi ramli ndio maana mimi mkononi kwangu nimeshika *salary slip*, hatufanyi ramli tunaongea vitu ambavyo vipo na vinaonekana. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, lilikuwa ni suala la kwenda tu kusema kwamba nimeteleza, lakini kwa nini hawezi kwenda kusema? Ninachoona mwenzetu ana kiburi, yaani ameja tu, ile wanayosema kunyanya mabega, kwamba nionekane mimi nakwenda kusema nimekosea, nimefanya hivi, *which is not good*, katika maisha ya kawaida ya mwanadamu yoyote.

Mheshimiwa Spika, sasa Mheshimiwa Jerry anatakiwa, kwanza naunga mkono adhabu aliyopewa, lakini nafikiri, sijajua sijui niseme anatakiwa apate *psychological counselling* sijui kitu kama hicho. Siongei hivyo kwa maana kwamba namtukana au nini, mimi ni mwalimu na Saikolojia ni somo ambalo tunafundishwa, *sometimes* mtu unaweza ukakuta anafanya mambo wewe unashangaa, kwa nini huyu mtu anafanya hivi! Hili suala kwa upande wangu naliona ni kubwa, lakini ni dogo, endapo tu yeye angeamua kuli-*handle* kwa namna ile ambayo mimi naiona.

Mheshimiwa Spika, sisi tunakatwa kodi na ile posho ambayo hatukatwi kodi ina matumizi, kama mimi nimepewa hela ya mafuta ya lita 10, nitalipia kodi hivi nitapata yale mafuta lita 10? Sipati, kwa hiyo ni mambo ya kawaida

ambayo yanataka tu uelewa wa kawaida. Nawaambia Watanzania sisi Waheshimiwa Wabunge tunakatwa kodi kwenye mishahara yetu, tena kodi ya kutosha. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. (*Makof*)

SPIKA: Ahsante sana Mwalimu Tunza. Mheshimiwa Tadayo, tafadhalii, utafuatiwa na Mheshimiwa Ali Hassan King.

MHE. JOSEPH A. TADAYO: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kupata nafasi hii. Nami pia kwa nafasi yangu kama Mbunge na Mjumbe wa Kamati iliyoleta hoja, naunga mkono hoja ambayo imeletwa kwa asilimia mia moja. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, tulipewa kazi hii na wewe ili kuwapa haki wenzetu hawa ambao kwa mujibu wa kanuni tunawaita mashahidi, kuwapa ile haki yao ya kikatiba ya kuwasikiliza. Tuliwasikiliza chini ya kiapo na wakakubali kwamba kweli hizi kauli ni wao walizitoa. Inakuja sasa kuangalia juu ya uhalali wa kauli hizi kisheria kama ambavyo ripoti imezungumza kwamba unasimama, unasema kwamba viongozi wamepewa fedha ili kuruhusu chanjo ambayo si salama iingie. Kwamba kila anayetetea chanjo, kila anayechanjwa ikiwa ni pamoja na mimi kwamba ni hela, ni hela, ni hela. Halafu unafika mahali unajigamba kuwa juu ya kila mtu, kuwa juu ya Bunge, kuwa juu ya Spika kwamba mimi naweza nikafyatua mtu ndani ya Bunge, naweza nikafyatua mtu nje.

Mheshimiwa Spika, sasa ni wazi kabisa kwamba hata bila kusoma sheria, kila mtu anapaswa kuthibitisha yale mambo ambayo anayasema dhidi ya wenzake, kwa sababu kila mtu anastahili jina lake liwe safi kama lilivyo. Kwa maana ya kwamba mimi nimeajiriwa, nafanya kazi ni Waziri wa Sekta au nafasi ye yeyote ile. Kazi yangu naifanya kwa mujibu wa sheria, sasa kama unasema kwamba mimi nimepewa hela ili nifanye hivi, basi unao wajibu wa kuthibitisha jambo ambalo shahidi wa kwanza, Mheshimiwa Gwajima alishindwa kabisa kufanya hivyo.

Mheshimiwa Spika, hali kadhalika kwa shahidi wa shauri la pili, Mheshimiwa Jerry Silaa, dai lake kubwa kwamba mishahara ya Wabunge haikatwi kodi. Sasa waraka wa msingi, *primary document* ya kuthibitisha mshahara wa mtu huwa ni *salary slip* ile ambayo inatumika kukulipa wewe mshahara. Mmiliki wa ile *document* ni yule anayekulipa, sasa Mhasibu Mkuu wa Bunge ameshakuja, ameshatoa ile, ametenga ile *salary slip* ni hii hapa, inakatwa kodi na amesema inakatwa kodi na ametueleza kwamba hata wakusanyaji kodi wenyewe waliwahi kuja wakatazama hili jambo, wakaridhika nalo. Hata hivyo, bado mtu unasisitiza kwamba upo sahihi. Maana yake sasa huu kwa kweli ni uvunjaji sheria wa makusudi tu ambao ndijo maana Kamati ikafikia hapo kutoa adhabu hizi ambazo mimi naziunga mkono kabisa. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, ni vizuri sisi Wabunge tukakumbuka kwamba baada ya kuchaguliwa tulipa kuilinda, kuitetea na kuhifadhi Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Katiba hii ndijo iliyoweka hii mihimili ambayo tunazungumzia habari ya kuigonganisha na kuidhalilisha. Katiba hii ndio inayogawa mamlaka na madaraka ya watu kufanya kazi. Pia Katiba hii imetupa nafasi hasa sisi Waheshimiwa Wabunge namna ya kuhoji au namna ya kurekebisha mambo ambayo tunafikiri hayaendi sawasawa. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 63, kwamba tunayo mamlaka ya kumhoji Waziri ye yeyote juu ya suala lolote lile ambalo tunaona haliendi sawa. Sasa endapo basi tunadhani kwamba Serikali inakwenda ndivyo sivyo hatuna mamlaka ya kwenda kuwahojia huko kwenye maeneo yetu, kwenye vikundi vyetu vya ngoma au kwenye Makanisa au mahali pengine popote pale. Sheria inatuongoza na kutupa wajibu kabisa wa kuja kuihoji mahali ambapo ni stahiki. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, hali kadhalika, endapo basi mtu ameona kwamba sheria inayotulipa sisi mishahara kama ilivyo kwenye kifungu cha 20 cha ile *National Assembly (Administration) Act*, haipo sawasawa, basi unataka kuanzisha mchakato wa marekebisho, basi sidhani kama

mchakato unaanzishwa hivyo. Sisi ni Wabunge, tunafahamu utaratibu wa kuanzisha mchakato wa marekebisho ya Katiba ili hata ile posho ya mafuta ambayo ukienda kununua mafuta tayari kodi imeshakatwa, kama unataka na yenyewe ikatwe tena sijui mara ya ngapi, basi mchakato wa kisheria upo wa kufanya hivyo, sio kwenda kuchochea wananchi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa sasa hivi, hizi kauli za wenzetu hawa wote wawili *effect*yake pia ni kuwachochaea wananchi kuichukia Serikali. Kwa sababu kwa upande mmoja ya Mheshimiwa Gwajima ni kwamba anawachochaea wananchi waone kwamba Serikali haijali afya zao, Serikali haijali usalama wao. Kwa hiyo watu wanapokea tu fedha huko wanaleta machanjo ambayo sio sahihi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hii nyingine ni kwamba Serikali ina upendeleo kwamba wengine wanakatwa kodi, wengine hawakatwi kodi. Kwa hiyo kauli zote hizi mbili zinakwenda zaidi hata ya makosa yetu ya kikanuni, kuna uchochezi hapa pia. Kwa hiyo ni vizuri kabisa Azimio hili la Bunge likapita kama ambavyo Kamati imelileta. Naliunga mkono, twende hivyo, turekebishesane ili tuweze kwenda sawasawa katika kuwatumia wananchi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana na naunga mkono hoja kwa mara ya pili. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Ali Hassan King, atafuatia na Mhehimiwa Agnes Hokororo na Mheshimiwa Sophia Mwakagenda, ajiandae.

MHE. ALI HASSAN OMAR KING: Mheshimiwa Spika, ahsante. Awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu.

Pia napenda kukushukuru wewe kwa kunipa hii nafasi ambapo Wabunge wengi sana wamezungumza kuonyesha hisia na kuonyesha kushangazwa na vitendo vya Wabunge wenzetu ambavyo vimetokea na zile *comedy* zote zilizojitokeza. Nafikiri kuna neno moja tu hapa tukisema,

tutaliweka sawa hili. Kuna msemo mmoja unasema *Khalif Tunraf*; wewe ukitaka ujulikane, upate umaarufu, basi wewe nenda kinyume tu.

Mheshimiwa Spika, kule kwetu kuna mtaa mmoja unaitwa Mchambawima; na ni kwa sababu huyo mtu hicho kitendo alikuwa akikifanya wima, kwa hiyo, alikuwa maarufu mpaka jina la mtaa lipo.

MBUNGE FULANI: Mchambawima! (*Makofi/Kicheko*)

MHE. ALI HASSAN OMAR KING: Eeh, kwa hiyo, hapa sasa hivi, kwa hivi tunavyoendelea, kwa watu kutaka umaarufu, tutapata wachambawima wengi tu, kwa sababu mtu ukitaka upate umaarufu, basi nenda kinyume. Ukienda kinyume utapata umaarufu; na ndicho kinachotafutwa hapa. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, mamlaka yaliyowekwa yanapaswa yaheshimiwe. Kama tutakwenda hivi kuchazeana na tutaachiana kama hivi, tutakuja kufika mahali pabaya. Amezungumza hapa Mufti wa Kigoma, Mheshimiwa Kilumbe Ng'enda, kwamba mamlaka anatoa Mungu na Mungu ndio anayempa mtu mamlaka na hakuna mamlaka mengine yejote ambayo hayatoki kwa Mungu. Sasa akitokea mtu akiwa ana dharau mamlaka, hapo moja kwa moja huyo mtu sio wa kumchezea, wala sio mtu wa kuchenza naye. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Gwajima ameeleza kwamba Serikali au watu ambao wameshughulika na chanjo wamepewa pesa; huu ni uongo unaoidhalilisha Serikali, unachochea Serikali na wananchi; na kwa nafasi yake kama Mbunge ina maana kwamba moja kwa moja analidhalilisha Bunge kwa sababu yeje amezungumza kama Mbunge. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mimi sikubaliani naye anaposema kwamba yupo katika mahubiri, alikuwa hayupo katika mahubiri. Ukitazama mtiririko, leo kimesemwa hiki, siku ya pili

yeye ndio anajibu. Leo kimefanywa hiki, siku ya pili anajibu, leo kazungumza Waziri wa Afya, anasema pia atamfyatua. Kazungumza Naibu...; alikuwa anajibu hoja kwa matukio ya Serikali siyo mahubiri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, tukipata wahubiri kama hawa, nafikiri kuna kesi moja. Kuna kisa kimoja cha Askofu Kibwetere aliwafungia watu Kanisani akawachoma. Kuna Askofu mwingine aliwapeleka watu pale uwanja wa ndege, aliwaambia watapata *visa* pale, wakalala wiki mbili pale. Sasa wahubiri kama hawa wakati mwingine lazima tuwatazame. Itakuja mahali, yaani ni *timing bomb*. *Bomb litakuja kulipuka!*

Mheshimiwa Spika, leo katika familia huko watu hawataki kuchanja kwa sababu ya maneno ya watu. Watu hawataki kufuata taratibu za nchi kutokana na maneno ya watu. Sasa mimi niseme moja kwa moja, naunga mkono hoja ya Kamati; na zaidi vyombo vya usalama, hili jambo linatuharibia. Vyombo vya usalama navyo vichukue hatua kali zaidi. Chama chetu nacho kiangalie kifanye nini katika hili kwa sababu hawa watu watatuharibia nchi, nasi hatutaki kufikishwa mahali pabaya. Hapa tunapokwenda, tunakwenda vizuri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nikija katika suala la ndugu yangu Mheshimiwa Jerry Silaa, ni kweli alikuja mbele ya Kamati, lakini mimi mwenyewe nashangaa kwamba kweli tufikie katika hatua hii Wabunge hatujui kama tunakatwa kodi! Au ndiyo tunarudi kule mchambawima! Halafu unakuja mbele ya Kamati, yaani mambo yote yanakuwa ni ya vituko vituko. sasa hii, nahisi adhabu iliyopendekezwa na Kamati naiunga mkono. Pia huku kwenye PAP nako tukutazame, ndiyo mwakilishi wa aina hiyo ndiyo tunampeleka huko. Sasa ni lazima tutazame na lazima tuangalie. Sisi kama Wabunge tukianza kuchafua hali ya hewa tutafika pabaya. Tupunguzeni kutafuta umaarufu jamani! Tupunguzeni kutafuta umaarufu, hili litatuharibia na tutaiharibu nchi yetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja ya Kamati, lakini zichukuliwe hatua nyingine zaidi kwa sababu tunakwenda kuharibu usalama wa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, nashukuru.

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Agness Hokororo na Mheshimiwa Sophia Mwakagenda, tunakaribia mwisho.

MHE. AGNES E. HOKORORO: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Kwanza kwa kuwa nami ni Mjumbe wa Kamati, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Spika, nianze kwanza na hoja ambazo pengine watu wamekuwa wakijuliza, maana ukisikiliza nje ya sisi Wabunge, wapo baadhi ya wananchi katika makundi mbalimbali wanahoji pia kwamba kwa nini Waheshimiwa Wabunge hawa wawili amba ni mashahidi walitokea mbele ya Kamati ama waliitwa kwenye Kamati yako ya Bunge?

Mheshimiwa Spika, naomba niliweke wazi hili kwa sababu pengine hawajui kwamba mashauri haya yote mawili yameshughulikiwa chini ya Sheria ya Haki, Kinga na Madaraka ya Bunge Sura ya 296. Kwa hiyo, siyo suala tu kwamba labda mhimili huu wa Bunge uliamua tu wenyewe bila kufuata sheria; ni kwamba ni suala la kisheria. Pia niwaambie wale amba pengine wamepata mashaka kwamba masuala haya yote mawili yameshughulikiwa kwa mujibu wa Kanuni za Bunge. Bunge lako Tukufu linaendesha shughuli zake kwa kufuata Kanuni za Bunge. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nilikuwa naomba nilieleze hili kwa sababu baadhi huko ukisikiliza wanasema wameonewa, mtu kwa nini ameitwa? Kwa nini hakwenda huku? Kwa nini huku? Pengine wanadhani ni shinikizo la mtu mmoja, lakini kumbe huu ni utaratibu wa kibunge. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, mashauri haya yote mawili kama ambavyo Mwenyekiti wa Kamati amewasilisha mbele ya

Bunge lako Tukufu, yote yameangukia katika Kanuni ya 85 - Utovu wa Nidhamu Uliokithiri.

Mheshimiwa Spika, hapa pia naomba nianze na shauri lile la kwanza la Msheshimiwa Josephat Gwajima. Sote tunatambua kwamba Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imetoa uhuru wa kuabudu, lakini uhuru huo wa kuabudu tunaopewa Watanzania na watu kuanzisha taasisi za kidini hupaswi kuvunja masharti ambayo Katiba hiyo imeweka na sheria nyingine za nchi yetu. Tunajua sote kwamba hakuna uhuru usio na mipaka; yaani haiwezekani mimi leo; na kwa sababu kuanzisha Kanisa au taasisi ya kidini mtu yejote anaruhusiwa; haiwezekani leo nikatoa maneno ambayo yanavunja sheria nyingine za nchi tu kwa kisingizio cha uhuru wa kuabudu. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kwa maneno ambayo yalisemwa na shahidi hayana shaka. Naomba niungane na Wabunge ambao wametangulia kwamba maneno yale yanaweza kuvunja amani na utulivu wa nchi yetu. Sasa tukiachia hiyo tukasema sasa kila mtu aamke tu, sidhani kama tunaweza tukaendelea kufurahia nchi yetu katika uwanda huu mpana wa utulivu ambao unamwezesha kila Mtanzania kufanya shughuli zake. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mbunge King hapo amesema, ukiacha ile mifano ya Kibwetere, tuliona pia kwenye maeneo mbalimbali; nakumbuka kama sikosei kule Kagera kuna mchungaji alitokea Kanisani akasema ameoteshwa aoe mke wa mwingine Kanisani, lakini tuliona Serikali pia ambaye ni Mkuu wa Wilaya alienda akachukua hatua kuhusiana na lile. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, pia yapo maeneo mengine. Kwa hiyo, kwa ufupi tu tuseme kwamba hili pia ambalo limefanywa na Mheshimiwa Gwajima kwa kisingizio kwamba alikuwa anasema yale maneno akiwa anahubiri waumini wake kwenye nchi 142; na kwa kuwa alikiri Tanzania ni miongoni mwa hizo nchi 142; kwa kufanya hivyo kwa kweli sioni kama

kuna shaka kwamba alikuwa anajaribu kuizua Serikali kutekeleza wajibu wake. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, niwasihi Wabunge kuliunga mkono Azimio hili la Bunge ili kuendelea kuulinda utulivu wa nchi yetu, kuilinda amani ya nchi yetu na pia kuleta ustawi wa jamii zetu. Hii chanjo ambayo pengine watu wanahimizwa wasiende kuchanja, tuliambiwa wote ni kwa hiari, lakini pia mashaka yale mengine ambayo yametolewa na mzungumzaji yanaendelea kuwachanganya wananchi. Kwa sababu akisema daktari yejote atakayebisha amepewa pesa, sasa tunaendelea kuwachanga wananchi. Kwamba hawa hawa Wabunge wanasema hii chanjo isichanjwe kwa sababu hakuna nafasi ambapo Mbunge anapofanya shughuli nyingine nje ya Bunge utasema sasa mimi Agness Hokororo sio Mbunge, nafanya kazi zangu kama mwananchi wa kawaida kwa sababu wote tumekula kiapo kwa mujibu wa Katiba.

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

SPIKA: Ahsante sana, ahsante Mheshimiwa.

MHE. AGNES E. HOKORORO: Mheshimiwa Spika, ahsante. Naunga mkono hoja.

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Mwakagenda Sophia, atafuatiwa na Mheshimiwa Mariam Ditopile.

MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipatia nafasi nami niweze kuchangia mada iliyokuwa mbele yetu. Naomba niwakumbushe waumini wa makanisa 142 ya Gwajima, lakini pia waumini wa Tanzania juu ya Biblia inasema nini? Biblia inasema, katika Marko 16:18a, "hata tukila vitu vya kufisha, havitatu dhuru." Hivyo basi, napenda kumwambia Askofu Gwajima kwamba, Biblia hiyo inazungumzia hata nikichanja chanjo iliyokuwa na sumu kama, imani yake yeye kama Askofu, hafahamu kwamba chochote kibaya kitakachoingia kwa waumini

wake hakina madhara katika miili yao sawa sawa na Biblia inavyosema. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, pia Biblia hiyo hiyo inasema katika Waefeso 6:12 inasema hivi, "kwa maana kwetu sisi damu na nyama, bali si juu ya wafalme na mamlaka ya nguvu za giza, vita vyetu sisi ni vya katika Ulimwengu wa Roho." Sasa kama yeche ni mtu wa imani, kama tukibebwa katika imani kitu chochote kibaya hakitawapata Watanzania na ndivyo tulivyo na ndiyo maana tunaenda mahospitalini tunatibiwa, Wakristo wanajenga zahanati, wanajenga hospitali, kwa sababu tiba ni sehemu ya mamlaka ya Mungu. Hata Nabii Luka aliandika Kitabu cha Luka alikuwa ni daktari maana Biblia inawatambua madaktari. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, Biblia hiyo hiyo inasema, katika Waembrania 11:1 "imani ni kuwa na hakika na mambo yatararijwao ni bayana na mambo yasiyoonekana." Ukiwa na imani hakuna kitu kibaya kitakupata. Gwajima usiwakwamishe Wakristo wako na Wakristo wa Makanisa 142, imani itatulinda kama Watanzania, tutakula dawa na vitu vibaya havitatupata maana tunamwamini Mungu, na Mungu yupo katika Taifa la Tanzania. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, Waraka wa Tatu wa Yohana 1:2 inasema: "Mpenzi naomba ufanikiwe katika mambo yako yote, katika mambo yako ya rohoni na ya mwilini." Hivyo basi, Biblia inatamka mwananchi wa kawaida afanikiwe mwilini, afanikiwe katika roho. Kuchoma sindano ni haki na ndiyo maana hata Gwajima akiumwa anakunywa *panadol* kwa kuwa Serikali inaamini Biblia inatambua katika matibabu.

Mheshimiwa Spika, walikuwepo viongozi wa dini ambao mapepo yaliwavaa; amemsema ndugu Kibwetere. Katika mwaka 2000 Machi, 17 alichoma kanisa na watu walikufa. Naomba tusimame katika imani ya Mungu, tusiwadanganye wananchi. Nanyi wananchi someni Biblia mjiamini. Ndiyo maana ukienda kujifungua, kama wewe ni Mkristo unakwenda hospitali kwa nini? Kwa sababu

madaktari wana elimu ya kimungu. Hujifungulii nyumbani. Gwajima asiwadanganye watu. Ahsante. (*Makofi*)

SPIKA: Mheshimiwa Mariam Ditopile, atatufungia shughuli hii Mheshimiwa Elibariki Kingu, halafu nitamwita mtoa hoja.

MHE. MARIAM D. MZUZURI: Mheshimiwa Spika, nashukuru. Ninukuu maneno ya Mheshimiwa Rais wetu Kipenzi Mama Samia Suluhu Hassan aliyozungumza pale Dodoma *UDOM* akiwa anaongea na viongozi wa dini mbalimbali. Alisema, Wabunge tulieni, acheni kudemka. Sasa sijui hatukumwelewa! Kwa sababu leo hii wananchi wetu wana changamoto nyingi, wanatutaka sisi Wabunge wao tuje hapa tuielekeze na kuieleza Serikali namna gani ya kuunga mkono juhudzi za Rais wetu ili Tanzania ifike kwenye nchi ya ahadi. Leo hii tunapoteza masaa yote kwa ajili yao kudemka na kutafuta kiki. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kaka yangu *Bishop* Gwajima anajua ni namna gani ninampenda na tunaongea mambo mengi, lakini mimi siyo mnafiki. Nilimwandikia ujumbe mfupi kwenye *WhatsApp* nikamwambia kaka hapa umepotoka. Hatukatai kutokekubali chanjo; na ndiyo maana msimamo wa Serikali chanjo ni hiari, lakini mwenzetu huyu anatumia vibaya kanisa lake kwenda kuweka tuhuma nzito kwa viongozi wetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, unaposema viongozi wamepewa fedha, Mheshimiwa Rais amepokea rushwa, ndicho unachomaanisha. Ukitisema viongozi wetu chanjo wanazopigwa wanadanganya, unamaanisha Mheshimiwa Rais, Mheshimiwa Spika ambaye kwa kweli ndio anayetuongoza hapa, Waziri Mkuu na wote waliochanja wanawadanganya Watanzania. Ni vizuri mmemwita mbele ya Kamati ameshindwa kuleta vielelezo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Kawe kwenye chama chetu waligombea wengi. Kawe kwenye Uchaguzi Mkuu viligombea vyama vingi na alitupa mzigo mkubwa sana. Ililibidi

twende *Roman Catholic* tufute mambo aliyoyasema, ilibidi twende kwa Waislamu tufute mambo aliyoyasema, chama kimemwamini, wananchi wa Kawe wamemwamini, ana majukumu ya kuwatumikia wananchi wa Kawe, arudi kwenye mstari. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kaka yangu Mheshimiwa Jerry Silaa kwanza sisi kama vijana wenzake; sijui wasomi wenzake wanasheria, maana mimi sio *penguin*; tumesikitishwa mno na *drama* zako. Umeitwa kwenye Kamati, jishushe *brother*, tuna safari ndefu. Unamtunishia misuli Ndugai, mwenzako kawa Mwenyekiti, Naibu Spika, Spika miaka kumi. Kongwa mimi mwekezaji kule, wanampenda huyu hawataki hata astaafu. Umekuja na begi zima unaanza kuongea kauli za shoo shoo, umejibiwa na vitu viwili; *salary slip* na kitabu hiki chenye maslahi na mwongozo wa kazi za Mbunge. Unajiita Wakili Msomi, nami nilli-*post* picha yako kabisa umevaa joho. Kaa ujithathmini, Taifa lilikuwa linakuhitaji, umeshajitia doa. Rudi kwa Mungu wako, rudi kwa wazazi wako, rudi kwa viongozi wako, chutama. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwa kweli mimi niseme naunga mkono Azimio la Kamati, lakini adhabu ni ndogo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwa suala alilolifanya Gwajima ni uhaini. Sisi kama Watanzania tunayemwamini Rais wetu, mimi kama Mwanachama wa CCM ambaye namwamini Mwenyekiti wangu, anapaswa kupewa adhabu. Kama anaona Uaskofu ni mkubwa, atuachie Ubunge wetu. Wapo wana-CCM wengi mahiri wa kuweza kuleta maendeleo makubwa. Kawe ilicheleweshwa chini ya upinzani, tunataka iende mbali. Kwa hiyo, naomba adhabu iwe ya juu kabisa kwenye Bunge na pia hatua nytingine za kinidhamu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, sisi kama vijana tunaipenda nchi hii, hatuko tayari kuona mtu ye yeyote akikwamisha juhudii za Serikali yetu chini ya Rais ambaye kwa kweli siku zote mama huyu hakuchukua fomu kugombea Umakamu wa Rais; Mama huyu hakutaka Urais, alimsindikiza mgombea wake wa Urais kunadi llani ya Chama. Yaliyotokea ni ya Mwenyezi Mungu.

Ndiyo maana tunasema ni chaguo la Mungu, hana kundi huyo. Kwa hiyo, tunaomba kwa kweli adhabu ziwe kali mno na baada ya hapo vyombo vingine vya mamlaka viwape adhabu. Hakuna lingine. *(Makof)*

SPIKA: Umesahau kutoa hoja tu. *(Kicheko)*

MHE. MARIAM D. MZUZURI: Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

SPIKA: Mheshimiwa Elibariki Kingu, tumalizie ili tumuite mtoa hoja.

MHE. ELIBARIKI I. KINGU: Mheshimiwa Spika, nitumie nafasi hii kukushukuru sana wewe binafsi kwa kunipatia nafasi kuwa msemaji wa mwisho, kwenye hoja illyoko mbele yetu. Jambo la kwanza ambalo nataka nilizungumze kuna dhambi moja kubwa sana watu wanaifanya kwa sababu tu wanajua kwamba Rais Magufuli amekufa na hawezি kujitetea. Gwajima katika mahubiri yake niliyoyasikia aliyojatoa kule Kanisani, amesikika akisema toka Rais Magufuli afe mambo yamekuwa yakienda ndivyo sivyo akiwa ananukuu jambo la chanjo ya *Corona*.

Mheshimiwa Spika, baba wa watu Rais Magufuli amefanyakazi yake ametimiza muda wake Mungu amemruhusu apumzike. Ametenda haki na mema mengi kwenye Taifa hili, Hayati Magufuli aachwe apumzike asihuishwe na mambo ya hovyo. Rais Magufuli alipokuwa madarakani alichokishauri alilishauri Taifa tusiwe na haraka ya kukimbilia chanjo lakini hakuzuia Taifa likijiridhisha lisichukue chanjo. *(Makof)*

Mheshimiwa Spika, hii imekuwa ikitumika kama kichaka, Magufuli, Magufuli, Magufuli, Magufuli muachenii Rais Magufuli apumzike na ninasema huko aliko, kaka yangu Askofu Gwajima anisikilize kwa sababu kama mdogo wangu Ditopile alivyosema, sio mnafiki. Nilimfuata Gwajima kwenye simu yake ya kiganjani nikamuambia haya unayoyafanya

ninakushauri unyamaze hayana maslahi na Taifa letu.
(Makofii)

Mheshimiwa Spika, nayasema haya kwa sababu, Askofu Gwajima anasema ana Kanisa na anatumikia watu wa Mungu. Neno la Mungu katika Warumi 13:1 linasema: Kila mtu na aitii mamlaka iliyo kuu; kwa maana hakuna mamlaka isiyotoka kwa Mungu; na ile iliyopo imeamriwa na Mungu. Na ndio maana kwa watumishi wa Mungu wanaomjua Mungu vizuri, Yesu wakati anazaliwa utawala wa Herode palikuwa pana sensa inaendelea Jerusalemu. Yusufu na Mariamu wakiwa ni wasomi wazuri wa Biblia wale watu wakiwa wamejazwa na Roho Mtakatifu *wali-complyna* agizo la Herode la Serikali tena wakati huo, Jerusalemu iko chini ya utawala wa Rumi wakaondoka kwenda kuhesabiwa kwa kutii mamlaka ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, na wakati huo nayasema hayo kitabu cha Mathayo 2:1 kinaonyesha namna Yesu alivyofanya msafara kwenda kutii agizo la mamlaka tena chini ya utawala ambao tunaweza tukasema kwamba walikuwa chini ya ukoloni. Lakini kama hiyo haitoshi Luka 12:7-9 neno la Mungu linasema, Mungu huyu anajua idadi mpaka ya nywele zilizoko katika kichwa chako. Sasa kama Mungu anajua idadi ya nywele kwa nini Mariamu hajasema kwamba Herode anatuita kwenda kuhesabiwa, Mungu anajua idadi ya nywele wagomee mamlaka ya wakati huo. Hiki anachokifanya Gwajima ni kiburi kilichojaa, kuvimba na kulewa sifa za dunia na sio sifa za kumuwalilisha Mungu katika madhabahu. *(Makofii)*

Mheshimiwa Spika, ninayasema haya kwa sababu, Askofu Gwajima ametoa tuhuma nzito sana kwa nchi na nafikiri haya mambo nimejiuliza maswali. Hivi ni kweli Jeshi la Polisi hawaoni *criminality* iliyopo kwa *statementza* Gwajima? Hivi kweli Jeshi letu la Polisi halioni hatari ya kauli za Gwajima kwamba zinaweza zikasababisha hata Serikali ikapinduliwa kwamba Rais ameamua kuuza watu wake? Nimejiuliza maswali nimekosa majibu!

Mheshimiwa Spika, jambo ninalotaka kulisema Askofu Gwajima yuko hapa jirani na ninajua watu watampelekea *clip* na zimfikie kwa sababu tabia ya unafiki msabato mimi sijawahi kufundishwa, nimefundishwa kuita nyeusi nyeusi kuita nyekundu nyekundu. Kitendo alichokifanya Askofu Gwajima jambo la kwanza, kwa mujibu wa uchambuzi wangu Askofu Gwajima alidhamiria kuichonganisha Serikali ya Mama Samia Suluhu na wananchi ili watu waache kuwa na imani na Serikali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kitendo cha Askofu Gwajima kujitokeza hadharani na kuwaambia watananzania kwamba chanjo hii mnayokwenda kuchanjwa hajifanyiwa utafiti, chanjo hii mkiitumia italeta madhara hilo jambo ni *it is a very big if not huge is subordination* kwa mamlaka za nchi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nasema naungana na Mariamu Ditopile, adhabu zitakazotolewa kwa Askofu Gwajima kwa hili, zisiishie hapo hata huyu Halima Mdee aliyekuwa Mbunge wa Kawe hajawahi kutufanyia vitimbi vyatnamna hii anavyovifanya Askofu Gwajima. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hili jambo nataka niseme kwa dhati kabisa limetufedhehesha na mimi nilikuwa nashangaa sana kwa nini chama changu mpaka leo wamekaa kimya hawajachukua hatua? Mwanachama anafikia *stage* ya kufanya haya mambo mazito mpaka Spika unaamua kumuita, Chama cha Mapinduzi kile tunachokijua. *What is wrong with my party?* Kuna shida gani? Jambo hili ni kutaka kukwamisha mipango. Hivi nilikuwa najiuliza amesema Kilumbe Ng'enda Rais Dkt. Magufuli kama Mungu angekuwa hai mpaka leo, Gwajima angeweza kufungua mdomo wake na kuleta hizi chokochoko? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nakuambia Wabunge tuko hapa kama kuna Mbunge anafikiri ya kwamba atatumia *forum* kwa sababu tu hakupendezwa na Rais Samia kuwa madarakani walahi nakuambia *tuta-deal* naye. Sisi *tuta-deal* naye. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nataka nikuambie kama kuna mtu alikuwa anategemea kupata mamlaka Serikalini imetokea bahati mbaya wote hatuwezi kuwa Mawaziri walioko Mawaziri ukaanza kuwachokonoa walahi nakuambia tutadeal na wewe. Ninasema ikitokea mmoja wetu anataka kujenga umaarufu binafsi badala ya umaarufu wa Taasisi na kulinda mifumo ya Taifa letu, kabla hawajaja kwako tutatwangana makonde huko, tuweke heshima. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nimalize kwa kusema pamoja na kwamba naunga mkono maazimio yote ya Bunge, nimemshauri rafiki yangu Mheshimiwa Jerry Silaa kwa dhati ya moyo wangu ninalisema moja ya marafiki zangu wa karibu sana Mheshimiwa Jerry Silaa. Na hata tukio lilipotokea nilimuandikia ujumbe anajua, zaidi ya mara tatu na ninalisema *from the bottom of my heart* tusiposimama kushauriana kwa lengo la kuelekezana sisi bado vijana nina imani Mheshimiwa Jerry atakutafuta, nina imani atakutafuta kwa wakati wake.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kwamba amechelewa chelewa nina imani atakuja, akija baada ya haya wewe mpokee kama baba akiomba radhi mpokee. Kwa sababu, ninajua wakati mwingine kuna mambo yanatokea hapa mtu unashindwa kuelewa huyu ni huyu ninayemjua? Unajiliza maswali. Lakini baada ya kusema hayo binafsi nikushukuru sana na nikupongeze sana kwa namna ambavyo umesimama kulinda heshima ya Mhimili huu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ukiacha Mhimili huu udharauliwe hata huko nje heshima yetu sisi Wabunge haitaonekana. Baada ya kusema maneno haya ninataka nimtie moyo Rais wetu aliyeko madarakani asije akadanganywa na mtu. Hatuwezi wote kuwa Mawaziri, Mawaziri walioko tuwaheshimu tuwaunge mkono. Hatuwezi wote kuwa Mawaziri ikitokea hatujapata nafasi tusiwe chanzo cha kuanza kulidhalilisha Baraza la Mawaziri la kumdhaliilisha Rais. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nakuambia Rais Samia Suluhu Hassan, Mheshimiwa Spika, nguvu yake kwa umma ni kubwa wananchi wanampenda haijawahi kutokea katika historia ya Taifa, fedha zinapelekwa kwa wananchi kwa kiwango hiki anachofanya Rais Samia Suluhu Hassan. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ninaomba jambo moja Mungu aendelee kulibariki Taifa letu, Mungu aendelee kuulinda umoja na mshikamano wa Taifa letu. Mungu amlinde Rais wetu na Mihimili yake yote mitatu ukiwemo wewe Spika. Wasalaam aleykum. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, ninaomba kutoa hoja na kuunga mkono hoja. (*Makofi*)

SPIKA: Mtoa hoja kwa makofi hayo, karibu uhitimishe nadhani dakika 15 zinakutosha sana. Kwa sababu, mengi wamekusemea wachangiaji. Karibu sana mtoa hoja.

MHE. EMMANUEL A. MWAKASAKA – MWENYEKITI KAMATI YA BUNGE YA HAKI, MAADILI NA MADARAKA YA BUNGE: Mheshimiwa Spika, kwa mara ya kwanza humu Bungeni kama kuna hoja ambazo sijawahi kuona hazipingwi na Mheshimiwa Mbunge ye yote ni hii ambayo ipo mbele yetu. Wachangiaji walikuwa Waheshimiwa 10 na wote wameunga mkono hoja ya Kamati. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mchangiaji wa kwanza alikuwa Mheshimiwa Omari Kigua ambaye yeye alizungumza namna Mheshimiwa Josephat Gwajima, ambavyo hakuweza kutoa ushirikiano kwenye Kamati na hata kwenye Taarifa ni kweli Kamati hii nyinyi Waheshimiwa Wabunge ni mashahidi hata kwa zile *clip* chache mlizoziona maana yake zingine zilirushwa.

Mheshimiwa Spika, tulijitahidi kuwa waungwana vitendo vilivyokuwa vinafanyika ndani ya ile Kamati, nimeshangaa kidogo wakati Mheshimiwa Shally Raymond alivyosimama nilitegemea angeweza kusema hata jinsi ilivyokuwa siku moja kwenye Kamati Mheshimiwa Askofu

Gwajima alivyoharibu hali ya hewa ya mle ndani mpaka Mheshimiwa Shally Raymond akasema kama kungekuwa na uwezekano wa kumrushia mtu ngumi humu, leo ingekuwa hivyo lakini wacha tumvumilie. Tulifanya uvumilivu mkubwa sana. Kwa hiyo, alichozungumza Mheshimiwa Omari Kigua ni kweli kuhusu Mheshimiwa Gwajima na hakuonyesha kujutia chochote.

Mheshimiwa Spika, lakini kuhusu Mheshimiwa Jerry Silaa kama alivyosema Mheshimiwa Kigua ni kweli. Yeye alisema amezua tafrani kwa wananchi kuhusu kusema Wabunge hawakatwi kodi. Lakini akasema naomba radhi kwa hilo lakini hakuna mahali ambapo alisema naomba radhi kwa kusema uongo kuhusu Wabunge kutokatwa kodi. Lakini Mheshimiwa Shally Raymond yeye alipoongea Habari ya Mheshimiwa Gwajima aliunga mkono hoja. Lakini alisema kwa nini Mheshimiwa Gwajima hakugusia nchi zingine amegusia tu Tanzania na wakati yeye anajinasibu anawaumini zaidi ya milioni 2,400,000 dunia nzima.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, inaonekana Mheshimiwa Josephat Gwajima yeye alilenga moja kwa moja Serikali kwa matamshi yake ambavyo yanakwenda. Lakini kwenye hili suala la Mheshimiwa Shally Raymond Waheshimiwa Wabunge si lazima mtu umtaje kwa jina unapomlenga. Wanasheria pia mnafahamu kuna neno linaitwa *innuendo* ni mahali ambapo unamuelezea mtu lakini humtaji jina lakini yale maelezo unayoyaeleza hata mtoto mdogo mwenye ufahamu atasema huyu unamlenga fulani.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, Mheshimiwa Josephat Gwajima yeye alilenga moja kwa moja kwa kutumia neno hilo la kisheria kwa sababu inaonyesha wazi Serikali ndio ilituhamasisha kuchanja na Mheshimiwa Rais, Samia Suluhu Hassan ndio alianza kuchanja na kutuhamasisha. Sasa ukisema wamepewa fedha wanaoshabikia chanjo unasema *indirect* lakini unailenga Serikali. Kwa hiyo, ni kweli alikuwa anachonganisha na kugonganisha Mihimili.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Tunza Malapo ye ye amethibitisha hapa kwamba, Mheshimiwa Gwajima pamoja na kwamba aliuaminisha umma kwamba ninakwenda kwenye hiyo Kamati nitapeleka ushahidi mwingine ambao hata sikuusema hata Kanisani. Lakini Mheshimiwa Tunza Malapo aliposimama hapa ni kweli Mheshimiwa Gwajima hakuwa na ushahidi wowote ambao aliowaaminisha watanzania wote.

Mheshimiwa Spika, na kuhusu suala la Mheshimiwa Jerry Silaa ni kweli hata kwenye kikao alikiri kwamba hata ye ye anakatwa kodi kwenye mshahara wake. Sasa tunajiuliza alikuwa na nia gani kuwaambia wananchi jambo ambalo sio la kweli.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Joseph Tadayo aliongelea suala la Mheshimiwa Gwajima kushindwa kuthibitisha suala la Viongozi kupewa fedha ili wachanjwe alishindwa kabisa. Tulipomuuliza unaweza ukututajia Kiongozi hata mmoja ambaye kapewa fedha? tena alibabaika sana mpaka akafika mahali akasema wanakamati mnakumbuka na *Hansard* zipo, ile fedha ni misaada. Lakini tukamuambia kwenye kauli zako hakuna mahali uliongelea suala la misaada lakini ulisema Viongozi wanaoshabikia chanjo wamepewa fedha.

Mheshimiwa Spika, lakini kuhusu Mheshimiwa Jerry Silaa, Mheshimiwa Tadayo alichangia kwamba Mheshimiwa Jerry Silaa alishindwa kuthibitisha kwamba, Wabunge hawakatwi kodi kwenye mishahara yao.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Ali King aliunga mkono hoja kama wengine na ye ye alisema kwamba ili ukitaka umaarufu unatakiwa uende tofauti na wenzio na hapa alisema, uende kinyume na akatoa ile mifano sikumbuki vizuri alisema nini, mchambawima ndio alitolea huo mfano.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, hiyo ndio hoja ya Mheshimiwa Ali King hata hapa Bungeni kama kwa mfano mtu akiamua tu kutafuta umaarufu akipanda hapa juu ya

meza ataandikwa na vyombo vyote mbalimbali. Lakini atakuwa ametenda kosa ambalo sio la kawaida lakini alikuwa anatafuta umaarufu, hiyo ndio hoja ya Mheshimiwa King.

Mheshimiwa Spika, lakini Mheshimiwa Agnes Hokororo aliunga mkono hoja kama wenzie. Aliunga mkono hoja zote mbili, lakini akaongelea Kanuni ya 85 ya Kanuni za Kudumu za Bunge za 2020 ambazo zinaongelea utovu wa nidhamu uliokithiri na akazungumzia kwamba hakuna uhuru usiokuwa na mipaka. Na hili ni kweli Waheshimiwa Wabunge hakuna uhuru ambaao ni *absolute* timilifu kabisa, haupo hata kwenye sheria kila uhuru una mipaka yake.

Mheshimiwa Spika, lakini Mheshimiwa Sophia Mwakagenda, ye ye alikwenda zaidi mbali kwa *ku-quote* vifungu mbalimbali vyta Biblia ikiwemo Marko 6, Waefeso 6:12, na akasema hata kwenye Biblia hakuna madhara ya kitu ambacho huamini hata kama utakuwa umepata chanjo, umepata tiba na kitu chochote. Na kwa kuwathibitishia hili wanakamati nadhani mliona kwenye mitandao wakati amekuja Mheshimiwa Josephat Gwajima hata kwenye Kamati kabla hajaitwa, wakati tunamuita alichelewa kidogo. Tukauliza kwa nini anachelewa kuingia wakati tumemuita? Wakasema anaona ameziidiwa ghafla kabla ya kuingia kwenye Kamati ameomba akaletewe dawa kwanza anywe. Kwa hiyo, hata Mheshimiwa Josephat Gwajima anakunywa dawa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, mchangiaji wa tisa alikuwa Mheshimiwa Mariam Ditopile ye ye alinukuu maneno ya Mheshimiwa Rais kuhusu Wabunge kutulia. Ni kweli wako Wabunge wanatafuta *kick* kwa jinsi alivyochangia, lakini *kick* zenyewe za namna gani? Kwa maana nyingine isiwe *kick* ambazo zinaharibu hadhi, heshima ya Bunge na pia kuchonganisha.

Mheshimiwa Spika, lakini pia na suala lingine aliloongelea Mheshimiwa Mariam Ditopile ni hili suala la kwamba Viongozi wetu wamepewa fedha. Kwa kweli hii

imewachanganya sana wananchi Waheshimiwa Wabunge na nyinyi mnafahamu. Wananchi wengi hawachanjwi wengine kwa imani ya kwamba waliochanjwa wamepewa fedha.

Mheshimiwa Spika, sasa maneno haya kama yanatolewa na Kiongozi ni kweli yanawachanganya wananchi na yanaleta kitu ambacho sio utulivu katika nchi. Na kwa suala la Mheshimiwa Jerry Silaa, Mheshimiwa Mariamu Ditopile kasema amesikitishwa na *drama* zake na ule ubishoo ambao alikuja nao kwenye Kamati yakiwemo yale mavitabu aliyokuja nayo rundo.

SPIKA: Ahsante, malizia sasa.

MHE. EMMANUEL A. MWAKASAKA – MWENYEKITI KAMATI YA BUNGE YA HAKI, MAADILI NA MADARAKA YA BUNGE: Mheshimiwa Spika, ingawa uliuliza vile vitabu hakuweza kuvitumia vyote. Aliweza kutumia kitabu kimoja tu Biblia katika lile rundo lote ambalo alikuja nalo. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, na la mwisho ni la Mheshimiwa Elibariki Kingu naye ame-*quote* vifungu vya Biblia na amelaani yote ambayo yamekuwa yakiendelea lakini ameuliza jambo moja Waheshimiwa Wajumbe. Kwamba, je, enzi za Hayati Mheshimiwa Dkt. Magufuli kwa mfano vitu ambavyo anafanya Mheshimiwa Gwajima angefanya? Waheshimiwa Wabunge na hasa akina mama tunaongea mambo ya *gender* na kwamba sisi tunaheshimu *gender*. Katika muda mfupi tu, anatokea mwanaume mmoja tena Mheshimiwa Mbunge, anaanza kuzungumza jambo ambalo hata mtoto mdogo ye yote ambaye ana akili timamu atasema hivi huyu mbona anamdhara mwanamke?

WABUNGE FULANI: Mheshimiwa Spika, ndiyo.

MHE. EMMANUEL A. MWAKASAKA – MWENYEKITI WA KAMATI YA BUNGE YA HAKI, MAADILI NA MADARAKA YA BUNGE: Enhee! ndiyo maana yake, anamdhara mwanamke ndiyo hoja ya Mheshimiwa Kingu! kwamba je, wakati wa

Mheshimiwa Hayati Magufuli angefanya haya? Maana yake kwa nini ayafanye wakati anaetawala ni mwanamke? Hii haikubaliki Waheshimiwa Wajumbe ninawaomba sana, Bunge zima liweze kuridhia maazimio yote mawili kwa ajili ya hizi hoja zote mbili ambazo tumeziwasilisha hapa kwa ajili ya majadiliano ambayo mmemaliza. Nirudie tena kuwaomba Wabunge wote waridhie maazimio yote mawili.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

MHE. SHALLY J. RAYMOND: Mheshimiwa Spika, naafiki.

SPIKA: Hoja imetolewa na imeungwa mkono na Wabunge wengi, tunakushukuru sana Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge, sasa wajibu wangu kabla sijawahoji niseme tu kidogo kwamba kama baadhi walivyochangia mambo haya kimsingi hayakuwa ya kufika hapa yote mawili, tukianza na la Mheshimiwa Jerry Silaa ndiyo kabisa, kwa sababu ni jambo la dakika moja, dakika mbili tu. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, duniani hapa katika mambo ambayo hayamfanyi mtu aheshimike mojawapo ni kuambiwa kwamba huyu halipi kodi, nchi za mashariki Wajapani, Wakorea hata baadhi ya Wachina na nchi zinazozunguka pale, kuonekana umekwepa kodi ni kosa kubwa baadhi anaenda kujinyonga, kwa sababu kwenye jamii inam-taint to the highest order hata kwenye Western World moja ya vitu ambavyo vinaweza kukudharaulisha sana kwenye jamii na ukachukuliwa hatua kali ni kuonekana wewe ni mwepa kodi.

Kwa hiyo, kitendo cha kusema kwamba kundi hili halilipi kodi katika mishahara yao, unawafanya wafanyakazi wote hawa wengine wa-fee/vipi kuhusu Wabunge. Walimu wetu waliopo vijijini huko na wafanyakazi wengine wote wanaskia Wabunge wao mishahara yao wanavuna yote mizima mizima ilivyo haikatwi kodi, ni picha mbaya sana.

Waheshimiwa Wabunge, Wabunge hawa wanahitaji heshima yaani hatujaomba Ubunge ili kuvunjiwa heshima hapana! Wanaheshima zao hawa za aina mbalimbali kila mtu ana heshima yake ya aina yake, lazima mtu ujizue kuvunja heshima za watu wengine kirejareja tu, ni jambo la hovyo sana.

Sasa bahati mbaya limekutoka tunakutarajia wewe yule yule usahihishe, husahihishi kwa hiyo? aah mimi nasema kuna kasehemu, ahaa! kama una hoja yako utajenga kwa utaratibu wako, lakini ulichosema hawalipi, sasa ukisema wanalipa robo, nusu hili suala ambalo halina maana tayari umeshaiharibia jamii na wakati huo walikuwa wanatozwa tozo za miamala, mnaelewa mjadala ulivyoendelea, ni mjadala ambao umewadharaulisha sana Wabunge, kwamba ninyi mnapitisha pitisha mambo tu kwa sababu ninyi hamlipi kodi katika mishahara yetu hatzungumzi kodi zingine. Sasa hili jambo nisingependa kabisa lijurudie ni tabia mbaya.

Bado Azimio hili halijamtaka Mheshimiwa Jerry Silaa aombe radhi kwenye *public*, lakini bado kama Spika namwambia lazima aombe radhi kwenye *public*. Yaani hilo ni lazima, enheee, soma Kanuni vizuri hivi wewe ukijifanya kiburi kwa Spika, wewe Mbunge utafanya kazi wapi? Soma, kila sentensi Spika, Spika, Spika, wewe utajifanya mjanja utapita wapi? (*Makofii/Kicheko*).

MBUNGE FULANI: Mheshimiwa Spika, niulize mimi.

SPIKA: Zaidi ya yote ni Mjumbe wa Kamati Kuu, wengine huwa mnasahau sahau hivi vitu, hatuendi hivyo! Umefanya jambo la hovyo lisahihishe huo ndiyo uungwana ndiyo utu. Ukishalisahihisha yamekwisha wala hakuna anayekutafuta wala anayefanyaje na hili ni funzo kwa wote ukifanya jambo la hovyo, wanasema ukipatikana uko vibaya basi chuchumaa, chutama wanasesma. Kwa hiyo, kwa kijana wetu Jerry Silaa na kwa vijana wengine achene habari ya kuropoka ropoka, kutafuta ujiko ambao hauna mbele wala nyuma, wewe Jimboni elezea mambo ya Jimbo *local politics*, *all politics is local*, wewe zungumzia *local politics* yako huko

na kama ni *national* basi nenda nayo *the correct way.* (*Makofi*)

Jambo la Mheshimiwa Jerry Silaa ni dogo sana ambalo alitakiwa alimalize mwenyewe siku nyingi na tulishamuonya mara kadhaa, sasa najua anaweza akachangua njia ya kuanza kubishana bishana huko nje, aichague, bado tupo hapa hapa, enhee si mna-*passion* vijana mnataka kushindana, kashindane. (*Makofi/Kicheko*)

Waheshimiwa Wabunge, kuhusu Askofu, hapa hatujamshtaki kama Askofu, toka mwanzo hapa tunashughulika, angalia taarifa ya Kamati ni Mheshimiwa Josephat Mathias Gwajima habari ya Uaskofu wake huko huko, na kila mtu ana dini yake hapa na Watanzania hivyo hivyo ni watu wenye nafasi mbalimbali katika madhehebu yetu ya dini tuliyonayo. Unaweza wewe ukawa ni Askofu halafu unawaangalia watu wengine unawaona kama hawaelewi dini au hawahusiani na dini, si hivyo hata kidogo! Hayo ni macho ya makengeza, watu ni waumini sana kwa wakati wao.

Waheshimiwa Wabunge, mimi ni Mzee wa Kanisa, kabisa wa miaka mingi, mimi ni *Lay Canon* wa Kanisa Anglikana Tanzania. Ni nafasi ya Mshauri wa Askofu. Nimeshakwenda mpaka kule Canterbury Makao Makuu ya Kanisa langu, nimeenda kule Nigeria kwa akina TB Joshua nimesali huko, Uyahudi nimekwenda mara nne, nimefika Capernaum kule kwenye Kijiji cha Yesu, Galilaya yote ile nimetembea naijua, Cana naijua, nimefika Nazareth najua unaposema Yusuph alitembea na Mke wake kutoka Nazareth kwenda mpaka Yerusalemu kuhesabiwa na wakakosa mahali pa kulala, kutoka Yerusalemu kwenda mpaka Bethlehem ambako ndipo alipozaliwa Yesu *distance zote zile nazijua na umbali wake na jinsi ilivyokuwa.* (*Makofi*)

Four times I have been there, mara ya mwisho nimekwenda nimefuatana na Mwalimu Mwakasege, kote maeneo matakatifu yale tunayajua, tunatamba sisi? Sasa kwa hiyo ukiwa Askofu utudanganye sisi? Dini tunajua,

tunaifahamu. Tunavyokwenda siyo, kutumia *platform* ya dini kila Jumapili kuhamasisha watu, mnisikilize kesho mtasikia mabomu, mabomu, kesho! (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani upo hapa, jamani Serikali mko hapa, hii haiwezi kwenda hivi enhee, haiwezi kwenda hivi, Mawaziri wenyewe mnashambuliwa, nani anashambuliwa na vyombo nya dola vinasema ahaaa tunasubiri tuone jinai, unasubiri uone uambiwe na nani? Wewe mwenyewe huoni? Sasa Bunge leo tumenawa upilato, nani yule tumenawa kabisa, kwamba sisi na hawa Wabunge wenzetu wanaofanya mambo ya hovyo sisi hatumo, ndiyo kazi tunayoifanya leo hapa. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, sasa wenzetu tunawatarajia kama Wabunge walivyotoa wito, Chama na wenzetu Serikalini kuna kazi ya kufanya, enhee baadhi yako kichwa ngumu ataendelea, sasa akiendelea kwanza Bunge hatutaacha, akiendelea tutaita tena, lakini kwa nini tuhangaike wakati wahusika wapo? Wala hatutamuita Gwajima sasa, enhee akiendelea Bunge hatutamwita Gwajima, mtashangaa tu Waziri wa Mambo ya Ndani Maadili enhee! Mwanasheria Mkuu wa Serikali Maadili, sijui nani anayehusika Maadili, ndipo mtakapoona sasa ile *collision* halisi hapa leo tunanawa, tunawaambia tumechoka hatuwezi kwenda na watu namna hii nchi gani inakuwa hivyo! Enhee tusimuachie Mama peke yake, watu na namna hii haiwezekani. Bunge ndiyo watu wa kwanza tutakao hakikisha Mama anaheshimika nchi hii. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, sasa naomba niwahoji, wanaaoafiki kwamba adhabu zilizopendekezwa na mtoa hoja na Kamati ya Maadili, Haki na Madaraka ya Bunge kwamba sasa zipite.

*(Hoja Iilitolewa lamuliwe)
(Hoja Iliamuliwa na Kuafikiwa)*

SPIKA: Bunge lote limeafiki kabisa adhabu zile. Adhabu hizi zilizotolewa kwa kweli ni *minimal* ni ndogo sana huo ndiyo

ukweli kwa makosa waliyoyafanya ni ndogo sana kwa sababu ni mikutano miwili na mikutano hiyo miwili maana yake na huu unahesabika, *actually* wanakosa Mkutano mmoja tu unaokuja ndiyo maana yaani tunazitoa tu kwa sababu ni wenzetu, ni ndugu zetu tunasikitika ni ndogo.

Waheshimiwa Wabunge, mnajua kwamba Kanuni zetu zinaturuhusu kutoa adhabu ya hadi Mikutano mitatu ambapo wangekosa hata Mkutano wa Bajeti ambaao ni mrefu lakini Kanuni inaturuhusu kutoa hata adhabu nyingine zaidi ya hizo. Tutakuwa tayari kufanya hivyo wakitulazimisha tuelekee huko.

Waheshimiwa Wabunge, kwa kuwa sasa jambo hili limeshatokea Mheshimiwa Josephat Gwajima hayupo, Mheshimiwa Jerry Silaa yupo nafikiri bado yupo enhee? Sasa kwa heshima na taadhima nakuomba utoke nje tutaonana katika Mkutano wa Januari, 2022. Ahsante sana.

Sergeant-At-Arms nakuomba uhakikishe Mheshimiwa anatoka kwa salama, *Sergeant* maana yake ni kwamba mnatoka naye mpaka nje kabisa ya viunga vyta Bunge na katika kipindi hiki ambacho wanakuwa wamesimamishwa na Bunge hawaruhusiwi kabisa kukanyaaga maeneo ya Bunge isipokuwa kwa ridhaa ya Spika, pia watapata nusu mshahara na nusu ya mambo mengine ambayo watakuwa wanastahili kuyapata hizo ndiyo Kanuni zetu zinavyosema.

Hapa (Mhe. Jerry W. Silaa) alitoka Ukumbini akisindikizwa na Sergeant-At-Arms

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, nimalizie kwa kusema si nia yetu kuona kwamba tunafika mahali hapa kwa Mbunge ye yote yule; ushauri wangu ni kwamba unapoona umeteleza na hata wenzako wanakuamba bwana hii njia siyo sawa jitahidi urudi katika mstari hiyo itakufanya uwe na siasa za muda mrefu. Kwa Wabunge vijana, mna safari ndefu ya kwenda usianze kwa mguu wa kushoto, ukianza kwa mguu wa kushoto safari hiyo hautafika, lazima uende vizuri utafika mbali.

Basi kwa kuwa shughuli za leo zimekamilika kama zilivyopangwa, sasa naomba nichukue hii kuahirisha shughuli za Bunge hadi kesho saa Nane kamili mchana.

*(Saa 7.10 Mchana Bunge Lilahirishwa hadi Siku ya Jumatano,
Tarehe 1 Septemba, 2021 Saa Nane Mchana)*